Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 18 Julai, 2013

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo kuamka mzima na mwenye furaha kusubiri kuwasilisha hotuba ya Wizara yangu. Lakini kwanza nakushukuru kunipa nafasi ya kuwa mtu wa mwanzo kwa asubuhi ya leo. Nahisi nilikuwa na wajibu sana wa kuchangia hotuba ya Waziri wetu wa Elimu.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa dhati kabisa kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa jinsi anavyoendelea na juhudi zake katika kuendeleza suala zima la elimu nchini. Ni mtu makini, mtu ambaye anajituma sana. Lakini pia nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa jinsi anavyomsaidia Waziri wake, umahiri wake wa kujibu maswali Barazani umeipatia sifa kubwa sana Wizara yetu ya Elimu.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru sana watendaji wote wa Wizara ya Elimu, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna na Wakurugenzi wote pamoja na Maafisa mbali mbali wanaofanya kazi katika Wizara ya Elimu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Elimu. Tumeona mabadiliko makubwa yakiendelea kufanyika katika Wizara yetu ya Elimu, na haya yanatokana na mashirikiano mazuri ambayo Mhe. Waziri ameyajenga.

Lakini pia nichukue nafasi hii nimshukuru kwa dhati kabisa Makamo Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa SUZA, Profesa Idrissa Rai pamoja na timu yake yote kwa jinsi wanavyosimamia suala zima la elimu ya juu.

Mimi nitazungumzia kidogo suala zima la Sera ya Elimu. Sera ya Elimu watu wengi wameizungumzia hapa na watu wengi wamekosoa na kusema labda umefika wakati sasa hivi kufanya mapitio ya Sera yetu ya Elimu. Tukumbuke kwamba Sera hii imetayarishwa na ikapitishwa kwenye taasisi zetu mbali mbali za Kiserikali na Baraza hapa ikapata baraka zake mwaka 2006. Sera hii iliandaliwa na watu makini sana, Mwenyekiti alikuwa ni Dokta Bilal, Mhe. Juma Duni, Mhe. Ali Juma Shamuhuna na wasomi mbali mbali wakaiandaa sera ile.

Mimi nadhani tusione kwamba Sera ina kasoro, inawezekana na wakati umefika kwa sababu mwaka 2006 pengine mwakani au baada ya miaka miwili ni wakati muafaka kuifanyia mapitio sera ile itakuwa imetimiza miaka 10. Lakini tuangalie tatizo ni la Sera au kuna mambo ndani yake. Kwa sababu sisi sote tuliokuwemo humu ndani kwa njia moja au nyengine ni *product* ya mitaala ama hiyo iliyokuwepo sasa hivi ambayo inabadilishwa kidogo tu ile iliyokuwa ya nyuma. Maana ndio tumo humu ndani tunawasilisha, tunazungumza vizuri na dunia inatambua.

Mhe, Naibu Spika, Wafunzi ambao wanakwenda nchi za nje kusoma kutoka Zanzibar asilimia 95 mpaka 96 wanafanya vizuri sana kupita wanafunzi wengi duniani na wametokana na sera hii hii ambayo leo Waheshimiwa wanapendekeza iangaliwe. Si jambo baya ili kuifanya iwe ni bora zaidi ni vizuri kuja kuiangalia, lakini tukumbuke kwamba elimu ya Tanzania Bara na hapa Zanzibar pamoja na matatizo yaliyokuwepo lakini bado tupo katika kiwango kinachokubalika kimataifa. Taasisi ile inayofanya utafiti kwa ubora wa elimu kwa nchi hizi za Kusini, Mashariki ya Afrika, imetoa katika ripoti yake na ikaonesha jinsi gani Zanzibar hasa katika elimu ya msingi inavyopiga hatua kubwa katika kuleta marekebisho makubwa.

Pia kuna suala zima katika mitaala hiyo wakazungumza baadhi ya Waheshimiwa kwamba vitabu havitambulikani, kila siku vinabadilishwa. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa kwamba Wizara ya Elimu vitabu ambavyo vinatumika ni vitabu ambavyo zinakubalika katika Baraza la Mitihani NACTE, lakini pia ni vitabu ambavyo vimetayarishwa kwa umahiri mkubwa na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha South Carolina cha kule Marekani. Vitabu hivi ni vya Sekondari kuanzia *form I* mpaka *form IV* na vyengine vya *form V* na *form VI* pia vilitafutwa kwa lengo la kukidhi mahitaji ya mitaala yetu.

Tusihukumu haraka haraka tukaona labda kutokana na matokeo haya kuwa mabaya kwamba labda kuna kosa la mitaala. Hakuna lolote, mambo ya kawaida kabisa yanatokezea, sawa sawa na bahari maji kujaa na kupwa. Miaka ya nyuma tulishuhudia vile vile matokeo yakawa mabaya, siku

nyengine yanakuwa mazuri, ndio watu wanajipanga. Jana nilimsikia Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi akisema hapa kwamba Wachina wana msemo wanaosema *ili kufika hatua elfu moja lazima uanze na hatua moja*. Tumpe moyo Waziri, tuzidi kumsaidia ili kuhakikisha kwamba elimu hii inapiga hatua ni moja katika Wizara ambayo ni nyeti kabisa.

Tujiridhishe kwamba Sera iliyokuwepo inawezekana ikawa na kasoro za hapa na pale. Bado tuamini kwamba sera ile imetayarishwa na magwiji wa elimu hapa Zanzibar na imepata baraka za wataalamu kutoka sehemu mbali mbali. Hata wafadhili wetu wa Shirika la Maendeleo waliisifu sana Sera ile ya Elimu. Mimi nadhani tatizo sasa kama wewe unavyopata mtoto mchanga unakuwa naye kila wakati huoni kama anabadilika, lakini anapokuja mtu mwengine anavyomuona yule mtoto anakwambia mtoto huyu kasi yake ya kukua ni nzuri na anakuwa mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala hili la maandalizi kwenye Sera ile ya mwaka 2006. Sera inasema elimu ya maandalizi itakuwa miaka miwili, elimu ya msingi miaka sita na elimu ya Sekondari miaka minne.Wengi wakasema ingefaa tukaanzisha kuwa na Chuo cha Maandalizi ya Ualimu. Ni wazo zuri sana lakini sera ile inapotwambia tujitayarishe kuwa na elimu ya maandalizi miaka miwili, *primary* miaka sita, sekondari miaka minne. Kuna hatua nyingi inabidi zipitiwe.

Hivi saa nadhani sina hakika nimeondoka kama miaka miwili iliyopita na nusu Wizarani. Nina hakika kuna darasa ambalo lilianza na utaratibu wa utekelezaji wa Sera hii ya Elimu, kama halitokuwa darasa la nne sasa hivi basi itakuwa ni darasa la tano. Serikali sasa hivi ipo kwenye *transition*, kwenye mfumo huu wa sera mpya. Nina hakika baada ya miaka miwili vijana wale pengine watafika darasa la sita au mwaka mmoja watafika darasa la sita na hatimaye kuingia *form I* moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimpe ushauri Waziri katika suala hili ambao Waheshimiwa wengi walikuja na mapendekezo ya kuanzisha Chuo cha Ualimu. Kwa vile SUZA inatoa mafunzo ya ualimu katka ngazi ya digirii, kama itawezekana kwa SUZA yenyewe, iandaliwe programu maalum ndani ya *SUZA* za wale walimu ambao wanafundisha elimu za mandalizi na hata ya msingi ili wapate ile *dose* yenyewe au ile taaluma yenyewe ya elimu ya Maandalizi kwenye Chuo Kikuu.

Imani yangu endapo SUZA watashirikishwa kikamilifu katika suala hili la kuandaa programu, mimi nina hakika wanaweza wakaandaa programu hata za miezi mitatu au sita na hatimaye walimu wetu hawa wakapata elimu ya kutosha. Elimu ya maandalizi ni ya msingi kabisa, imani iliyojengeka kwa

wengi ni kweli, vijana wetu waliopita elimu ya maandalizi basi wao huwa wanafanya vizuri zaidi kuliko wale ambao hawakupitia maandalizi.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri kwa hatua yake ya kutembelea kwenye Mikoa na kuzungumza na walimu Wakuu. Walimu wengi Wakuu wamefurahia na wanapongeza hatua ile. Namuomba sana Mhe. Waziri ziara hizi ziendelee kwa kushirikiana na Naibu Waziri wake, ziara ziendelee kwa sababu zina faida kubwa. Ziende zaidi ya hapo kukutana na walimu Wakuu, kukutana na walimu katika Wilaya. Pia kama muda utaruhusu pia kukutana na wale wanafunzi ambao wanafanya mitihani. Nina hakika kabisa kwamba hiyo itasaidia.

Mhe. Naibu Spika, limezungumzwa suala la ubora wa elimu. Tuangalie kuna sekta nyingi sana lakini moja naweza kusema ni tatizo ni utandawazi. Vijana wetu au wanafunzi wengi kutoka darasa pengine la tano, la sita na hata watoto wadogo mpaka Sekondari, kabla ya kuchukua muda wa kudurusu masomo yao basi wanatumia simu muda mwingi zaidi kuliko wakati mwengine wowote.

Simu Wizara ya Elimu ilipiga marufuku matumizi ya simu kwa wanafunzi. Nina hakika marufuku ile bado inaendelea na naomba iendelee. Simu zinatuletea matatizo makubwa sana kwa watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika, kuna wakati baada ya kupiga marufuku wakati ule Mwalimu Mkuu akakamata simu mbili ndani ya darasa kwa mwanafunzi wa *form I*, zikaletwa Wizarani. Mhe. Naibu Spika, huamini mambo yaliyokuwemo ndani ya simu ile, maisha yetu hatujayaona. Lakini watoto wanayo na wanatizama wakati wa kusoma wao wanatizama simu. Mimi naomba sana tusaidiane hili jambo ni letu sote suala hili la watoto. Wazee pia waache tabia ya kuwapa simu watoto wao, kama jamii haijasaidia tutalaumu kila siku.

Tuition zilipigwa marufuku, nina hakika kwamba zinaendelea kupigwa marufuku, tuliweka mwisho saa mbili, athari zake zikaonekana. Kama kutakuwa na uwajibikaji wa kutosha ndani ya skuli basi *tuition* hizi zinaweza zikasaidia tu lakini hazitokuwa na umuhimu mkubwa sana. Ni lazima walimu waendelee kufanya kazi.

Mwisho Mheshimiwa naomba ombi maalum kwa Mhe. Waziri na Wizara kwa ujumla. Mhe. Waziri ombi langu, wananchi wa Jimbo la Makunduchi wamenituma na mimi nafikisha salamu zao. Kwanza wanapongeza ziara uliyofanya kwa kukutana na walimu Wakuu, lakini kwa bahati wazee

wenyewe hukukutana nao. Sasa nakuomba kwa heshima kabisa na taadhima najua mimi na wewe tukiombana huwa tunapeana, tunasaidiana.

Mhe. Waziri historia bado inaendelea na naomba tuiendeleze. Nakuomba sana ufanye ziara maalum ya kutwa nzima wewe Naibu Waziri wako na watendaji wote wa Wizara kwanza tuzitembelee taasisi zilizokuwepo katika Jimbo la Makunduchi na baadaye tufanye mkutano nao, ili wananchi wa jimbo la Makunduchi na wao wana mawazo ya kusaidia japo kwa moja au mawili. Lakini pia kubadilishana mawazo na kusikia busara na hekma kutoka kwako wewe. Naomba sana Mheshimiwa ombi hili, sisemi mara baada ya kumaliza bajeti hii lakini jitahidi ikiwezekana kabla ya mwisho wa mwaka huu *Inshaallah* tutafute wakati ili tufanye ziara hiyo.

Pia namuomba Waziri la mwisho naomba ile skuli ya Miwaleni basi nayo kazi iliyobakia si kubwa sana, tuikamilishe ili watoto wale waanze kupata elimu yao.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi naiunga mkono bajeti hii hotuba ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja na naomba Waheshimiwa wote tuiunge mkono hotuba hii kwa sababu ndio itakayotuletea mwanga na maendeleo makubwa katika nchi yetu. Mheshimiwa nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha asubuhi hii ya leo kuja katika Baraza hili tukufu na kuweza kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar. Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Tumbatu naomba kutoa maoni yangu kwa maana ya kusaidia kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote kwa kuandaa kitabu ambacho kimejaa mambo mengi sana ya kitaalamu na kueleza hali halisi ya elimu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niingie katika maeneo mawili makubwa na baadaye niingie katika Jimbo langu la Tumbatu. Kama nilivyosema mwanzo nipo hapa nikiwa Waziri lakini nipo kwa niaba ya kuwawakilisha wananchi wa Jimbo langu la Tumbatu.

Mhe. Naibu Spika, eneo kubwa ambalo limezungumzwa na Wajumbe wengi sana na hata tumemuona Mjumbe wetu mmoja ambaye si aghalabu kusema kwa sauti kubwa sana lakini juzi nimemshuhudia akisema kwa sauti kubwa

sana naye ni Mhe. Viwe. Kuhusu suala la ajira ya walimu. Nataka nichukue nafasi hiyo kwanza kumpongeza Mhe. Viwe lakini pili kuwapongeza Waheshimiwa wengine ambao wamelizungumzia suala hili kwa upana zaidi.

Nataka niseme kwamba suala la tatizo la ajira kwa vijana wetu, sio eneo hili tu la walimu hata katika maeneo mengine ni kubwa sana. Ndio maana serikali ikaja na njia nyengine mbadala ya kuweza kutoa nafasi za ajira katika sekta binafsi na sekta nyengine za kujiajiri wenyewe. Tuliona kwamba kwa kutegemea tu kuwaajiri vijana katika sekta ya umma hilo ni jambo ambalo haliwezekani hapa Zanzibar lakini haliwezekani katika nchi nyengine yoyote ile duniani. Kwamba kila anayemaliza kusoma, anayepata elimu, anayesomeshwa aajiriwe na serikali. Ni kweli ni jukumu la serikali kuhakikisha kwamba wananchi wake wanaishi katika maisha bora.

Nataka niseme kwamba tatizo hili la ajira ya walimu limezungumzwa na wachangiaji wengi. Sisi kama Wizara ya Utumishi wa Umma kwa mjibu wa sheria ya utumishi wa Umma kila mwaka tunakuja na mpango wa orodha ya nafasi mpya za ajira zilizokubaliwa kwa mujibu wa sheria. Hili kwa nini linakuja? Linakuja kwa sababu kuepusha hayo mambo ambayo mtu pengine anaweza akaajiri anavyotaka yeye bila ya kuzingatia uwezo uliopo wa serikali. Tuna mpango huu tunasema ni mpango wa orodha ya nafasi mpya kwa mwaka wa bajeti husika.

Kwa mfano mwaka huu wa bajeti kuna nafasi 2400 na zaidi mwaka jana tulikuwa na nafasi 2552 mwaka huu tuna nafasi 2410 za ajira ambazo tutaajiri wafanyakazi mwaka huu. Yoyote yule Mkuu wa Taasisi anapohitaji ajira lazima afuate mpango uliopo hapa, hawezi kufanya vyenginevyo. Kwa sababu hawa ambao wamekubaliwa ndio fedha zao zilizotengwa katika kasma nzima ya mishahara ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2013/2014 na wale wa mwaka jana walitengwa kwenye bajeti ile ya mwaka jana. Tunaweza tukawa na vijana wengi wanaohitaji ajira lakini vijana hao itabidi lazima wazingatie mpango maalum wa serikali ambao umezingatia uwezo wa kuwaajiri vijana kwa mujibu wa hali halisi ya fedha ilivyo.

Kwanza nataka nieleze hivyo. Mwaka jana tulitangaza nafasi za walimu wa digirii ya sayansi. Tume ya Utumishi Serikalini imetangaza nafasi za ajira za walimu wa digirii na diploma ya sayansi mwezi wa Oktoba 2012, na tulipokea maombi 712. Maombi tuliyoyapokea kwa Unguja na Pemba ambapo katika ajira hiyo kibali cha ajira ya ualimu kwa Unguja ni 323 na kwa Pemba 144. Hawa ndio tuliowapata, tungehitaji kupata wengine zaidi walimu wa sayansi wa digirii ya kwanza na diploma lakini kwa tuliowapata ni hawa 323 kwa Pemba 144.

Tume ya Utumishi serikalini ilitangaza tena nafasi ya ajira ya walimu wa sayansi wa digirii na hesabati na kupokea jumla ya maombi 54 tu ambapo walimu wote wakapewa kibali cha kuajiriwa. Nasema wangejitokeza zaidi wengine tungewaajiri. Lakini kwa sababu hawapo tuliwaajiri hawa ambao tumewapokea. Tume ya Utumishi Serikalini ilitangaza ajira ya walimu wa maombi ya Pemba ilikuwa 2374 na kwa Unguja 7805. Nafasi zenyewe zilikuwa ni 150, lakini tulipokea maombi zaidi ya elfu kumi. Sasa kama una nafasi 150 umepokea maombi zaidi 10,000 kwa vyovyote vile hata wangu miye nisingempatia.

Maana Mhe. Viwe alisema pengine mtu wake hakuchukuliwa. Hata angekuwa wangu mimi angeachwa kutokana na ufinyu wa nafasi, huo ndio ukweli wenyewe ulivyo. Tunapopokea sisi maombi ya ajira tunatengeneza *short list* ya walimu. Kwa mfano kama walimu 150 wa cheti tulipeleka zaidi ya watu 150 lakini Wilaya zenyewe zilitakiwa zieleze mahitaji katika maeneo hayo. Kwa mfano Tumbatu, kuna upungufu wa walimu gani jambo ambalo Tumbatu hakuna kwa sababu kwa taarifa yetu walimu sasa tunapeleka maeneo mengine, kule Tumbatu hakuna shida kabisa ya walimu.

Nataka nitumie nafasi hii kuwahamasisha Waheshimiwa Wajumbe ambao wana visiwa, wawashajihishe vijana wao waweze kusoma masomo ya sayansi na masomo mengine ili tatizo la visiwani liweze kuondokana. Visiwani kuna mazingira maalum, unapomtoa mwalimu kutoka Makunduchi kwa hivi sasa ukampeleka Tumbatu, inaweza ikampa shida. Lakini kama mwalimu anatokea pale pale Tumbatu ambapo mazingira yale keshayazowea inakuwa rahisi sana kuweza kumuajiri. Sheria yetu hii inazingatia hilo.

Kwa mfano Kojani kwa Mhe. Hassan Hamad Omar, kuna vijana wa Kojani ambao wamesoma na wana sifa za kuajiriwa, basi Tume itazingatia kuwachukua wale waliokuwepo kule kisiwani kwa sababu ya mazingira maalum. Lakini katika maeneo mengine hiyo itategemea wale wataalamu ambao wamejitokeza.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme ajira hazitolewi kwa upendeleo isipokuwa liliopo ni kwamba sisi tukishapata tukishakuwa na nafasi 150 tunapeleka orodha ya watu 2000 Wizara ya Elimu wao wanaangalia mahitaji yao, mahitaji yao ni wapi na wapi. Pengine mtu kaomba Tumbatu lakini pengine Tumbatu hakuna nafasi, yule aliyeomba Tumbatu hata kama ana sifa lakini nafasi inayotakiwa ni ya Kisiwapanza atapewa yule wa Kisiwapanza kwanza. Hiyo haiwi ya upendeleo inakuwa kwa sababu wewe umepewa fursa ya kuomba na ukachagua skuli ambayo unataka kusomesha. Inapotokea ile nafasi ambayo umeichagua wewe ya skuli unayotaka kuisomesha haipo maana yake sio kwamba umeonewa ni kwamba mahitaji katika skuli au katika

eneo ulililoliomba hayapo, yapo katika maeneo mengine ambayo wenzako wameomba.

Labda niseme kwa kipindi kijacho tutahakikisha hata yale matangazo tunapoyatangaza tutasema, kwamba tunatangaza nafasi tatu za walimu wa sayansi katika skuli ya Makoongwe kwa hiyo mtu uombe Makoongwe. Tunafanya hivyo kwa sababu mara nyingi tumekuwa tunawaajiri walimu halafu ukishawaajiri wanaomba uhamisho wanakwenda kufanya kazi katika maeneo mengine. Ili tupunguze tatizo hili la upungufu wa walimu kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo tutazingatia hilo.

Nataka niseme Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka huu wa fedha Wizara ya Elimu imepanga kuwaajiri watu 542. Hawa watu mishahara yao itatumia karibu milioni 167 kwa mwezi, na kwa mwaka watatumia bilioni 2 na milioni 12. Huwezi tena ukaja ukatoka katika mpango huu ukaamua tu kuajiri kwa sababu waliopo ni wengi hawajaajiriwa, hatuwezi kufanya hivyo. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wawakilishi kwamba tunapiga kelele hapa kuwambia wenzetu kwamba tunafanya kazi kwa mazowea.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme Wazanzibari wote tuondokane na mazowea tuliyoyazowea huko nyuma, tuondokane na hayo, sasa tunakwenda kwa mujibu wa *plan* zetu tunazoziweka na kwa mujibu wa uwezo uliopo wa serikali wa kuweza kuwaajiri Wazanzibari, kwa mwaka huu tutaajiri watu elfu mbili na kitu, maana yake tutaajiri hao, hatutaajiri watu 3000 wala 5000. Lakini kama ninavyosema hawa vijana wa *certificate* waliopeleka maombi ni 10000, lakini nafasi zilizokuwepo kwa mahitaji yaliyokuwepo ni watu mia moja hamsini.

Na hivi ninavyozungumza kuna nafasi hamsini katika nafasi za Wizara ya Elimu za mwaka unaomalizika tumeshindwa kuzijaza kwa sababu hatuna watu wenye sifa, watu wa sayansi na watu wenye *geography* hawapo, lakini kama wapo nasema tena natoa *challenge* kama wapo watu wa namna hiyo niletewe sasa hivi nitawaajiri.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu bado tuna upungufu katika skuli zetu watu wa *geography*. Unaweza ukawa una watu wa *geography*, kwa sababu kinachofanyika nini? Watu wengine wamekosa kuajiriwa kwa sababu vyeti vyao havikukamilika, kuna walimu hata wangu mimi kutoka Tumbatu wamepata *supplementary* pale vyuoni hawakusapua kwa lugha nyepesi mnaweza mkasema, hakuwa- *supplement*, kwa hiyo hawa hata kama ana cheti, kile cheti hakijakamilika. Sasa hao wapo wengi sana, hawa hawawezi kuajiriwa lazima wakamilishe utaratibu uliopo nasema hata kwangu Tumbatu wapo wanafika 30, lakini kwa sababu mimi Waziri wa Utumishi na mtu hana

sifa, hakukamilisha nimuajiri kwa sababu anatoka Tumbatu? Hilo haliwezekani katika utaratibu wetu wa sasa na sheria yetu hii imeweka wazi kwamba uajiri wowote utafanywa kwa uwazi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 57 kinasema kila Taasisi ya Utumishi wa Umma inaweza kuajiri idadi ya watumishi kwa mwaka wa fedha wowote kulingana na mpango wa mwaka wa rasilimali watu baada ya kitendo cha kuwapata watu kujaza nafasi kilichofanywa na Tume ya Utumishi husika, mpango wenyewe ndio huu niliouleza. Humu katika *nominal roll* ya Wizara ya Elimu kuna walimu ambao wamesema watawaajiri, walimu wa *degree* ya sayansi, wataajiri katika kipindi cha mwaka huu walimu 85, walimu wa sayansi *degree* ya kwanza watawaajiri katika mwaka huu.

Sasa hawa kama wapo tutawaajiri, lakini huwezi kuichukua nafasi ya mwalimu wa sayansi ukaenda ukamuajiri mwalimu wa *Art* haiwezekani, kwa sababu mahitaji yetu ni walimu wa sayansi na sisi hapa tunapiga kelele, lakini Wizara ya Elimu hii itaajiri walimu wa Diploma 166 katika mpango wao wa mwaka huu wa sayansi, huwezi tena nafasi 151 ukaenda ukaajiri walimu wa *Art*, haiwezekani, lakini itaajiri walimu wa *Art* pale ambapo inaonekana haja ya kufanya hivyo ipo. Kwa hiyo Waheshimiwa Wajumbe lazima nataka hili lieleweke.

Mhe. Naibu Spika, bado ninasema kuna nafasi 50 za walimu wa sayansi na walimu wenye sifa za *geography* kwa kazi ya *Degree* na *Diploma* kama wapo na wakishathibitishwa vyeti vyao na Wizara ya Elimu kwamba vyeti hivyo ni halali nitawaajiri kesho.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nilisema ni kwamba sheria hii hii inasema kama kuna mtu hakuridhika na masuala ya uajiri kifungu cha 57 kifungu kidogo cha 6 kinasema: Kamisheni ndani ya muda usiozidi miezi 3 tokea uajiri kufanywa inaweza kuchunguza au kuamuru uchunguzi wa utaratibu wowote wa uteuzi wa uajiri kwa matakwa yake yenyewe au baada ya kupokea malalamiko yaliyopelekwa kwake, na uchunguzi utakapokamilika Kamisheni inaweza kutoa maelekezo yoyote inayoyaona yanafaa.

Mhe. Naibu Spika, nitoe wito. Kama kuna mtu kahisi kaonewa katika ajira hii tufuate utaratibu. Tupeleke malalamiko Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Kamisheni itachunguza na ikibainika kwamba huo uajiri umetolewa kwa upendeleo uajiri utafutwa, utasitishwa ndani ya miezi mitatu. Sheria hii Waheshimiwa tumeipitisha sisi, tuiseme hii sheria ya utumishi wa umma kama kuna mtu yeyote yule kaomba ualimu lakini anahisi kaonewa hakufanyiwa haki si kwa sababu ya ufinyu wa nafasi apeleke malalamiko Kamisheni yatashughulikiwa na hatimaye taratibu za kisheria zitafuatwa.

Sasa nataka niseme hili tatizo la ajira ni kubwa kwa sababu ya udogo wa nafasi ziliopo almuradi tu tufuate sheria.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano unaweza ukasema skuli kapelekwa mwalimu mmoja tu wa sayansi, haina maana kwamba kule kwenye skuli hakuna walimu wengine wa sayansi, pengine huyo mwalimu ndiye aliyepatikana, lakini kama wapo wengine nawashajihisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika maskuli yao kama wanao walimu wa sayansi na shida ya walimu wa sayansi ipo watuletee, tunaye huyu mwalimu wa sayansi na katika skuli yangu kuna upungufu wa walimu wa sayansi watuletee, watuletee ili tuweze kufuata utaratibu tuweze kuwaajiri.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka niliseme kuhusu suala la maposho ya Walimu Wakuu na watu wengine ambalo limezungumzwa na Wajumbe. Nataka niseme kwamba walimu wakuu na walimu wasaidizi na wengineo kila anayestahiki kupata posho naomba nitoe taarifa kwamba kuanzia mwezi huu wa Julai walimu hawa wakuu wataanza kupata maposho yao na viwango vya maposho vimebadilika kutoka posho la zamani ambalo hakuwa analipata mwalimu mkuu na wale wengine ambao wameombewa maposho yamebadilika kutoka kiwango kile ambacho kilikuwepo mwanzo na sasa tuna kiwango kipya, na Waheshimiwa Wajumbe wakitaka orodha hii nitawapatia kwamba hilo tayari limeshamalizika.

Mhe. Naibu Spika, lakini kulijitokeza suala jengine la walimu wale ambao wameendelezwa kwenye masomo ya sayansi. Ni kweli maombi yameletwa kwetu, kuna wale na kuna walimu wa *UPE*, zamani walimu wa *Form* III walikuwa wanaajiriwa. Nataka nichukue nafasi hii kusema niwapongeze sana wale walimu wa *Form* III ambao wamejiendeleza mpaka kufikia kwenye *Level* ya *Degree* ya kwanza hivi sasa na wale wanazingatiwa katika kulipwa malipo yao kwa mujibu wa viwango vyao vya elimu kama mfanyakazi mwengine yeyote yule ambaye analipwa. Lakini kuna wale walimu ambao hawakujiendeleza katika mwaka huu tutatumia karibu milioni mia tano na kitu kwa ajili ya wafanyakazi wote ambao hawakujiendeleza kielimu, lakini wana *experience* na wanafanya kazi vizuri hawa watakuwa *senior assistance* katika maeneo tafauti, *scheme of service* ya Wizara ya Elimu ipo tayari na hao watazingatiwa katika kupewa maslahi yao katika bajeti ya mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme katika bajeti ya mwaka huu kuna karibu milioni mia tano kwa ajili ya kuwazingatia watu kama hawa ambao hawana *qualification* lakini wamefanya kazi katika kipindi cha muda mrefu katika Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini kuna wale walimu ambao wameendelezwa kwenye masomo ya sayansi, wale walimu vile vile watazingatiwa na watapata maslahi yao katika bajeti hii ya mwaka wa fedha

2013/14 na kama nilivyosema kwamba mazingatio ya mishahara yanafanywa hivi sasa na mara tu baada ya kukamilika basi kila mmoja anayestahiki kupata haki yake atapata haki yake. Na napenda nitoe taarifa na ahadi kwamba kila yule ambaye amezungumzwa hapa Baraza la Wawakilishi tutawaletea si kwa maana ya kutoa taarifa kwenye *public* lakini tutawaletea Waheshimiwa Wawakilishi ule utekelezaji wa mambo ambavyo yamekwenda juu ya yale maombi ambayo yameletwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hasa yanayohusu masuala ya maslahi ya watumishi wa umma.

Baada ya kwisha kusema hayo Mheshimiwa sasa niache kuzungumzia suala la Wizara na niende sasa katika kuwatetea wananchi wa Jimbo langu la Tumbatu. Mhe. Naibu Spika, kwa uchache sana nataka niseme katika Jimbo langu yapo majengo mengi sana ya skuli ambayo yamejengwa na yapo majengo ambayo sasa hivi ni chakavu sana. Nilikuwa naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amani kama alivyosema Mhe. Haroun hapa ifanye ziara katika Jimbo langu na mimi mwenyewe nitakuwa tayari kushirikiana nao kwenda kuona hali halisi ya miundombinu ya majengo ya skuli yale yaliyokuwa chakavu na yale ambayo tayari sisi kama wananchi tumeshafika hatua na sasa jukumu hilo ni la Wizara ya Elimu au serikali kwa jumla, nitaomba sana hilo jambo lifanyike ili kuondosha kadhia ya watoto kusoma katika mikono ya skuli kule katika Jimbo la Tumbatu kwa jumla. Katika Jimbo la Tumbatu katika Wadi ya Mkokotoni na kule kisiwani Tumbatu.

Mheshimiwa baada ya kwisha kusema hayo si machache sana lakini naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia 100. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha leo kufika hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa wazima wenye afya na tukikaribia kumaliza kumi la mwanzo, Mwenyezi Mungu atujaalie atutakabalie saumu zetu na atupe kila la kheri lenye mafanikio duniani na kesho akhera.

Pili Mheshimiwa nikushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kumsaidia Mhe. Waziri kuchangia baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu walitaka kujua ndani ya Wizara yetu kinachotendeka. Niwashukuru kwa dhati kabisa na mimi Mheshimiwa niwaahidi kadri ya Mwenyezi Mungu atakavyotujaalia kwa maslahi ya nchi yetu, hoja Mhe. Naibu Spika, ni nyingi tumepata wachangiaji karibu 30 ambao wamesimama na kuzungumza lakini wachangiaji 12 wa maandishi. Nadhani ni Wizara ya kwanza kupata karibu wachangia 42 na hoja zao ni hoja nzito. Kwa hivyo namuomba Mwenyezi Mungu atusaidie mimi na Mhe. Waziri wangu atupe uwezo wa kuweza kuwatosheleza Wajumbe wako wa Baraza tukufu hoja hizi.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuchangia kwa kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, niwashukuru sana Mheshimiwa kwa jitihada yao wanayochukua katika kufanya kazi zao siku hadi siku katika Wizara yetu na ushauri ambao wanatupa tunauchukua na tunauthamini sana na haya ambayo wameyazungumza. Mhe. Kamati ilijikita zaidi katika maeneo yafuatayo. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, bodi ya huduma ya Maktaba, Idara ya Elimu ya maandalizi na msingi na elimu mjumuisho pamoja na miradi ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba majengo ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa elimu yapo katika hali mbaya na pia zina nafasi ya kutosha kwa wakaguzi waliopo. Lengo la Wizara ni kujenga jengo jengine kwa ajili ya Idara zetu zilizopo katika maeneo ya Makao Makuu ya Wizara na ile ambazo ziko Pemba. Tatizo ni ukosefu wa fedha lakini michoro tayari tumeiandaa kwa hivi sasa Wizara itafanyia matengenezo Ofisi ya Mkaguzi Mkuu ya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, tunaelewa kwamba Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa elimu ni chombo muhimu katika maendeleo ya elimu na ndio maana chombo hiki kimekuwa chombo kinachotegemea na kupata ruzuku na matumizi ya kawaida. Kama tulivyosema katika hotuba ya bajeti, Wizara imepitia mfumo wa ukaguzi na ina mpango wa kutayarisha sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu itakayoambatanisha muundo mpya wa ukaguzi wa elimu ambao utaleta ufanisi katika kusimamia utekelezaji wa elimu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la Maktaba. Wizara imechukua ushauri uliotolewa na kamati ya kuanzisha maktaba katika maktaba za Wilaya na tutaendelea kushajihisha wananchi kuanzisha maktaba katika Wilaya na katika shehia au mitaa. Bodi za huduma za maktaba pia itaendelea kununua vitabu kwa ajili ya maktaba pamoja na kutafuta wafadhili watakaotusaidia kutupatia vitabu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Maktaba Kuu Pemba, mkandarasi ameshapatikana na kakabidhiwa eneo la ujenzi na anategemea kuanza ujenzi huo mwishoni wa mwezi huu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu elimu ya maandalizi kwa Zanzibar ni kweli hakuna chuo maalum kinachofundisha walimu wa maandalizi lakini tuna vituo vya walimu wa maandalizi viwili Unguja na Pemba ambavyo vinatoa mafunzo kwa walimu wa maandalizi ni Saateni Unguja na Chachani kwa Pemba. Hata hivyo kuna walimu ambao wanachukua diploma na shahada ya kwanza katika

vyuo vikuu vya Tanzania Bara na hivi karibuni walimu watatu walipata shahada ya kwanza ya elimu ya maandalizi wamemaliza masomo.

Wizara ina mpango wa kuanzisha masomo ya Diploma ya elimu ya maandalizi katika vyuo vyetu vya Ualimu. Pia Wizara inatayarisha *module* ya masomo ya ualimu wa maandalizi ambayo itatolewa kwa njia ya redio na kupitia katika vituo vya ualimu kwa walimu. Mhe. Naibu Spika, vyuo vya kur-an vinasimamiwa na ofisi ya mufti, kazi kubwa ya wizara ni kutoa mafunzo kwa walimu wa madrasa ya vyuo vya *qur-an* ili kuhakikisha inatoa elimu inayotakiwa. Hata hivyo tutashirikiana na Ofisi ya Mufti kuangalia namna gani ya utoaji wa elimu katika vyuo vya *qur-an* na madrasa inaweza kuisaidia na kuimarika.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu upungufu wa walimu katika skuli za msingi hasa katika mikoa ya Pemba, serikali itaendelea kuajiri walimu wa skuli za msingi. Hivi sasa Wizara imo katika hatua za kuajiri walimu 75 wa cheti kwa ajili ya skuli za Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu walimu wanaofundisha katika vituo vya Amali. Wizara imeamua kuongezea posho la kufundishia kuanzia mwezi wa Julai, 2013 kufikia 30,000. Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru tena Mwenyekiti wa Kamati na kuwahakikishia kuwa maoni ya Kamati tunayafanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna Waheshimiwa ambao walichangia na ni wengi karibu kumi na moja kuhusu mitaala. Mhe. Abdalla Juma wa Chonga, Mhe. Mohammed Haji Khalid wa Mtambile, Mhe. Mgeni Hassan Juma wanawake viti maalum, Mhe. Suleiman Hemed Khamis wa Konde, Mhe. Saleh Nassor Juma wa Wawi, Mhe. Abdalla Mohammed Ali Mkoani, Mhe. Salim Abdalla Hamad Mtambwe, Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mji Mkongwe, Mhe. Asha Bakari Makame viti maalum, Mhe. Ashura Sharif viti maalum, Mhe. Salmin Awadh Jimbo la Magomeni.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya Mhe. Abdalla Juma Abdalla na Mhe. Abdalla Mohammed Ali na Mhe. Salim Abdalla Hamad na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Asha Bakari, Mhe. Ashura Sharif na Mhe. Salmin Awadh, walitoa ushauri wa kubadilisha mitaala ili iweze kuwasaidia wanafunzi baada ya kumaliza elimu ya lazima na kuangalia idadi ya masomo kwa elimu ya msingi pamoja na muelekeo wa wanafunzi katika kujifunza. Ni ushauri mzuri Mhe. Naibu Spika, na Wizara yangu inauchukua na kuufanyia kazi.

Hoja ya Mhe. Mohammed Haji Khalid katika ngazi ya elimu ya sekondari sote tunatumia mitaala mimoja Tanzania nzima hakuna tofauti ya muhtasari wa masomo baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Saleh Nassor Juma elimu ya maandalizi kwa walimu kwa wanafunzi inayo mitaala rasmi kwa upande wa mafunzo ya walimu na wa maandalizi, Wizara yangu imeanza hatua ya awali ya kuandaa mitaala kwa ajili ya kuwafundishia walimu wa maandalizi katika vyuo vya walimu. Aidha muhtasari wa somo la michezo tayari umeandaliwa kwa mwaka 2009 na ulianza kutumika kwa mwaka 2010 katika skuli zetu zote za msingi Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya Mhe. Suleiman Hemed Khamis Skuli za Zanzibar zinazo mihutasari ya kufundishia. Aidha kwa upande wa vitabu ngazi ya sekondari kuna vitabu vya kutosha na kwa upande wa elimu ya msingi Wizara yangu iko katika hatua ya kuchapisha vitabu vya darasa la kwanza mpaka la nne kwa masomo ya sayansi, sayansi jamii, hesabati, Kiswahili na Kiingereza. Ikiwa kuna skuli za sekondari katika Jimbo lako zina upungufu wa vitabu vya kiada nakushauri uende ofisi ya elimu na mafunzo ya Amali Pemba ili upatiwe vitabu hivyo.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya Mhe. Ashura Sharif Ali mihutasari mipya ya elimu ya msingi imesambazwa katika skuli zote za Unguja na skuli za Pemba kwa idadi inayolingana na wingi wa elimu kwa skuli husika. Kwa skuli binafsi kila skuli imeomba na imepatiwa nakala mbili kwa kila somo.

Aidha ufuatiliaji uliofanywa na taasisi ya elimu Zanzibar kuhusu utekelezaji wa muhtasari wa darasa la kwanza ulibaini changamoto zifuatazo zinazokabili walimu; ni ukosefu wa vitabu vya masomo mengi, mihutasari mirefu na migumu kwa baadhi ya mada. Ili kukabiliana na changamoto hizi karibuni Wizara yangu inategemea kupokea vitabu vya kiada na miongozo ya walimu ya darasa la kwanza mpaka la nne. Vile vile tutafanya mapitio ya mihutasari ili kubaini upungufu uliopo na kufanyia marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar. Mhe. Mwanaidi, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Ashura walitaka kujua kuhusu ubovu wa Ofisi ya Mkaguzi Pemba, kutowepo kwa usafiri wa kuaminika katika Ofisi ya Mkaguzi Mkuu Pemba. Mheshimwa jibu ni kweli hali ya jengo hairidhishi, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu Pemba inafikiria hatua ya awali ya kutafuta ardhi na kuanza jengo lake. Pia tunatafuta njia mbadala ya kuomba jengo jengine la Ofisi ili liweze kutumika kabla ya kuanza hilo jengo ambalo tunakusudia kujenga.

Kutokuwa na usafiri Mheshimiwa hali halisi ni kama ifuatavyo; lipo basi moja la watu 16 ambalo lilinunuliwa jipya lakini huwa linapata matatizo hapa na pale mara nyingi na kwa sasa linafanya kazi, ipo Rover ya zamani ambayo nayo inahitaji matengenezo ya mara kwa mara lakini hivi sasa inafanya kazi. Zipo vespa tatu za wakaguzi ambazo zinatumika na vespa nane mpya zinatarajiwa kupelekwa Pemba kwa matumizi yanayotarajiwa.

Mhe. Panya Abdalla Ali na Mwanajuma Faki Mdachi, na Mhe. Mgeni,Mhe. Ashura, walishauri kuhusu kuwepo kwa ukaguzi wa Wilaya huko maskulini. Jambo hili Waheshimiwa tunalichukua na kulifanyia kazi katika kupitia mfumo wa ukaguzi Zanzibar unakusudiwa uwepo aina ya wakaguzi ambao badala ya kutoka mijini tu wawepo pia wakaguzi watakaoshughulikia masuala haya kiwilaya au kizoni, hatua hiyo inawezekana baada ya kutafakari kwa kina jinsi ya watakavyoweza kuendesha kazi wenyewe, matakwa ya kibajeti na kadhalika. Vile vile itahitajika kuwasilishwa mswada katika Baraza jinsi ya kubadilisha mfumo mzima wa ukaguzi wa maskuli Zanzibar na mambo yanayohusiana na haya. Hatua hiyo itachukuliwa muda utakapotekelezwa kwa vile ndio kwanza zipo hatua za awali.

Mhe. Naibu Spika, kuendesha vipindi vya *tucheze tujifunze* kwa njia ya radio maarufu kwa TUTU. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia suala hili ni Mhe. Viwe, Mhe. Rufai Said Rufai, na Mhe. Panya kwa jumla walitaka kujua ufafanuzi wa mambo mbalimbali ikiwemo muda wa kurusha vipindi, maslahi ya wasaidizi huchelewesha na uwezekano wa kuajiri.

Mhe. Naibu Spika, ufafanuzi wa hayo Wizara yangu imo katika utekelezaji wa sera ya elimu ya mwaka 2006 ambapo imeweka elimu ya maandalizi kuwa ni miongoni mwa elimu ya lazima. Hata hivyo baadhi ya maeneo hasa ya vijijini imekuwa vigumu kuanzisha madarasa haya kutokana na hali ya mazingira. Hivyo programu ya tucheze tujifunze TUTU imeanzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha watoto wa vijijini nao wanapata fursa hii, na ilianza rasmi mwaka 2007 kwa majaribio katika Wilaya ya Kaskazini A na sehemu ndogo ya Wilaya ya Magharibi kwa upande wa Unguja na Wilaya ya Micheweni kwa upande wa Pemba.

Pia programu hii inaendelezwa kwa darasa la kwanza na la pili katika Wilaya hizo. Hivyo kipindi cha redio kinarushwa kutoka Shirika la Utangazaji Zanzibar ambapo vipindi vya maandalizi hurushwa asubuhi kwa muda wa nusu saa mara tatu kwa wiki na vile vile darasa la kwanza na la pili hurushwa nyakati za asubuhi na hurushwa jioni pia mara tatu kwa wiki. Mbali ya vipindi hivyo Wizara imeandaa miongozo ya walimu na wanafunzi kurahisisha ufuatiliaji wa vipindi hivyo wakati vinaporushwa hewani. Kwa

mantiki hiyo hurushwa vipindi saa kumi na mbili kama alivyoomba Mhe. Mwakilishi itakuwa ni vigumu kwa wanafunzi kwani wanahitaji muongozo na maelekezo ya walimu wao.

Kuhusu maslahi ya wasaidizi Wizara itahakikisha inawalipa posho lao kwa wakati kama inavyotolewa mishahara na wala haijawahi hata mara moja kulimbikiza posho hilo kwa miezi 6 kama alivyodai Mheshimiwa Mjumbe. Mbali na hayo Wizara imeongeza posho la wasaidizi kutoka 20000 zilizokuwa zikilipwa wakati wa mradi huu ulipoanzishwa hadi hivi sasa 30000 wakati mradi huo umechukuliwa na Wizara.

Ombi la Mhe. Mjumbe kutaka Wizara iwaajiri imelipokea; hata hivyo inawashauri wajiendeleze kwanza kwani hawajafikia kiwango stahili cha taaluma yao ya kuajiriwa kama walimu. Vile vile hawajasomea ualimu isipokuwa Wizara imewapatia mafunzo mafupi ya kuweza kupunguza tatizo hili la elimu ya maandalizi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ashura, alitaka kujua kwa nini walimu wanahamishwa bila ya idhini yao. Mheshimiwa kuhusu kuhama kwa walimu ni jambo la kawaida na inatakiwa wakati wowote inategemea mahitaji ya skuli kulingana na idadi ya walimu waliopo.

Suala la Mhe. Salmin Awadh, kuhusu idadi ndogo ya walimu wa sayansi katika Skuli ya Nyerere. Mheshimiwa ni kweli tatizo la walimu wa sayansi kama alivyoeleza na tunavyozungumza siku zote ni kuwa skuli zote za Unguja na Pemba. Skuli zetu za Unguja zinahitaji walimu 381 kwa mwaka huu walimu wa sayansi waliojitokeza na kuajiriwa ni 57 tu, kwa upande wa skuli ya Nyerere wamepelekwa walimu 2 na wengine wamesambazwa katika skuli 40 za Unguja kwa mujibu wa ajira ya kiwilaya, mahitaji ya walimu hawa wa sayansi ni kama ifuatavyo:- Kusini ni 40, Kaskazini ‘A’ 71, Kaskazini ‘B’ 31, Kati 87, Mjini 53 na Magharibi ni 99.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ashura na Mhe. Nassor Salim Ali pia walizungumza kukosekana kwa Dakhalia katika Skuli zetu mpya na tumejipanga vipi kupeleka wanafunzi katika Skuli hizo.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa skuli hizo zote ziko chini ya mradi wa elimu ya lazima na zimeshaanza kusomesha. Wanafunzi waliopelekwa ni kutoka skuli za jirani ambapo ni kupunguza msongamano. Kutokana na uhaba wa fedha mradi huu haukuweka kipaumbele Dakhalia, na kwa wakati huu muhimu uliipa ujenzi wa Maktaba, Maabara na Vifaa pamoja na Vitabu.

Kuhusu ujenzi wa skuli za ghorofa Unguja. Mhe. Naibu Spika, sera ya elimu ni kujenga skuli za ghorofa kwa wilaya ili kupunguza tatizo la uhaba wa nafasi. Kwa Pemba tumejenga skuli tatu za ghorofa ikiwemo Chuo cha Ualimu cha William Benjamin Mkapa, Skuli ya Sekondari ya Mkanyageni na Skuli ya Madungu mpya.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rufai kuhusu Chwaka - Tumbe hadi lini itakuwa Skuli ya Wilaya. Skuli zote hizi ambazo tumezitaja ziko chini ya mradi wa elimu ya lazima hazitokuwa skuli za wilaya kwanza mpaka hapo zitapokuwa na Dakhalia.

Mhe. Naibu Spika, kama ninavyoeleza siku zote hapa kama nia ya skuli hizi ni kuwa skuli za wilaya, lakini kwa sababu ya bajeti yetu toka kutia saini mkataba na wakati wa ujenzi bajeti ilikuwa tayari imekuwa juu vifaa vimepanda, kwa hiyo ikabidi tuzitoe kwanza hizi Dakhalia na tujenge hizi skuli, lakini tuko katika matayarisho ya kuhakikisha kwamba na hizi Dakhalia zitajengwa na zitakapojengwa Mhe. Naibu Spika, ndio zitaweza kuzifanya skuli hizo kuwa ni skuli za wilaya.

Mhe. Naibu Spika, Skuli ya Chwaka-Tumbe inavuja, skuli zote ziko chini ya mradi wa elimu ya lazima ambazo zimekabidhiwa bado Mkandarasi yumo katika kipindi cha mpito kwa mwaka mmoja. Hivyo Mkandarasi wa skuli hiyo yuko Pemba na ameanza kufanya kazi skuli ya Utaani-Chasasa na baadae ataendelea kufanya matengenezo katika skuli hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, kuhusu walimu wa Nigeria alieleza kama wapo, aliuliza na wamepata faida gani. Walimu wa Nigeria wapo na wamepangiwa kufundisha katika skuli zetu mpya zilizo chini ya mradi wa elimu ya lazima kwa skuli zetu nyengine vijijini kwa Unguja na Pemba. Na kwa kweli walimu hawa wanaendelea vizuri na utendaji wao wa kazi, na kwa kweli Wizara ya Elimu inaturidhisha.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abdalla Juma, kuhusu kuzigawa skuli kuwa za wanawake na wanaume. Mhe. Naibu Spika, shauri hilo si baya kwani hata Wizara yetu imeanza kufanya majaribio kwa skuli moja ya Benbella Unguja na skuli ya Utaani kwa Pemba ambapo wanasoma wanafunzi wanawake pekee.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hija, alizungumza kuhusu vumbi la skuli ya Madungu Mpya Sekondari. Mhe. Naibu Spika, tayari imeshaelezwa wakandarasi na tayari kazi ya marekebisho imeshaanza hii ni kutokana na kuwepo kipindi cha mwaka mmoja cha mkandarasi kufanya matengenezo ya mapungufu yoyote ambayo yanajitokeza.

Mhe Naibu Spika, ahadi ya kuwapatia mkopo vijana waliomaliza mafunzo yao, hili alilizungumza Mhe. Ashura na alilizungumza Mhe. Panya Ali.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri suala hili nililijibu juzi katika suali langu la nyongeza ambalo aliniuliza Mhe. Panya na nikamjibu lakini kwa maslahi ya waliomleta hapa basi si vibaya tena kulijibu tena suali hili. Mhe. Naibu Spika, nilisema fedha za mkopo kwa ajili ya kuwapatia vijana wanaohitimu mafunzo yao katika vyuo vyetu vya amali zipo na wanatakiwa watimize masharti ya mkopo ikiwa ni pamoja na kujikusanya katika vikundi vya ushirika; hatua ambayo tayari imekamilika na sasa wamo katika hatua ya kupata usajili wa vikundi vyao na wakimaliza watapata mikopo hiyo.

Nachukua fursa hii kuwaomba wanaoshughulika na utoaji wa leseni ya vikundi vya ushirika wawasaidie vijana wetu kupata kwa haraka na sisi tuwapatie fedha ili waingie katika soko la ajira na kuweza kujisaidia wao wenyewe pamoja na familia zao.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha Mamlaka ya mafunzo ya amali imetenga fedha maalumu kwa ajili ya kuwapatia mafunzo maalumu ya wahitimu wa mwaka huu kuwafunza zaidi namna ya kutimiza elimu na mafunzo waliyoyapata kuwawezesha kujiajiri. Kazi gani ya kuzifanya wataweza kupata faida kubwa namna ya kutafuta washiriki katika vikundi matumizi mazuri ya mikopo, uanzishaji wa biashara na namna gani wataweza kupata faida kubwa kwa mufa mfupi kwa kupitia vikundi vya ushirika.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa taarifa rasmi kuwa vyeti vya wahitimu wa vituo vya amali viko tayari na wakamilishe taratibu za kumaliza mafunzo wachukue vyeti vyao.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Maktaba, hoja ilikuwa ni upungufu wa vitabu vya sayansi katika Maktaba Kuu, kuchelewa kuanzishwa kwa ujenzi wa Maktaba Pemba, kuanzishwa kwa Maktaba ya Wilaya, Skuli hazina Maktaba. Wanaotoa hoja na masuala haya ni Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Suleiman Hemed, Mhe. Ibrahim Makungu, Mhe. Asha Abdu Haji, Mhe. Salma Mohammed Ali na Mhe. Ashura Sharifu Ali.

Mhe. Naibu Spika, shirika linapata vitabu kupitia njia mbali mbali; kuna vitabu ambavyo shirika linanunua kwa fedha za SMZ na nyengine zinapatikana kwa njia ya misaada kutoka shirika la maendeleo la watu binafsi ndani na nje ya nchi. Miongoni mwa vitabu vilivyonunuliwa ni pamoja na vitabu vya sayansi ukilinganisha na mahitaji ya wanachama na vile vile idadi ya wanachama wanahitaji Maktaba imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, shirika litaendelea na utaratibu wake wa kununua vitabu kila hali itaporuhusu. Katika mwaka wa fedha 2012/13 shirika limenunua vitabu tofauti vikiwemo vya sayansi vyenye thamani ya 8,000,000/= na kwa mwaka huu shirika limejipangia kununua vitabu vyenye thamani ya 20,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa vitabu hivyo.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa Maktaba Pemba ni kweli umechelewa kuanza, sababu hasa iliyopelekea uchelewaji huo ni upatikanaji mdogo wa fedha za maendeleo, lakini hata hivyo hatua kubwa imechukuliwa mkandarasi ameshapatikana na *inshallah* kazi inategemea kuanza tarehe 7/8/2013.

Suala la kuanzishwa Maktaba ya Wilaya ni muhimu sana na ndio hasa lengo la Wizara kuwa na Maktaba katika kila wilaya ili huduma za maktaba ziwafikie walio wengi. Kwa sasa shirika linachukua jitihada ya kushajihisha jamii kuwa na muamko wa kuanzisha Maktaba katika jamii zao ili iweze kusaidia.

Shirika linatoa mafunzo juu ya kuendeleza Maktaba hizo na pia kugawa vitabu mbali mbali. Hadi hivi sasa Maktaba 4 za jamii chini ya MJUKIZA, Maktaba hiyo iko Chukwani, Welezo, Kiembesamaki na Mpapa, Uzini na Fumba, Bweleo na Tumbatu. Shirika linatoa wito kwa jamii kujiunga na jamii hiyo MJUKIZA ili Maktaba hizo zienee maeneo mengi na kuweza kutoa huduma kwa jamii kwa karibu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa Skuli hizi hazina Maktaba, jitihada mbali mbali zimekuwa zikichukuliwa ili kupunguza tatizo hilo. Wizara imeshaanza kulifanyia kazi katika skuli mpya ambazo wamejenga, suala la maktaba linapewa umuhimu mkubwa. Pia shirika la huduma za Makataba limeanza na programu ya Maktaba ya sanduku kwa kulenga kuwa na Maktaba kamili. Skuli 35 za msingi zimefaidika na mradi huu na pamoja na za kati, skuli ya Mkokotoni imeshajikomboa kwa kuwa na Maktaba kamili. Mashirikiano ni muhimu sana katika suala hili ili lengo la kuwa na Maktaba kila skuli liweze kufikiwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba hizi hoja ambazo amezileta Mhe. Ismail Jussa, ni nyingi ni karibu ya hotuba yetu yote ya bajeti atakuja kuziwasilisha Mhe. Waziri hapa kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku, kuhusu darasa wanalotumia wanafunzi wenye ulemavu wa akili Michakaeni. Baada ya kuona hali ya mvua inazidi kuathiri na huenda Kamati yako imechelewa sana Wizara imeshaezeka, hata hivyo msaada wako tunauhitaji sana kwa mambo mengine kama kupiga rangi katika skuli hiyo.

Kuhusu suala la maji Bopwe, skuli ilipata ufadhili wa kuchimba kisima na hivi sasa kimo katika hatua za majaribio, zile pesa 2,000,000/= ambazo tuliahidiwa kuzipata bado hazijapatikana lakini Wizara imefanya jitihada nyengine na tumepata mfadhili na ndio hatua za mwanzo ndio tumezianza, kwa hivyo nakuomba Mheshimiwa huna haja ya kupiga buti bajeti yangu naomba uunge mkono mia kwa mia kwa sababu hoja zako zote tayari tumezifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu hati miliki za skuli. Suala la uvamizi wa maeneo ya skuli limechangiwa na Wajumbe wengi Mhe. Mwanaidi Kassim, Mhe. Saleh Nassor, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Ali Salum, Mhe. Jaku Hashim, Mhe. Subeit Khamis. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Waheshimiwa wote waliochangia kwamba ni muhimu skuli zetu kupatiwa hati miliki ili kudhibiti uvamivi ulioshamiri. Kamati za skuli pamoja na Wizara zimekuwa zikijitahidi kuomba kwa Idara husika lakini kikwazo kimoja kinachochangia kutopatikana kwa hati miliki ni malipo ya gharama za upimaji. Wizara imetenga fedha katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi kifungu namba 220110 kwa ajili ya kusaidia gharama ya upatikanaji wa hati miliki kushirikiana na Idara husika katika kulipatia ufumbuzi tatizo hili kubwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Subeit Khamis Faki, alitaka kujua namna ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanavyotafautiana na wenzao katika ufanyaji wa mitihani.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri, naomba kidogo unistahamilie tuna wageni tuwatambulishe maana wana haraka halafu tutaendelea.

Waheshimiwa Wajumbe naomba kuwatambulisha kwamba tumepata wageni hii leo, wageni wenyewe wanatoka *CommonWealth Parliamentarian Women CWP* ambayo ni Mhe. Beatrice Shelukindo; Mbunge wa Jimbo la Kilindi Tanga kwa Chama cha Mapinduzi na Kamishna wa Tume ya Kudumu ya Bunge na Mwenyekiti wa *CWP*. Na wa pili Mhe. Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum Kaskazini Pemba kwa Chama cha *CUF*, na ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili, na wa mwisho ni Bi. Justina Shauri; Mkurugenzi Msaidizi na *Desk Officer CommonWealth Parliamentarian Women East Africa Region*, lakini pia wameongozana na wenyeji wao wa kwanza ni Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Waziri wa Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais na Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwenyekiti wa Baraza. Kwa hiyo karibuni sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naendelea. Mhe. Subeit Khamis Faki, alitaka kujua namna ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanavyotafautiana na wenzao katika

ufanyaji wa mitihani. Mhe. Naibu Spika, mitihani ya wanafunzi hawa hurekebishwa kulingana na mahitaji yao, pia hupewa vipaumbele maalumu kwa kuongezea muda wanapofanya mitihani yao, vile vile kwa wale wasioona hutayarishiwa maandishi maalumu, hata hivyo usahihishaji wao huwa tafauti vile vile na wanafunzi wengine.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salum Abdalla Hamad, alitaka kujua kuhusu posho la usahihishaji mitihani. Mhe. Naibu Spika, wasahihishaji wote wamelipwa posho zao kabla hata ya kuondoka katika kambi ya usahihishaji. Kwa hivi sasa nafurahi kusema kuwa hatuna deni linalodaiwa kwa Wizara kuhusiana na walimu ambao wanasahihisha mitihani hiyo. Mhe. Salim Hamad vile vile na Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Suleiman Hemed, walitaka kujua Wizara ina mpango gani katika kuboresha matokeo ya kidato cha nne, kidato cha pili na darasa la saba.

Mhe. Naibu Spika, Wizara kwa mwaka huu wa fedha 2013/14, Wizara imeanzisha tena mitihani ya pamoja na majaribio ya ngazi ya Mikoa ambayo itasimamiwa na Baraza la Mitihani ya Zanzibar. Mitihani hiyo itakuwa na kiwango sawa sawa na ile ya taifa, kwa hivyo wanafunzi wetu watapata uhalisia wa mitihani itakavyokuja. Vile vile ni agizo la Serikali lililotolewa na Baraza la Mapinduzi. Kwa upande wa alama za maendeleo ya wanafunzi kuna muongozo unaotumika ambapo kila mwalimu wa somo ni lazima afuate kabla ya alama hizo kupelekwa Baraza la Mitihani la Taifa kwa matumizi yao.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Haji, alieleza kuwa kuna walimu waliosomea tokea mwaka 1978 ili kuziba mapengo ya walimu anataka kujua idadi yao na kuomba wasaidiwe mishahara yao ili itononoke kabla ya kustaafu.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Wizara iliajiri vijana wengi na baadae ndio wakaanzisha mafunzo ya elimu masafa ili kuwakomboa walimu hao, walimu wengi wamefanikiwa kupata cheti ya *grade* ya tatu na waliobaki ni kidogo, walimu waliobaki wa vituo vya ualimu ni kama ifuatavyo: - Miti Ulaya 25, Wingwi 30, Mizingani 76, Michakaeni 40 kwa Pemba. Bububu 77, Mkwajuni 42, Dunga-Kitogani 300 na Kiembesamaki ni 63 kwa Unguja. Ili kuwamaliza walimu hao mafunzo ya elimu masafa awamu ya nne yataendelea kwa mwaka huu.

Mhe. Suleiman Hemed, alieleze hofu ya kukosekana ufundishaji wa walimu. Wanaopenda kujifunza kwa njia ya elimu masafa, kwa mujibu wa utaratibu uliopangwa na Wizara hatutegemei kukosekana kwa ufundishaji; kwanza mafunzo ya ualimu hutolewa siku mbili nazo ni Alkhamis na Jumamosi na

siku za kazi ni Alkhamis tu. Pia Walimu Wakuu wamepewa agizo la kuwapunguzia idadi ya vipindi walivyopangiwa pindi siku ya Alkhamis wakiwepo kwenye mafunzo yao. Kwa hiyo Mheshimiwa hatutarajii kuwa walimu hao wakosekane katika maskuli yetu kwa sababu siku ambayo tumewapangia kwenda kuchukua mafunzo ya kazi ni siku moja tu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Subeit Khamis, alitaka kujua kwa nini hakujapelekwa *Matron* katika Chuo cha Kiislamu Pemba. Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu wetu mtu anayetakiwa kuwa *Matron* awe na taaluma ya ualimu au *nurse*, hivyo Wizara imefanya utaratibu wa kuwahamasisha walimu kuomba nafasi hiyo, tulipata walimu wachache wa Chuo cha Kiislamu lakini kutokana na uhaba mkubwa wa walimu Wilaya ya Micheweni tulishindwa kuwapangia. Hata hivyo mara tu baada ya ajira za walimu wa cheti ikipatikana tunakuhakikishia Mhe. Subeit kuwa suala hili litamalizika.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kujengewa Msikiti. Wizara haijengi Msikiti ila hutafuta wafadhili wa kujenga Misikiti hiyo na naomba kumuhakikishia Mhe. Subeit kuwa Msikiti huo utajengwa Chuo cha Kiislamu kwa ufadhili wa Serikali ya Saudia na tayari tumeshapata Mfadhili huyu, na Mheshimiwa hiyo isiwe hoja ya kukataa bajeti yetu, wewe ni mwenzetu na najua ni mdau wa elimu kwa hiyo naomba uiunge mkono bajeti hii mia kwa mia ujue kama msikiti wako uko katika hatua ya karibuni ya kujengwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Ashura Sharif na Mhe. Salum, walitaka kujua kwa nini Wizara haijaanzisha mafunzo ya cheti kwa elimu maandalizi. Mpango wa kuanzisha mafunzo ya Stashahada ya elimu ya maandalizi umeanza, Idara ya Mafunzo ya Ualimu imeanza kuorodhesha walimu waliosomea elimu ya maandalizi kwa ngazi ya shahada na stashahada ili waweze kuwa wakufunzi katika Vyuo vya Ualimu. Wakati huo huo Chuo Kikuu cha Aga khan cha Dar es Salaam kwa kusaidiana na Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi imeanzisha mafunzo kazini kwa walimu watakaosomesha skuli za maandalizi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Mohammed Suleiman Hemed na Mhe. Mgeni Hassan, walionesha utashi wao kuwa walimu wa sasa hawapatiwi elimu ya msingi ya ualimu kiasi ambacho ufundishaji wao sio mzuri.

Mhe. Naibu Spika, Vyuo vya Ualimu vinaendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya ualimu kama ilivyokuwa ikitolewa zamani, mafunzo yote yanamjenga mwalimu anayefundisha aweze kusomesha wanafunzi wake kama inavyotakiwa na elimu ya mitaala wanayofundishwa.Halikadhalika wanafunzi hufundishwa uandishi na herufi mbali mbali na upatikanaji wa vifaa vya

kufundishia. Wakati huo huo wanafunzi hufundishwa maadili ya ualimu ili kufanikisha hayo, kila Chuo huanzisha kamati ya dawa, kamati ya mazingira. Aidha wakufunzi wa Vyuo wamepatiwa mafunzo na mbinu za kufundishia kwa kuzingatia jinsia, yanayotolewa ili nao wafundishe wanafunzi wao.

Mhe. Naibu Spika, ili kuendelea na taaluma zaidi ya mafunzo yanayofundishwa madarasani, Wizara kupitia mradi wa elimu ya lazima inaendesha mafunzo mbali mbali kama ilivyotajwa katika vitabu vya bajeti ukurasa wa 18. Aidha kwa mwaka huu wa fedha tunatarajia kuendesha mafunzo ambayo hutolewa kwa walimu wenye vyeti lakini husomeshwa sayansi, hisabati katika madarasa ya sekondari.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya hati miliki kwa skuli ya Ndagoni. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Saleh Nassor wa Jimbo la Wawi na Mhe. Salum Abdalla wa Jimbo la Mtambwe. Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe taarifa ya kuwa, skuli hii haikuvamiwa na inayo hati miliki na hati miliki nitaikabidhi kwako Mhe. Naibu Spika, hata hivyo Wizara yangu itakaa na wahusika kama ushauri ambavyo umetolewa na Wawakilishi, tunaukubali ili kujenga mustakabali mzuri kwa manufaa ya jamii na watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya ajira ya cheti. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Hassan Hamad wa Kojani. Mheshimiwa alisema kwamba kuna kijana mmoja wa Chokocho Wilaya ya Mkoani ameajiriwa katika Wilaya ya Wete, Jimbo la Mtambwe. Mhe. Naibu Spika, yeye anaona kuwa si vyema kijana huyo kuajiriwa na kupelekwa skuli ya Mzambarau Takao na kuwa anatoka Wilaya ya Mkoani. Wizara haina taarifa na kijana huyo ambaye amejiriwa, tunaomba Mheshimiwa atupatie jina la kijana huyo aliyeajiriwa ili tuweze kulifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hija Hassan Hija, aliuliza sababu zilizofanya wahisani waingize fedha kidogo katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na muhisani katika mradi huo wa BADEA, mchango wa wahisani umekuwa mdogo ukilinganisha na makadirio kwa sababu nne kubwa.

Sababu ya kwanza ni kuchelewa kwa baadhi ya wasambazaji wa vifaa kukamilisha uletaji wa vifaa hivyo, usambazaji wa vifaa vya maabara vya baiolojia kuwasilishwa vifaa hivyo vilivyo chini ya kiwango na hivyo kukataliwa, vifaa vilivyoletwa kuahirishwa vihamishwe vifaa vyake na kutofanyiwa malipo, mkandarasi wa ujenzi kutokamilisha baadhi ya kazi na kusababisha malipo yake kuchelewa. Baadhi ya maombi ya malipo yalipelekwa BADEA, Sudan kuchukua muda mrefu karibu miezi mitatu kabla ya kufanyiwa malipo. Hata hivyo, mradi huo unatarajiwa kukamilika katika

mwaka huu wa fedha. Mkandarasi wa ujenzi hivi sasa anaendelea kufanya kazi zake zilizobakia na usambazaji wa vifaa vya maabara, vya fizikia, yuko katika hatua ya kusambaza vifaa vilivyobaki vya maabara.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Subeit Khamis Faki alichangia suala la ajira katika Jimbo lake la Micheweni. Mheshimiwa alisema kama kulikuwa na vijana watano ambao walijitolea katika skuli ya Maziwa Ng'ombe lakini walioajiriwa ni wawili. Naomba nimueleze kwamba, kuwa hapo kulikuwa na vijana watano kweli, vijana wanne wameajiriwa na kupatiwa kazi katika skuli ya Maziwa Ng'ombe na kijana mmoja hakuweza kuajiriwa kwa sababu hakuwa na cheti. Kwa hivyo, sifa ya kuajiriwa ilikosekana.

Pia Mhe. Subeit aliuliza tatizo la usafiri wanachuo wa Chuo Cha Kiislam Kiuyu. Taarifa tuliyonayo hivi sasa ni kuwa gari aina ya SUZUKI iliyopo chuoni imeharibika na iko katika matengenezo *garage* ya Gombani na uongozi wa chuo wanayo taarifa hiyo. Gari iliyobakia ni aina ya TATA na inafanyiwa matengenezo katika mwaka wa fedha baada ya kuingiziwa fedha.

Kuhusu hoja ya masomo ya sayansi katika skuli ya sekondari ya Vikunguni nayo Mhe. Salma Mohamed Ali aliizungumza. Taarifa tulizonazo ni kuwa skuli ina walimu wawili wa masomo ya sayansi; mmoja ni wa kidato cha sita na wa pili ni mwalimu wa muda kutoka skuli ya sekondari *Fidel Castro.* Hawa wote wanafundisha masomo ya sayansi isipokuwa somo la *chemistry*. Wizara yangu itakaa na ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba ili kuangalia uwezekano wa walimu wa sayansi katika skuli hii. Kwa somo la *physics* nalo lifundishwe katika kidato cha nne. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Salma aunge mkono hoja yetu wakati suala lake tukilifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Wizara imeripoti kuwa utafiti uliofanywa katika skuli 334 inaonesha kuwa wanafunzi 73 wenye mahitaji maalum katika skuli hizo idadi hii ni kubwa sana. Je, kuna walimu wangapi wenye uwezo wa kufundisha? Hoja hiyo pia aliichangia Mhe. Jaku Hashim Ayoub, napenda kujibu kuwa walimu walipata mafunzo ya Nukta Nundu kupitia warsha za muda mfupi wiki nne mpaka sita ambao wana uwezo wa kufundisha walimu wasioona ni 218, wanaume ni 77 na wanawake ni 141.

Mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi wenye ulemavu wa uoni, walimu waliopata mafunzo ya Nukta Nundu ya muda mrefu kupitia Chuo cha Kiislamu Mazizini ngazi ya cheti ni 189, wanaume 39 na wanawake 150. Walimu waliopata masomo ya muda mrefu ngazi ya cheti na hawa walipata Chuo cha *Patandi* Arusha ni sita, wanaume watatu na wanawake watatu. Walimu waliopata mafunzo ya muda mrefu ngazi ya *diploma* katika Vyuo vya

Patandi Arusha na Chuo Kikuu cha Kyambogo Uganda ni 5, wanaume 4 na mwanamke 1. Walimu walioko masomo ya ngazi ya shahada ni 4 wote wanaume walimu wote ni kwa fani ya wasioona tu.

Mafunzo ya muda mfupi kwa wanafunzi viziwi, wenye uzito wa kusikia. Walimu waliopata mafunzo ya lugha ya alama kwa kupitia warsha ya wiki nne hadi sita wanafundisha wanafunzi hao ni 325; walimu 142 ni wanaume na 183 ni wanawake. Katika kozi ya Chuo Cha Kiislam walimu hao hao wamepatiwa mafunzo ya Nukta Nundu, Lugha ya Alama na mafunzo mengine katika kipindi cha mwaka mmoja. Mafunzo ya muda mrefu kwa walimu hao walipata mafunzo ya lugha ya alama kwa muda mrefu katika Chuo cha Kiislamu ngazi ya cheti ni 189, walimu 39 wanaume na 150 wanawake. Walimu waliopata mafunzo ya muda mrefu ngazi ya cheti katika Chuo cha Patandi Arusha ni 3 wanaume 2 na mwanamke 1. Walimu waliopata mafunzo ya muda mrefu ngazi ya diploma Chuo Kikuu cha Kyambogo Uganda ni mmoja na ni mwanamme. Walimu walioko masomoni ngazi ya stashahada ya kwanza ni mwanamme mmoja.

Hoja nambari mbili walimu waliofundisha katika madarasa ya Elimu Mjumuisho kupatiwa vifaa hili alilizungumza Mhe. Asha Abdu Haji. Kwa mwaka 2012 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilinunua vifaa mbali mbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalum vya shilingi 600 milioni, miongoni mwa vifaa hivyo ni mashine ya Nukta Nundu**,** Shime Sikio, mashine mbili za kutolea *photocopy* kwa maandishi ya nukta nundu, fimbo nyeupe, radio kaseti na vifaa vya kunasia sauti na karatasi za nukta nundu kwa wanafunzi wasioona.

Vifaa kama hivyo vya shilingi 88 milioni pia vitanunuliwa kupitia mradi wa Elimu Mjumuisho na maendeleo ya vijana unaotekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wa Akili. Aidha, walimu 146, 50 wanaume, 96 wanawake wamepewa mafunzo ya kutengeneza vifaa vya kufundishia na kujifunza kwa kutumia mali ghafi zinazopatikana katika maeneo wanayoishi.

Mhe Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja ya wanafunzi wasioona na msaada wanaopatiwa kupitia Chuo Kikuu cha Tunguu. Kuna mwanafunzi ambaye alimzungumza Mhe. Jaku Hashim, Wizara ya Elimu kitengo chake cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kinafanya kazi ya uhamasishaji ya kutoa taaluma juu ya wanafunzi wenye mahitaji maalum na jinsi ya kuwapa msaada unaohitajika katika kujifunza kwa walimu. Wanafunzi wenzao na wazazi akiwemo mwanafunzi huyu asiyeona anayesoma *Zanzibar University*. Wizara inatoa mafunzo ya Nukta Nundu kwa walimu wote waliokuwa wakisomesha

tokea darasa la kwanza hadi la saba, na kwa walimu wa Haile-selassie kwa masomo yake ya sekondari.

Pia iliwahamasisha wanafunzi wenzake kumpatia msaada unaohitajika katika masomo yake akiwa katika skuli na nje ya skuli. Kuwahamasisha wazazi wake ambao walielewa umuhimu wa elimu kwa mtoto wao na kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa walimu wake. Kumpatia mwanafunzi huyo vifaa kadhaa vinavyomsaidia katika kujifunza ikiwa ni pamoja na mashine ya nukta nundu, karatasi za kuandikia, fimbo nyeupe, pamoja na kuchapishiwa mitihani yake akiwa katika ngazi ya msingi, alipatiwa vifaa vya ziada alipokuwa sekondari; vifaa hivyo ni pamoja na redio, vinasa sauti, *laptop*, kompyuta na hata kuchapishiwa baadhi ya *notes* zake pale ilipohitajika pamoja na walimu waliokuwa wakimfundisha sekondari kupatiwa mafunzo mbalimbali ya kuwawezesha kumsomesha.

Mhe. Naibu Spika, mbali ya hayo pia alipatiwa mwalimu mtaalamu aliyekuwa na *diploma* ya wasioona ambaye alipangiwa Skuli ya Haile Selassie kwa siku tatu kati ya siku tano ili aweze kumsaidia kwa karibu zaidi. Vile vile aliingiziwa *program* inayozungumza katika kompyuta yake inayomuwezesha kusoma na kuandika maandishi ya kawaida ambayo anaweza kusoma mtu yeyote.

Mhe. Naibu Spika, Wanafunzi Wenye Ulemavu kutengwa kwa kusomeshwa katika madarasa yao peke yao na kufanyiwa mitihani yao tofauti, hoja hii ilichangiwa na Mhe. Subeit Khamis. Kutokana na mikataba mbali mbali ya kitaifa ikiwemo mkataba wa haki za binadamu wa mwaka 1948, mkataba wa haki za mtoto wa mwaka 1089 anayetakiwa kila mtoto asome, mtoto ana haki yake ya kupata elimu; lakini tamko la elimu kwa wote la mwaka 1990, tamko la Salamanca la mwaka 1994, mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu wa mwaka 2006 na mengineyo imesisitiza kwamba mtoto mwenye ulemavu asitengwe katika madarasa yao pekee katika kuwapatia elimu, bali wasome na wanafunzi wenzao katika madarasa ya kawaida. Hivyo, kuwatenga ni kuwanyima haki zao za msingi, Sera yetu ya Elimu ya Taifa ya Zanzibar ya mwaka 2006 na Rasimu ya Sera ya Elimu ya Mjumuisho ya mwaka 2009 imesema aidha kwamba wanafunzi wenye ulemavu wasitengwe kwa ulemavu wao katika kuwapatia elimu lakini wasome na wenzao katika madarasa ya kawaida.

Rasimu ya Sera ya Elimu Mjumuisho inasema kwamba wanafunzi viziwi, wasioona na wenye ulemavu wa akili watatengewa muda wa kujifunza lugha ya alama, maandishi ya nukta nundu na kurekebisha tabia zao. Kwa kipindi fulani ndani ya siku, muda uliobaki wa kusoma husoma na wanafunzi wenzao

katika madarasa yao. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, utaona umuhimu wa wanafunzi hawa kukaa pamoja na kusoma na wanafunzi wenzao.

Resource room; ni darasa ambalo lina nyenzo zitakazomuwezesha mwanafunzi kujifunza maarifa yanayohitajiwa katika kupata kama lugha ya alama na nukta nundu na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, suala la wanafunzi hawa kufanyiwa mitihani yao nilikwishalijibu katika kipindi cha maswali na majibu ambapo lilikuwa swali Nam. 62. Lakini kama haikutosha kwa maslahi ya Baraza lako hili tukufu na maslahi ya wananchi ambao wamemleta Mheshimiwa.

Wanafunzi wenye mahitaji maalum wako katika makundi mbali mbali, miongoni mwao wenye ulemavu wa wasioona, usikivu viungo, akili na walemavu wengineo. Wanafunzi wenye magonjwa sugu, wanafunzi waliyoathirika au wanafunzi wenye virusi vya UKIMWI, wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu na wengineo. WEMA imeandaa sera mjumuisho ambapo imezingatia mahitaji ya wanafunzi mbali mbali katika uandaaji, usimamiaji, usahihishaji mitihani. Baraza la Mitihani Zanzibar linazingatia Sera ya Elimu Mjumuisho, miongozo ya sera hiyo imeandaliwa baada ya kupitishwa sera hiyo.

Kwa mfano, katika ukurasa wa 45 kipengele 5.5 kinasema kwamba, "Iwapo kutakuwa na mwanafunzi mwenye mahitaji maalum tofauti watakuwa wanafundishwa katika kiwango tofauti kwa kutumia njia tofauti ili kukidhi mahitaji yao. Pia kuwe na utungaji wa mitihani wenye utafauti kulingana na mahitaji yao". Masuala haya pia yanaweza kuwa katika hali tafauti kama hivi. Mwanafunzi mwenye kukosa umakini kutokana na sababu za kimasomo na kijamii, ulemavu wa viungo na uoni, wanafunzi wanaojibu kwa kutumia maandishi ya nukta nundu au mwanafunzi anayetumia dawa zinazowafanya wasiweze kujibu mitihani yao katika hali ya kawaida.

Masuali huchapwa katika maandishi makubwa kwa wanafunzi wenye uoni hafifu, masuali huchapwa katika nukta nundu kwa wanafunzi wasioona, masuala hutayarishwa kwenye CD au Video katika lugha ya alama na wanafunzi viziwi hujibu kwa kutumia lugha ya alama mbele ya *camera*, na kwa wale watakaoshindwa kuandika. Masuala watakayosoma wanafunzi wakajibiwa kwa mdomo njia hii inatokana na wanafunzi wenye matatizo mahsusi katika kuandika na kusoma. Kusoma kwa kubadilisha herufi maneno kama *box* yeye huandika *boss.*

Mhe. Naibu Spika, pia kulikuwa na masuala yatakayorekebishwa katika kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye matatizo ya kijamii ya kimaono,

kiutamaduni au kiakili ambayo hayawezi kwenda sambamba na wenzao darasani. Masuala yatakayowataka wanafunzi kufanya kazi kwa vitendo vile vile wataweza kujibu masuala yatakayokuwa katika mazingira nambari moja na wala sio mbili. Hata hivyo, kuna hatua ambazo tayari zimeanza kufanyiwa kazi Baraza la Mitihani Zanzibar ikiwemo kuongezeka kwa muda wa dakika 15 kwa kila saa moja kujibia mitihani kwa wanafunzi wasioona. Kushirikishwa kwa walimu wataalamu wa fani za uziwi na uoni katika utungaji wa mitihani ya wanafunzi hao na usimamiaji na usahihishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum watakapoweza kufanya mitihani katika mazingira yaliyoelezwa na hapo juu kutakuwa na haja ya kutoa kipaumbele maalum cha kuwarekebishia kiwango cha ufaulu masuala yatakayokuwa katika hali mbali mbali kutokana na mahitaji yao.

Juhudi zote hizi zinachukuliwa na zitachukuliwa ili kila mwanafunzi aweze kusoma na kufanya mtihani wake kwa hali yake bila ya kupoteza nguvu au kuburuzwa katika darasa la kawaida.

Mhe Naibu Spika, naomba nimalizie jambo kuwa tuna hoja nyingi sana na kuna hoja ambazo nilitaka kumsaidia Mhe. Waziri wangu za wale watu 12 ambao walichangia kwa maandishi naomba muongozo wako tufanye nini.

Mhe. Naibu Spika: Pitia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Naheshimu maamuzi yako Mheshimiwa naomba basi nimalizie kwa suala moja hili ambalo alilizungumza Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Ismail Jussa kuhusu Skuli ya Kengeja.

Mhe. Naibu Spika, na Baraza lako tukufu litakuwa ni shahidi suali hili niliwahi kulijibu kwa Mhe. Mohamed Haji Khalid. Mimi nilimueleza kwamba nakubaliana naye kuwa kuna madarasa pale ambayo ni mabovu, lakini kuna madarasa ambayo tumeyafanyia kazi na kuyajenga na Mhe. Ismail Jussa alisema kuwa kachukua picha pale, na mimi kwa bahati nzuri kwenye tarehe 8 nilikuweko katika ziara Pemba na katika skuli ambazo nilichukua picha ili kwa kuja kuzifanyia kazi katika wizara yangu moja wapo ilikuwa ni skuli ile. Kwa hivyo, pia nitampatia Mhe. Ismail na Mhe. Hussein Ibrahim ili twende sambamba wajiridhishe na haya ambayo nitayaeleza.

Mwaka 2010 pale tulifungua darasa jengo ambalo lina madarasa 4 na Dr. Amani Karume ndiye ambaye alifungua madarasa yale. Bahati nzuri siku hiyo hiyo akatuwekea tena jiwe la msingi la banda ambalo lilikuwa na madarasa 3, kwa bahati nzuri tumelifungua kwenye mwaka 2012 zinafanya kazi. Kuna banda pale la mabati ambalo ni la toka mwaka 1910. Mheshimiwa banda lile

lipo na tumelifanyia marekebisho, kwa sababu lilikuwa likivuja nikaenda nikaliona kwa mara ya kwanza nikataka bati ambazo zimeezuliwa skuli ya Castro zipelekwe pale ziende zikaezekewe lakini bado lina matatizo banda lile kwa upande wa nyuma ambapo Kamati ya Ustawi wa Jamii ilipopita ilitutaka wizara banda lile tulijenge kwa matofali kwa huu upande wa nyuma.

Sasa hapa Mhe. Naibu Spika, nitataka ridhaa ya Baraza lako tukufu kwa sababu wenyewe banda lile wameliweka kama ni historia ya skuli yao. Kama nilivyosema limejengwa mwaka 1910, kwa hivyo hawataki banda lile liondolewe wanataka libakie vile vile isipokuwa lifanyiwe ukarabati kwa mujibu wa vile lilivyo kwa *material* yale ambayo yalijengewa.

Lakini vile vile kuna banda moja ambalo mimi niliagiza nilipokwenda lilikuwa katika hali ngumu, nikamuagiza Afisa Mdhamini banda lile alivunje. Bahati nzuri nimekwenda juzi nikaona kama banda lile tayari liko chini limevunjwa na wenyewe wamekusudia kujenga skuli ya ghorofa pale.

Kwa hivyo, nachukua fursa hii pia kuomba Kamati ya Skuli pale na walimu, walimu wakuu waanze ujenzi wao ule na tayari kuna matofali ambayo nimeyakuta pale karibu matofali 800 na mchanga umewekwa kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa skuli hiyo ili wao waanze na sisi kama inavyoeleza sera yetu ya mwaka 2006 kwamba kuwashajihisha wananchi wajenge na sisi tutamaliza.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunistahamilia kwa muda mrefu ambao nimechukua, lakini kama ambavyo nilizungumza kwanza ni kutokana na hoja hizi kuwa nyingi, nzito, zinazohitaji upeo na maarifa makubwa kuweza kuyajibu.

Kwa hivyo, nimalizie kuwashukuru na kuwaomba Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu watuunge mkono hoja yetu hii mimi na Waziri wangu na watendaji wetu tuwasikivu, tunasikiliza hoja zao na tutazifanyia kazi kwa hali ambayo Mwenyezi Mungu atatujaalia na bajeti tutayotiliwa na serikali. Naamini serikali inajua umuhimu wa elimu. Kwa hivyo hawatasita kututilia pesa kwa kile ambacho tunakiomba.

Mhe. Naibu Spika, nimalize kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nawashukuru sana Wajumbe wako, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kufanya majumuisho hii leo ya hoja za Waheshimiwa Wawakilishi na michango ya Mawaziri wawili na Naibu Waziri mmoja waliyoitoa baina ya jana na leo. Pia namshukuru sana

Naibu Waziri wangu, kwa ufafanuzi mkubwa sana wa kuridhisha aliyoutoa kwa hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, hoja zilizotolewa ni nyingi mno, wachangiaji kama alivyosema Naibu Waziri ni 42 haijapata kutokea, wala siwalaumu na wala sitaki niseme hivyo kwamba ninawalaumu, lakini nawapongeza sana kwa kutambua umuhimu wa elimu maana wasingetambua umuhimu wa elimu wasingechangia kiasi hicho.

Sasa kwa kuwa wachangiaji ni wengi, hoja ni nyingi Mhe. Naibu Waziri amechukua takriban saa nzima kutoa ufafanuzi wake, umeniomba na mimi nichukue saa moja kama sikuweza naomba univumilie niongeze kidogo kwa sababu nataka nitoe ufafanuzi wa kina hasa kwa wale Wajumbe ambao mwaka jana sikuwatendea haki ya kuwajibu vizuri.

Mimi nawashukuru sana kwamba mwaka jana hawakunipigia buti, na mwaka huu nawaomba wasinipigie buti. Mheshimiwa hakuna hata mmoja asiyejua umuhimu wa elimu, nawaomba Wajumbe wasimtizame Ali Juma Shamuhuna waitizame wizara.

Mhe. Naibu Spika, mimi nawashukuru wale wote ukiacha Waheshimiwa 3 na hata sitaki niwataje, lakini Waheshimiwa wote *statement* zao za mwanzo ni pongezi.

Mheshimiwa tunampongeza, Mheshimiwa na watendaji wake tunapongeza jinsi kadhaa wa kadhaa, lakini sasa, hizo lakini ni za msingi kabisa na wana haki ya kutoa hoja, wana haki ya kutushauri, wana haki ya kutukosoa na hilo nimelipokea kwa mikono miwili. Huo ndio utangulizi wa hotuba yangu.

Mhe. Naibu Spika, hotuba hii imechangiwa na Waheshimiwa wafuatao:-

Mhe. Farida Amour Mohammed
Mhe. Abdalla Juma Abdalla
Mhe. Mohamed Haji Khalid
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk

Mhe. Naibu Spika, nitaomba unipe ruhusa nimjibu mwanzo yeye mwaka jana nilimsahau, lakini sitaki nirejee kosa lile na hoja zake alizitoa ni nzuri na madhubuti za kujenga na majibu ninayo.

Mwengine ni:-
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Huyu hoja yake imeshazungumzwa na Mhe. Naibu Waziri. Lakini mimi nitaitilia mkazo kwa umuhimu wa hoja yake na hamasa zake za mchango wake alioutoa.

Mhe. Hija Hassan Hija, huyu alikuwa Makamo Mwenyekiti wangu katika Kamati iliyopita.
Mhe. Mgeni Hassan Juma, ambaye sasa ndiye Mwenyekiti wangu wa Kamati ya sasa hivi.
Mhe. Suleiman Hemed Khamis
Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
Mhe. Hassan Hamad Omar
Mhe. Saleh Nassor Juma
Mhe. Abdalla Mohammed Ali
Mhe. Asha Abdalla Haji
Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ni kigogo huyu wa kuuliza maswali na maswali ya nyongeza.
Mhe. Ali Salum Haji
Mhe. Rufai Said Rufai
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Ismail Jussa Ladhu, huyu ni kigogo cha Mji Mkongwe
Mhe. Asha Bakari Makame
Mhe. Salim Abdalla Hamad
Mhe. Salm Mohammed Ali
Mhe. Ashura Sharif Ali
Mhe. Salmin Awadh Salmin
Mhe. Subeit Khamis Faki
Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
Mhe. Mohammed Said Mohammed

Na wengine Mhe. Naibu Spika, waliochangia ni hawa :-

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora
Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo
Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Mhe. Naibu Spika, hawa wote nawashukuru sana kwa michango. Na pia nawashukuru wale wote waliochangia kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, lile ambalo Mhe. Naibu Waziri wangu hakupata kulitolea ufafanuzi, mimi nitajitahidi kulitolea ufafanuzi kwa muhutasari.

Waliochangia kwa maandishi ni:-

Mhe. Thuwayba Edington Kissasi
Mhe. Wanu Hafidh Ameir
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Nassor Salim Ali
Mhe. Mohammed Abdalla Ali
Mhe. Mlinde Mabrouk Juma
Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Kazija Khamis Kona
Mhe. Salma Mussa Bilali
Mhe. Salim Mohammed Ali
Mhe. Omar Ali Shehe
Mhe. Mbarouk Wadi Mussa

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuwataja hawa waliochangia kwa maandishi na kwa kusema, niwape heshima zao.

Mhe. Naibu Spika, hawa waliochangia kwa maandishi nitawachangia kwa ufupi sana.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niseme michango yao napokea na nimeifahamu na ahsanteni sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir ndio nilipokea maandishi yake ya mwanzo. Amezungumza vitu vingi vya maana sana pamoja na kutushauri. Lakini amezungumzia suala ambalo nitapenda nichangie kidogo kuhusu mporomoko wa maadili.

Mporomoko wa maadili Mhe. Naibu Spika, ni mkubwa kweli ni mkubwa kwa walimu, mkubwa kwa baadhi ya Walimu Wakuu lakini zaidi kwa baadhi ya wanafunzi. Najitahidi kupokea lile wazo lilitolewa mwanzo kuhusu adabu mbadala, na suala hili limechangiwa na kiasi watu watatu. Wengine wanasema iendelee kama swahibu yangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amesema Adabu Mbadala iendelee isiondolewe. Lakini Mhe. Abdalla Juma amesema Adabu Mbadala iondolewe na bakora zirejeshwe kwa sababu wanafunzi hawana heshima.

Ninachotaka kusema ni kwamba hili suala la Adabu Mbadala silo. Ndio tuliolipitisha kwamba Adabu Mbadala hapana. Tunalifanyia utafiti na tumechagua kama skuli 3 mpaka 4 kutoka kwenye bakora na kuja kwenye Adabu Mbadala. Kwa mfano Adabu Mbadala mwanafunzi wanafanya utovu wa nidhamu anaambiwa akapige matuta au akapalilie, akafagie skuli na kadhalika, wengine tunawafungia muda wa saa za skuli.

Imeonekana kidogo kwa upande mmoja inawaudhi hawa wanafunzi kuwafungia, kuwafagilisha, kuwalimisha na kadhalika. Kwa hivyo, tunaiona hii Adabu Mbadala inakidhi haja. Lakini kwa upande mwengine tumehisi hizi bakora kama alivyozungumza Mhe. Makame Mshimba wakati mwengine hatuzitumii kwa uadilifu tunazitumia kwa kisasi kikubwa na tunawaumiza watoto.

Kwa hiyo, watoto wanajenga uanafunzi na wazee wanajenga uadui kwa walimu. Sasa hilo tukaliona kwamba inafaa tuliondoshe au tulifanyie utafiti baada ya adabu ya fimbo twende kwenye adabu mbadala tuangalie itasaidia vipi.

Kwa hivyo, mawazo tafauti yaliyotolewa hapa ndio yanataposaidia na mengine tunayatafuta. Mpaka hatimae tunasema tukubali Adabu Mbadala au tunarejesha bakora. Lakini hivi sasa hatujaweka Adabu Mbadala kwamba ni ya kudumu.

Mhe. Hamza Hassan Juma ni msemaji mzuri na ni msemaji mkubwa. Lakini hakubahatika kuchangia kwa mdomo alichangia kwa maandishi. Ana hoja mbili au tatu. Anasema hili posho tunalowapa walimu wanaofundisha madarasa ya wanafunzi maalum. Posho hili la shilingi 5000 ni dogo mno halitoshi.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimwambie Mhe. Hamza Hassan Juma na kwa faida ya ukumbi huu Posho tumeliongeza kwa mujibu wa bajeti yetu ya mwaka huu tumetoka kwenye 5000 na tumekwenda mpaka 30000. Wizara yangu ni wizara sikivu maoni haya yametoka hapa katika masuala tunayajibu. Lakini Mhe. Hamza Hassan Juma leo kaona alilete kwa maandishi nimelipokea na sasa nalijibu. Kuanzia mwezi wa Julai kwenye bajeti hii tutakuwa tayari tutalipa shilingi 30000 badala ya shilingi 5000.

Mhe. Hamza Hassan Juma alimtetea mkandarasi fulani tuliyempa kazi na tukamlipa asilimia 90 ya gharama za kazi tulizompa sijui kama Mhe. Hamza Hassan Juma kama anajua imebakia asilimia 10. Na kawaida yetu huwa tunazuia asilimia fulani ili tutizame kazi kama amemaliza au hakumaliza.

Na hapa pia namjibu Mhe. Hija Hassan Hija lile jawabu langu la nyongeza zaidi la lile jibu alilojibu Mhe. Naibu Waziri Skuli kule Pemba. Tulipozuia asilimia fulani ya gharama za kazi tunazozitoa basi huwa tunahakikisha tunatizama kazi iliyofanywa imemalizika na tumeridhika na kama tumeridhika tunakabidhi malipo.

Mhe. Hamza Hassan Juma mkandarasi huyu tumemlipa shilingi sabini na tisa milioni mia tisa sabini na nne na mia saba na arubaini na tano. Na tumezuia asilimia kumi ya kazi zake. Huyu kuna kazi hajazimaliza na anajua tushamuita tumeshazungumza naye na kaahidi atakamilisha. Mhe. Hamza Hassan Juma nataka nikuthibitishie atakapokamilisha kazi hizi tukiridhika fedha tunazo na tutamlipa pesa zake.

Mhe. Hamza Hassan Juma tumesema hapa tusipokupa maelezo ya kutosha utazuia kifungu. Maelezo ya kutosha ndio hayo. Huyu tutamlipa pesa zake akimaliza kazi iliyobakia na si kubwa imebaki kidogo tu. Nakuomba Mhe. Hamza Hassan Juma usizuie kifungu. Mimi na yeye tumetoka mbali sana sasa leo tena uje kuzuia kifungu changu si mambo makubwa hayo.

Mhe. Nassor Salim Ali amezungumzia kuhusu suala la nyumba. Suala hili la nyumba tumeliangalia vizuri sana lakini uharibifu wa mazingira ni mkubwa, mchanga umechimbwa pale wiki moja iliyopita kulikuwa na kikao cha Mkuu wa Mkoa na Mkurugenzi wetu wa Utumishi na Maafisa mbali mbali akiwemo Mkurugenzi wa Manispaa na kadhalika.

Sasa ushauri utatekelezwa na pale Lumumba na patarejeshwa katika hali yake ya zamani. Kweli kabisa pana magereji ya ajabu ajabu wamehamia kinyemela, sasa hawa tutawaondosha. Kuna wachimbaji mchanga kuna maeneo yetu tumeyawekea vyuma lakini vyuma vimeng'olewa, watu ndio wanafanya njia ya kupita, tutawashughulikia hawa na hatua nyingi zaidi tutachukua, tutahakikisha kwamba Lumumba inarejea katika hali yake.

Mhe. Naibu Spika, amesema hali mbaya sana ya majengo yake ya Skuli ya Mwembeladu. Mimi nakubali hali mbaya lakini vijijini ni hali mbaya sana, na kila mwaka tunaweka sehemu ya fedha za kuzikarabati. Tunakarabati moja baada ya moja.

Mheshimiwa hivi juzi ulikuja na kilio chako cha kuvuja skuli zako, sasa safari hii kile kimenyamaza kwa sababu tumetengeneza, tutafanya hivyo moja baada ya moja kadri ya nafasi zitakavyowezekana.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma kaniuliza skuli yake ya Pangatupu mbona kimya mpaka leo. Kwanza kuna skuli ndogo haijamalizwa. Lakini pia kuna skuli tumeizungumza ambayo imeahidiwa na Falme za kiarabu na tunapitisha skuli hizi mbili moja ni Pangatupu na Skuli nyengine Micheweni. Mara tu baada ya kupata wapimaji tunawapelekea wahisani watakuja kumaliza hiyo kazi.

Mhe. Fatma Mbarouk Said nakushukuru kwa kuipongeza wizara yangu, lakini kama walivyofanya wengine wote mpaka Mhe. Ismail Jussa kaipongeza

wizara yangu, nasikitika sana Naibu Waziri wangu hakuwahi kujibu mimi nitajitahidi kadiri ninavyoweza.

Mhe. Fatma Mbarouk Said ameipongeza lakini…

TAARIFA

Mhe. Ismail Jusa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, kuhusu hili la kifungu Mhe. Naibu Waziri kaniletea nakala zote kama nilivyokuwa nataka nimepokea maelezo yote. Kwa hivyo, nampunguzia kazi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mhe. Mwakilishi wa Mji Mkongwe nakushukuru sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said mafanikio yatapatikana katika skuli zetu yamechangiwa sana na wananchi mbali mbali wakiwemo na Wawakilishi. Nakubaliana na hilo kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nitoe kauli rasmi kwamba Wawakilishi na wananchi nawapongeza sana na nawashukuru sana. Walipokutana katika skuli na katika kamati zao za mitaa kazungumzia suala la mabanda na kadhalika, kazi hiyo itakwenda kwa kasi kubwa sana. Kiasi ambacho Mhe. Naibu Waziri ni aibu kusema lakini naomba radhi sana. Sioni aibu kusema kwamba sisi wizara tuko nyuma kutelekeza hizi kazi wanazofanya wananchi lakini kutokana na uwezo wa bajeti zetu.

Lakini nathubutu kusema kwamba tunahitaji kuzirekebisha skuli hizi moja baada ya moja. Na bado tutaendelea na wala hatuwasimamishi wananchi wasiendelee kujenga Mhe. Ibrahim Makungu hapa alitwabia bora sasa tusite kujenga hizi skuli, kwa sababu nyingi hatuzikamilishi kila siku kazi yetu kujenga tu. Lakini pale pale Mhe. Ibrahim Makungu akasema skuli yake ina wanafunzi 150. Sasa tujenge au tusijenge? Tuendelee kuwa na skuli za wanafunzi 150, mwalimu huyu ana kipaji gani cha kuwasomesha wanafunzi hao.

Mhe. Ibrahim Hussein Makungu katika hili tusiwazuie wananchi kujenga maskuli na sisi tutajitahidi hivyo hivyo kila mwaka kuongeza bajeti. Bajeti ya mwaka jana na mwaka huu tafauti na *inshaallah* na mwakani itakuwa tafauti itakuwa kubwa zaidi ili kuzisaidia skuli hizi kujengwa.

Skuli hiyo inayo wanafunzi 150 ni yako wewe, Skuli ya Kijitoupele nayo pia ndio siri iliyopo skuli za msingi zote za Kijitoupele zote zina wanafunzi 150. Serikali ya Jamhuri ya watu wa China tumekubaliana na watatujengea Skuli

moja kubwa ya ghorofa Fuoni. Skuli hiyo ikimalizika tatizo tulilonalo Kijitoupele inaondoka najua bado watu wanazaliwa na wataongezeka lakini tunajitahidi.
Mhe. Omar Ali Shehe suala la Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, umezungumzia skuli zetu 19 kujenga. Mchango wako ulikuwa mkubwa na mzuri sana nakushukuru sana na nakupongeza sana kutokana na wakati nilionao ni finyu, ushauri ulioutoa, pongezi ulizotoa na maelekezo yote tunayakubali, tunayapokea na tutayafanyia kazi.

Mhe. Salma Mussa Bilali umetupongeza kwa kuhakikisha Vyuo vya Qur-ani na Vyuo vya msingi tunavihudumia na pongezi hizi zimetolewa na Mhe. Kazija Khamis Kona alinikumbusha ziara ya Mhe. Rais Tumbatu, na sisi tunaikumbuka na tunajitahidi kwa upande wa Tumbatu kulikarabati hili jengo na tumejitahidi kuwa karibu nao na Mheshimiwa hayupo hapa. Lakini nataka nimthibitishie ombi lake la kuitembelea Tumbatu tumelipokea wala sitangojea Mfunguo sita wakati wa maulid hapana. Tukimaliza Ramadhani tutafanya ziara ya Tumbatu na Makunduchi zaidi ya zile ziara ninazofanya mwenyewe kila ninapopata nafasi.

Ametushauri Mhe. Kazija Khamis Kona hapa kama Walimu Wakuu wasikae sana katika skuli zao kila baada ya miaka mitano waondoshwe. Mhe. Naibu Spika, tumeupokea ushauri tutauzingatia.

Ameshauri kipindi cha watoto wakizungumze sana katika redio tunafanya hivyo pamoja na kile kipindi cha "*Tucheze Tujifunze*" kwa hivyo, nimepokea ushauri wako.

Mhe. Salma Mohammed Ali ametukumbusha kwamba katika Skuli ya Ole kuna jengo ambalo katika ziara ya Mhe. Rais Afisa Mdhamini alitoa ahadi sasa na mimi nitahakikisha kwamba Afisa Mdhamini anafanya kazi yake sio kuhakikisha tu. Vizuri safari hii katika bajeti yetu ya Pemba tumeipeleka Pemba wenyewe na Afisa Mdhamini ndiye Mkuu wa bajeti hiyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa tumelipokea ombi lake au agizo lake na *inshaallah* siku zijazo na sio nyingi tutatekeleza kauli hiyo. Ametaka tumjulishe ni maombi mangapi yaliyopelekwa kwa kutaka mikopo, bila shaka kutoka huko Ole. Nafikiri kwa sasa takwimu sina, lakini nitamjibu na hili nitajirekebisha sitosahau, nitajibu hata kabla ya kikao chengine cha bajeti ya kawaida nitakujibu.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad, huyu alishauri kuhusu mafao, ametuhimiza tushirikiane na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

hatuna matatizo na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Katika hotuba yangu nilisema kuwa tunapata mashirikiano makubwa sana na wizara hii na fedha tulizoomba hususan katika shughuli za maendeleo na kazi za kawaida kwa kiasi kikubwa sana tumezipata, hatuzipati zote lakini kwa kiasi kikubwa sana tumezipata.

Kwa hivyo, katika mazungumzo yangu nilimuomba Waziri na ninamuomba tena kwa sababu hapa yupo na hilo wala sina matatizo nalo, tutaendelea kushirikiana. Mhe. Waziri anaujua umuhimu wa wizara yangu kama Wajumbe nyote mliokuwepo hapa mnavyoijua na ndio maana mkaichangia sana, kwa sababu hiyo Mhe. Mohamed Mbwana Hamad usiwe na wasiwasi. Mhe. Mohammed Haji Khalid hoja zako zote zimejibiwa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika hoja za Mjumbe mmoja mmoja, niahidi nitaanza na swahibu yangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Nimekuja na silaha zangu. Katika mchango wa Mhe. Makame Mshimba alizungumzia suala la skauti na hili analizungumza sana. Alituandikia barua alisikitika na hatukumjibu mpaka leo.

Mhe. Naibu Spika, nataka nithibitishe jibu la barua tulioandikiwa ni hili hapa, na aliyetuandikia sio Mhe. Makame Mshimba, aliyetuandikia ni Khamis A. Khamis ambaye ni Kiongozi wa hiyo kamati ya eneo hilo linalozungumzia suala la skauti ya elimu. Tulimjibu baada ya miezi miwili, sio kwamba mpaka leo hatujamjibu na jibu letu lilikuwa hivi.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali halihusiani na kuanzisha shughuli za skauti na kuna toleo lilitoka la serikali, kuwa shughuli hizi zimezuiliwa zisifanywe na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuna wizara ya Mhe. Zainabu ndio inayoshughulikia masuala haya ya skauti na bi Zainab ameninong'oneza kuwa yuko mbioni kulianzisha suala hili. Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa namuomba Mhe. Mshimba amshauri huyu bwana aliyetuandikia hii barua, kwamba barua yake sasa ai-*review* aipeleke kwa Mhe. Zainab Omar, lakini kama kuna mchango mwengine wowote ambao Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inatakiwa ifanye, mimi nitakuwa mtu wa mwanzo kulisaidia suala hili.

Mhe. Naibu Spika, suala la pili la Mhe. Makame Mshimba lilikuwa ni suala la maendeleo ya skuli, maendeleo ya mchezo, akasema suala la michezo linahitaji kusimamiwa vizuri, kwa sababu huko ndiko tutakakoweza kupata vipaji. Mhe. Naibu Spika, hoja zilikuwa nyingi.

Vile vile alizungumzia suala la kuimarisha michezo. Nataka nimuhakikishie kwamba hilo tutalifanya kwa uwezo wetu. Nimemuona Mhe. Mshimba. Mhe.

Mshimba aliuliza ile *Global Fund 5.2 millions* msaada ule, alitaka kujua utatumika vipi na tumeupanga vipi. Ule msaada bado hatujakabidhiwa tumekabidhiwa ahadi, na bila shaka wenzetu wakiahidi wanatekeleza na tumeseme pesa hizi zitatumika katika kuimarisha skuli za msingi na za maandalizi.

Wachangiaji wengi walizungumzia suala la kuimarisha skuli ya maandalizi na msingi. Walisema pamoja na kushughulikia vyuo vikuu na skuli za sekondari, lakini tusipozishughulikia skuli za maandalizi na msingi tutapata *product* mbovu katika skuli za sekondari.

Waheshimiwa wengi walichangia hili na mimi nakubaliana nao kwa asilimia 100, na ndio maana kwa kuanzia hizi *5.2 millions USD* tunazipeleka huko. Pia alizungumza walimu wetu tuwapatie mafunzo mara kwa mara. Katika hotuba yangu ya bajeti niliwataja hasa, walimu watakaopatiwa mafunzo walioko mafunzoni ni watano. Kwa hivyo, *refresher course* kwa lugha nyengine ni muhimu sana, walimu wetu ni lazima wapate *refresher course* ili wajikumbushe uwezo wao tupate hatma nzuri kwa wanafunzi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kitengo cha michezo hiki hapa nimeshakiona, nimeshakichangia. Fedha za wahisani amezungumza tuzitunze mnatuletea nyingi, lakini sisi serikali tunatoa kidogo, kwa hivyo tuvitunze na tuvitumie vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe, ingawa amesema katika Jimbo lake la Kitope hakuna skuli ya wilaya. Ni kweli kabisa, lakini Kaskazini 'B' kuna skuli moja ya wilaya, na kwa hivyo Mwenyezi Mungu akitujaalia miaka ijayo tutaliangalia suala hilo. Lakini hii ni kuthibitisha na kuonesha jinsi pesa za wahisani tunavyozitumia vizuri, hususan mkopo wa *World Bank*. Tuseme tutakavyosema na mtakavyosema vyovyote mimi nitapokea, mmesema kuna skuli nyingi tumezijenga nzuri lakini hazina maabara, hazina *library*, wala hazina chochote. Katika skuli za wahisani za *World Bank* mkopo, skuli zote kila moja ina maabara, ina *library*, ina chumba cha mikutano na ina nyumba tatu za walimu.

Mhe. Naibu Spika, katika awamu ya pili inayokuja tumeshazungumza na *World Bank* na wao wamekubali kimsingi kutokana na namna tunavyozitumia pesa katika awamu ya kwanza. Awamu ya pili pesa tutakazozipata tutatumia kwa kujenga nyumba saba za walimu zilizobakia, tulikubaliana tujenge nyumba 10 kila skuli, basi tumejenga nyumba 3 kwa kila skuli na zimebakia nyumba 7, tumeziweka katika awamu ya pili.

Vile vile tumekubaliana tujenge uzio, na tumezungumza sana suala la uzio kwa skuli hizi na pia skuli nyengine tutajenga uzio katika hiyo awamu ya pili.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mshimba alizungumzia *SACCOS* ya wizara ya elimu ipo, sawa, imefanya kazi nzuri ya kuwakopesha walimu vipando na vifaa vya ujenzi, je wananchi vipi? Mhe. Mshimba nataka nimuambie kwamba *SACCOS* za wananchi zinashughulikiwa na wizara ya Maalim Haroun na ziko nyingi, na Maalim Haroun anazishughulikia. Alichotaka yeye, kwa sababu mimi nime-*approach* anipatie na mimi msaada. Alichotaka yeye *SACCOS* kwanza isajiliwe, itambuliwe na iwe na mfumo madhubuti. Sasa Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Mjumbe aonane na Maalim Haroun kama ana *SACCOS* zake 2 au 3 amuendee atapata ushauri mzuri.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa nakushukuru sana kwa michango yako. Mhe. Naibu Spika, natumai Mhe. Mshimba safari hii ameridhika na hoja nilizojibu michango yake.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa nimepokea pongezi, alisema katika maktaba zetu hasa ile ilioko pale mjini haina vitabu vya kutosha, akazungumza kwamba Pemba hakuna maktaba tuhakikishe kipindi hiki tunajenga. Ametoa pongezi sana kwa wizara ya elimu kushughulikia habari ya skuli ya maandalizi. Vile vile ametushauri tujitahidi kutafuta hati miliki za maeneo yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kadiri tulivyoweza maktaba yetu ya Unguja kwa kiasi kikubwa ina vitabu vya kutosha, ina *facility* za kompyuta za kutosha, na *Alhamdulillah* wananchi wameitikia wito wetu wa kuhudhuria katika maktaba hii. Sasa pamoja na hayo napokea ushauri wake na Mkurugenzi wetu wa maktaba yupo na amesikia. Ile *association* ya *Book aid* kila tukikutana nayo tutaendelea kuwaomba watusaidie hivyo vitabu na sisi wenyewe vile vile tutanunua, lakini nataka nimuhakikishie kwa sasa vitabu viliopo si haba.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa maktaba Pemba nimeshasema. Mwaka jana swahibu yangu Mhe. Hija Hassan alinibana sana katika kamati ile, akasema fedha tulizotenga kwenye maktaba Pemba ni kidogo sana, tuzihamishe tuzipeleke kwengine kwenye maana, lakini zile haziwezi kufanya jambo lolote. Mimi nikamsikiliza, lakini Mhe. Naibu Spika, hatujazihamisha zile fedha zipo. Mwaka huu tumeomba fedha nyengine si haba na ujenzi wa maktaba Pemba kama haujaanza basi tukimaliza bajeti unaanza. *Alhamdulillah* nataka nimthibitishie Mhe. Hija Hassan pesa mara hii zipo na tukianza tunamaliza hatusiti.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla umeshajibiwa na Mhe. Naibu Waziri. Mimi cha kuongezea nimekusikia kilio chako, usizuie fungu langu, nakuomba sana Viwe usizuie fungu langu. Tutaendelea kusaidiana na kwa mujibu wa takwimu tulizonazo kilio chako tumekitekeleza vya kutosha, lakini hoja yako tumeifahamu inayohusiana na kilio chako tumeifahamu, ulitunong'oneza tumefahamu tutaitekeleza.

Vile vile Mhe. Viwe Khamis ulizungumza kuhusu TUTU sasa ianze saa 12 ameshajibu Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Naibu Waziri alijitahidi kujibu masuali yako, lakini alijibu suala la Skuli ya Sekondari ya Madungu. Kama nilivyomjibu Mhe. Hamza Hassan Juma, tulipotoa *contract* hizi, kuna kifungu asilimia fulani tunazuia ili kuhakikisha wanapotukabidhi kazi wameimaliza kwa asilimia 100. Hawa watu wa Mhe. Hija Hassan Hija au ile skuli ya Madungu *contractor* tumeshakutana naye, kazi aliyoifanya hatukuridhika nayo, hatukumlipa fedha zake kwa asilimia 100 na hivi karibuni atakuja kufanya marekebisho ya zile sakafu. Mheshimiwa wewe ulipozungumza mavumbi, nilishtuka nikasema sijui tutafanya vipi ikiwa mavumbi haya yanaletwa na zile gari zinazopita zikipituka yanaingia darasani mavumbi sijui tutafanya vipi, lakini kumbe mavumbi yenyewe ni maeneo yale ya sakafuni. Hilo Mhe. Mjumbe nataka nikuthibitishie tutalirekebisha haraka sana na *contractor* tumeshaonana naye na tumeshazungumza naye.

Mhe. Naibu Spika, masuala mengine Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu ajira Pemba za walimu, kuwa tunazitoa kwa upendeleo, na hivi na hivi. Mhe. Naibu Spika, sababu ya kusema shughuli hizi za ajira tupate maoni kutoka Wilaya za Pemba zenyewe, wao wenyewe wanalalamika. Hizo wilaya za Pemba na viongozi wa skuli za Pemba wanalalamika, kuwa mnawaajiri watu kutoka Unguja wa Pemba mnawaacha, mnatuletea kutoka Unguja kuja Pemba wakifika tu wanarudi wanaomba uhamisho. Tukaona kuondosha matatizo haya sasa tuwape wenyewe. Wilaya za Pemba na Wilaya za Unguja wao ndio wanaotuletea zile orodha za wale watu ambao wa kuajiriwa. Lakini jamani tukitaka tusitake, idadi ya wanafunzi wetu wanaohitimu kusomesha ualimu ni kubwa mno.

Mhe. Naibu Spika, tumepata kibali cha kuajiri watu 400, tumeombaomba tukapata tena kibali cha kuajiri watu 150 wa *primary* skuli. Sisi walimu wa *primary* skuli waliohitimu ualimu tuna zaidi ya 2,000, kati ya 2,000 tutaajiri 150. Ni kweli utasema tunapendelea tutafanya nini? Ni kweli hatuna njia. Sio hatuna njia tusifanye upendeleo, hatuna njia ya kwamba ni lazima kuna wengine tutawaacha.

Mhe. Haji Omar Kheri namshukuru sana kwa ufafanuzi alioutoa, mimi namuunga mkono kwa asilimia 100. Kama bado kuna walimu waliosomea, wana vyeti vilivyokamilika, hawana matatizo na tena ni walimu wa sayansi tuwaorodheshe tutazungumza naye, ameshatuahidi hapa tutazungumza naye atatusaidia. Nina hakika hawezi kutusaidia kuondosha tatizo hili kwa asilimia 100, lakini tutapunguza.

Mhe. Hija Hassan Hija ulizungumza suala la mwalimu wako mmoja kutoka Mwambe, tena mwalimu huyo ni wa sayansi mpaka leo hajaajiriwa na tena kaomba muda mrefu. Nakubali, nimepokea hoja yako na nitaifanyia kazi kweli kweli wala sio masihara. Nitizame hivi kwa nini hajaajiriwa mpaka leo hakuna kosa jengine, cheti chake kiko safi, kapasi? Sasa kama cheti kiko safi kapasi tena mwalimu wa sayansi ambao tunawataka kwa nini hajaajiriwa. Suala hili nitalifuatilia binafsi kwa nguvu zangu zote, ili nihakikishe kama huyu mwalimu hana matatizo basi tutampelekea Mhe. Haji Omar Kheri atupe kibali.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri muda umebakia dakika tano, kwa hivyo ufupishe ili tupate kuanza vifungu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: *Inshaallah.* Sijafika hata nusu. Lakini Mhe. Naibu Spika, nilisema hii wizara ni kubwa ina maidara mengi, ina vifungu vingi. Kuna vifungu zaidi ya 500 vimejadiliwa hapa, sasa kuweza kuvijibu vifungu vyote hivi kwa muda wa saa moja kama walivyofanya wenzangu wenye idara nyengine ni ngumu, lakini pia naheshimu maamuzi yako na Wajumbe vile vile wanistahamilie.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wengi waliuliza akiwemo Mhe. Ismail Jussa Ladhu na wengine kuhusu suala la hii ripoti ya Tume ile iliyoundwa na Waziri Mkuu, na mimi nilisema nitafanya kongamano ya kimataifa, kulizungumzia suala hili la wanafunzi wetu kufeli, hapana sio kufeli ni kufelishwa. Maana tuliporekebisha mbona wengine wamepasi. Wanafunzi wengi waliofeli nilisema nitafanya kongamano la kimataifa, azma ile bado ninayo na hii kazi sasa tumewapa SUZA wanajiandaa. Lakini tulikuwa tunasubiri tupate hii taarifa au ripoti hii kutoka kwa Waziri Mkuu, na ripoti hii imeshapatikana na imeshatolewa anayo Waziri Mkuu, anayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na anayo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Sisi wizara bado hatujapata ripoti hii wala hatujaiona, hilo ni moja ambalo lililonikwamisha kwamba huu mkutano nisiuitishe bado.

Lakini la pili Waheshimiwa Wajumbe mnaelewa kwamba kabla ya kufanywa hayo mabadiliko ya *result* nilitembelea wilaya zote 10 za Unguja na Pemba, na nikazungumza japokuwa mwenzangu hapendi neno hili, lakini ndio lipo na

lugha inakuwa, lugha sio *static*. Alizungumza juzi Mhe. Nassor Ahmed Mazrui vizuri sana, kule kwenye vikao vyetu.

Mhe. Naibu Spika, wadau wengi niliwashirikisha nikakutana nao katika hizi wilaya. Mambo ya msingi tulizungumza kwa nini watoto wetu wamefeli? Tukazungumza jukumu la wazazi, tukazungumza jukumu la Walimu Wakuu na pia tukazungumza jukumu la walimu wetu, lakini pia sikusahau kuzungumza jukumu la wanafunzi wetu. Mhe. Naibu Spika, tathmini ya vikao vile vilifanikiwa sana na kila tulipoondoka walikuwa wanatushauri tusikae muda mrefu kabla hatujarudi tena kufanya vikao vya namna ile na mimi nikawaahidi.

Mhe. Naibu Spika, sisi tulichukulia kwamba kwa sababu tumeshafanya vikao vya wilaya zote, na tunalotaka kulizungumza kwa ule mkutano mkubwa wa kitaifa ndio tumeshazungumza na wilaya zote 10, tulichukulia kwamba kwa kiwango kikubwa tumeshamaliza ile kazi. Lakini hoja yenu inatukumbusha kwamba ahadi ni deni. Waheshimiwa wote mliochangia suala la mkutano ule wa kimataifa nilioahidi, nasema tukishaletewa ile taarifa ya ile Tume tuliyoiunda ya Waziri Mkuu, tukishaletewa tutaiangalia, tutaijadili, tutaisoma na tutaiingiza katika mkutano wetu, maana ile ndio ajenda muhimu ya kuiingiza katika huo mkutano wa kitaifa. Lakini mkutano upo na tumewakabidhi Chuo Kikuu cha Taifa SUZA wanauandaa.

Mhe. Naibu Spika, basi nakubaliana na hoja yako kwamba nisite hapa kutoa michango hii ili tuanze sasa kujadili vifungu. Lakini naomba nimalizie kwa kusema naiheshimu michango yote iliyotolewa na ningepata muda wa kutosha, basi ningejadili sana mchango alioutoa swahibu yangu Mhe. Saleh Nassor Juma mkereketwa mkubwa, na pia ningeujadili mchango mzuri sana alioutoa Mhe. Salmin Awadh Salmin. *(Makofi)*

Katika siku Mhe. Salmin Awadh Salmin ameamka vizuri basi ni jana. Kwa kweli mchango wangu nikitumia lugha ya kigeni ulikuwa *extremely constructive*, na la mwisho nililolipokea ni kwamba ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa asilimia mia moja, na pale alinipa faraja ya kwenda kulala nikapata usingizi mzuri. *(Makofi)*

Lakini leo nakuombeni wenzangu kwamba ningepata muda wa kutosha basi ningejadili hoja yenu moja baada ya moja na nyengine hoja zenu zote ambazo mumezitoa hapa. Mhe. Naibu Spika, hakuna hoja hata moja safari hii iliyozungumzwa kwa ukali au hamasa na kadhalika, yaani hoja zote zilikuwa za kujenga. *(Makofi)*

Mhe. Naibu spika, nataka nitoe ahadi na watendaji wenzangu wananisikia. Kwanza wachangiaji walisema, walitusifu kwamba tunao ushirikiano mzuri, tunafanya kazi kwa pamoja na kadhalika na hilo ni kweli kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nilivyokuja mwaka jana sivyo nilivyokuja mwaka huu, kwa sababu mwaka jana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nilikuwa nikiiogopa na hata kuizungumza vya kutosha, lakini mwaka huu hapana, kwa sababu tayari nimeshaifahamu na ninaiweza na haya yanatokana na wenzangu kunipa ushirikiano mkubwa sana hususan Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wote ninawaomba sana hawa wenzangu waendelee kunipa ushirikiano, na kazi tuliyopewa ni nzito na lazima tuitekeleze.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja, ili iamuliwe. Kwa hivyo, niwahoji wale Wajumbe waliokubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2013/2014 wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya wizara yangu. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitia vifungu kimoja baada ya kimoja vya bajeti yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 23 – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	15,000,000/=
Jumla ya Fungu		**15,000,000/=**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0401

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kutoa hoja yangu, ambapo Mhe. Waziri anilijibu lakini bado sijaridhika.

Mhe. Waziri alisema kwamba katika mwaka 2012/2013 kulikuwa na mafanikio ambayo yamepatikana, amenijibu lakini bado sijaridhika, na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani ambao wamenichagua basi nikasema nisimame tena kwa sababu nilikuwa na mengi ya kuyachangia.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na wakati na Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wenyewe mnatuambia kwamba muda ni mdogo na tunakubali kwa hayo, na kwa bahati nimechangia madogo tu na nikamuomba Mhe. Waziri anitolee ufafanuzi.

Kwa hivyo, ufafanuzi wenyewe ni kwamba baada ya kuwa mafanikio yametajwa mbali mbali ya wahisani, lakini bado na sisi kama ni Wawakilishi na hilo ni jukumu letu katika Baraza hili ni kwamba ni lazima tuwajibike kwa yale ambayo tumeyaomba kwa wananchi.

Kwa kweli niseme Mhe. Waziri amenijibu na kutokana na hali ya kwamba ukarabati wa maskuli amesema, ujenzi wa skuli za sekondari za ghorofa, ukarabati wa skuli za sekondari Forodhani. Mhe. Mwenyekiti, haya yote ni moja ya majumuku ambayo serikali imefanya.

Lakini sisi kama Wawakilishi mimi na Mbunge wangu ambaye nitakuwa sikumtendea haki kama sikusema hapa. Mhe. Mwenyekiti, tumeyaangusha madarasa matatu na wenzangu hapa wamepiga kelele hapa sehemu tofauti wanangojea serikali.

Sasa kwa kujua majukumu yetu, basi tumeyaangusha madarasa matatu na tukayajenga mpaka kusimama, na haitoshi baada ya hapo *procedure* tumefuata na baada ya hapo tumeshamaliza sasa na hili nataka Wizara ya Elimu kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba iliondolee kabisa kusema kwamba wananchi wajitolee na baadaye wao watawaunga mkono, kwa sababu tunaona kwamba haliwezekani na kwa majibu aliyosema Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, ninaomba Mhe. Mwenyekiti, kabla hawajatoa ripoti zao hizi basi lazima wapitie na maskuli kuwauliza angalau walimu wakuu, ili hizi ripoti ziwe sahihi. Kwa maana hiyo, baada ya hapo tumefanya kazi hiyo na *procedure* tumezifuata, lakini hata mwisho kutokana na hali tuliyoiona kwamba madarasa yale yamechoka na tukaogopa kuja kupata maafa ambayo baadaye tungekuja kupewa pole.

Mhe. Mwenyekiti, ninaomba Mhe. Waziri atueleze ni kwa nini hawajakaa na Walimu Wakuu wakatoa ripoti hii ama hotuba hii bila ya kuzingatia, na sisi kama Wawakilishi na Wabunge tunalo jukumu la kufanya kazi kama hizi. Kutokana na hali hiyo, naona bado hajanijibu swali langu, hivyo naomba anijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni kweli katika mchango wake wa maandishi Mhe. Fatma Mbarouk Said alizungumza kutotajwa kwa majengo ambayo yamemalizika. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kawaida Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali huwa hatutaji kuwa Mhe. Fulani amechangia kitu fulani na Mhe. Fulani amechangia kitu fulani. *(Makofi)*

Kweli mimi binafsi nilikwenda kukagua jengo hilo na nikaliona ubovu wake na yeye mwenyewe akatuletea barua pamoja na Mhe. Mbunge wake kwamba wanataka kulitengeza jengo lile, na tayari wamelitengeneza ijapo kuwa hawajakabidhi wizarani rasmi.

Lakini huchukulia mchango ule kama ni wa walimu na Kamati ya Skuli, kwa sababu ndio wanaokaa wakapanga bajeti zao wakapitisha na wanapojenga wakajenga na wanapobakisha tukaenda tukamaliza. Kwa hivyo, sisi huwa hatumtaji kama Mhe. Fatma umechangia skuli fulani na tukatia kwenye bajeti yetu, isipokuwa huwa tunazungumza kwamba skuli fulani imejengwa, na sisi kama wizara tumemaliza. Kwa hivyo, tunatambua kama wizara kwamba Mhe. Fatma Mbarouk Said pamoja na Mbunge wake wameijenga skuli ile na tunaomba sasa watukabidhi rasmi. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na kwa majibu aliyotoa Mhe. Naibu Waziri kwamba hatujakabidhisha. Kwa kweli baada ya kumaliza kazi hiyo basi tuliituma Kamati ya Wazee ya Skuli, ili sasa baada ya kufanya kazi ile kubwa ambayo kabla ya kuimaliza tuliomba msaada pia kutoa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba watusaidie, sasa tatizo ni kwamba hawakuthamini ule mchango wetu tuliochangia pale.

Lakini tunachokiomba angalau tulitaka kwamba waje pale tukabidhiane lile jengo na baadaye pia zikatokea *complain* kwamba sisi tumejenga lile na ilikuwa hakuna haja ya kuliangusha chini na kumbukumbu zipo, yaani kabla hatujajenga lile jengo, lilionesha hatari kwamba jengo lile wakati wowote linaweza kuanguka.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja yako.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba Mhe. Waziri masuala ya kusema hatukuwakabidhi, yaani mpaka leo hatujafanya makabidhiano na baada ya kuona wizara wenyewe tumepeleka na wala hawakutujibu, basi tunaona aa! *Tenda wema wendezako*. Kwa hivyo, mimi kwa haya kwa hii leo nasema tunapitisha na tuendelee, lakini suala hili Mhe. Waziri alikubali Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante jana wakati nilipokuwa nikichangia ukurasa wa 73 kuhusu Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha nililalamika kuhusu mchango wa walimu wanaosomesha katika mazingira haya.

Kwa kweli nimechangia suala hili kwa sababu kuna malalamiko ya wanafunzi wenye mahitaji maalum wanakwenda skuli, lakini wanaambulia kukusanyika tu na wenzetu tatizo kubwa ni vifaa pamoja na walimu wenye ujuzi. Je, serikali imejipanga vipi kuhusu suala hili na wala sina nia ya kutaka kuzuia kifungu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, suala hilo ni kweli alilichangia Mhe. Mjumbe na mimi nilitoa ufafanuzi mkubwa sana.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba wanapouliza masuala yao wakati tunapojibu, basi wawepo ndani ya Baraza, ili wasikilize kile ambacho tunajibu.

Vile vile Mhe. Mjumbe nilimwambia kwamba hivi sasa Mhe. Mwakilishi mimi nimekujibu na Mhe. Waziri atakujibu mpaka ile posho ambayo tumeongeza kwa hawa wafanayakazi wetu hawa ambao wanawasaidia watoto wenye mahitaji maalum kutoka shilingi 5,000/= mpaka 30,000/= Mhe. Mwenyekiti nilijibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu sio hivyo, na kwanza nataka nimpe pole kwa kubadilisha hata viatu Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sema kwenye *microphone* na ukizungumza bila *microphone* ni tatizo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimeshamwambia kwamba serikali imejipanga vipi kuongeza walimu kutokana na hivi sasa walimu wamekuwa kidogo na wakaenda kule wanafunzi wanakaa madarasani wanashindwa kutwa tu na wala hawaambulii elimu yoyote wanayoipata.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, hoja ya kuongeza walimu madarasani na wanafunzi wengine wanashinda hawana walimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, niliijibu hoja hiyo na nikaeleza idadi ya walimu ambao tunao na wangapi wako masomoni na vipi ambavyo tunatarajia kuongeza walimu hao. Kwa kweli orodha kubwa sana ambayo itatuchukulia muda nikisema nirejee kile nilichokizungumza, kwa hivyo, nitampa hapa kwa maandishi, ili ajisomee mwenyewe kwa sababu nililijibu na yeye alitoka nje hakusikia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumza sana mchango wangu katika haja ya kuangalia tena Sera yetu ya Elimu, Mitaala na Mihutasari ya Masomo. Lakini nimepata ufafanuzi kwanza kutoka kwa maalimu wangu aliyekuwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Haroun Ali Suleiman, na baadaye kwa kiasi fulani kwa Mhe. Naibu Waziri pamoja na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali hasa maelezo yake ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa bado ninasema kwamba katika majibu yaliyokuwa yametolewa inaonekana ni kama vile tunachosema ni kwamba matatizo hayapo katika mfumo, isipokuwa yapo katika utekelezaji.

Kwa hivyo, mimi bado nataka maelezo ya Waziri muhusika au Naibu Waziri wake juu ya hoja hiyo ambayo nimeitoa, kwa sababu Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika ametusaidia kwa uzoefu wake, lakini Mhe. Mwenyekiti hoja alizonijibu na ninaheshimu kwamba ni sehemu ya serikali, bado naona hazikujibu ule msingi hasa wa wasiwasi nilionao wa matokeo mabaya tunayoyapata hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tunafupisha muda na niseme tu kwamba nilikuwa nimekusudia buti kama 22. Lakini kutokana na hali niliyoiona nimeamua kuzipunguza mpaka 2, yaani hii niliyosimama na nyengine 1, pia nitawaomba wenzangu kwa kiwango hicho cha asilimia wakipunguze, ili tumsaidie Mhe. Waziri kwa ajili ya kwenda kuendelea na shughuli zake. *(Makofi)*

Sasa naomba hili nisaidiwe Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema mfano mmoja tu, kwamba katika kujibu hoja yangu Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika alizungumzia mfano wa vitabu nilioutoa, na

alisema kuhusu vitabu kwamba havina matatizo na viliandaliwa kutokana na msaada wa *USAid* na baadaye vikaleta waandishi kutoka *South Carolina University*.
Mhe. Mwenyekiti, hoja hii hata Bara wamejitokeza kwa sababu unasema kama hivi na Bara kumefumuliwa madudu mengi katika mradi kama huo ambao amezungumza. Kwa kweli na mimi wala sitaki kuchukua mfano mmoja kwa jumla hiyo mifano tuliyoitaja kuanzia sera, mitaala, mihutasari, maslahi ya walimu, vitendea kazi na mambo mengine mengi pamoja na hivi vitabu Mhe. Mwenyekiti yanahitaji kutizamwa upya.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, mbali ya ule mkutano ambao ameahidi kutufanyia. Je, serikali katika hili anisaidie ina mpango gani wa kufanya upya mapitio ya Sera ya Elimu kwa ujumla wake na mfumo wetu wa elimu, ili kutizama haya maneno tunayokumbana nayo sasa pamoja na kuongeza bajeti kila mwaka mpaka mwaka huu yamefikia ni maradufu kuliko yaliyokuwa ni mwaka 2010. Kwa nini bado matokeo ya mitihani ni mabaya? Kwa nini kiwango cha elimu kinaendelea kushuka katika Zanzibar? Mhe. Mwenyekiti, naomba iniambie serikali imejipanga vipi katika kulikabili suala hili? Naomba kupata jawabu hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba mchango wa Mhe. Ismail Jussa Ladhu tumeupokea kwa makini sana, na ulikuwa ni mchango mzuri sana, na kweli alizungumzia habari ya mitaala, vitabu na kadhalika.

Sasa ninachotaka kuzungumza ni kwamba katika hilo kongamano ambayo tumekusudia kulifanya la kitaifa, basi tutayapitia yote haya na tutaiangalia tena sera, kwa sababu sera tumeiandika tokea mwaka 2006 na pengine imeshapitwa na wakati. Kwa hivyo, sisi wenyewe tukiendelea kusoma au kusomesha na kuendeleza wizara hii, basi tunakuta baadhi ya maeneo ya ile sera yana matatizo kutekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa inavyozungumzwa kwamba kuna haja ya kuipitia sera. Vile vile na mimi nilisema kwamba ule muda ulionipa ni mdogo, lakini nilisema kama ningekuwa na muda wa kutosha basi ningejadili au ningetoa ufafanuzi wa hizi hoja tuache zile za maandishi, lakini alizozitoa Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Suala la vitabu Mhe. Mwenyekiti, vitabu vya sekondari tunavyo vya kutosha, isipokuwa vitabu vya *primary* bado tunao upungufu. Kwa hivyo, kuhusu marekebisho tutakuja kuzungumza pamoja katika hilo kongamano. Pia katika ziara yangu ya hivi karibuni Japan nilizungumza na *Chairman* wa *JICA*

kumuomba suala la kuchapishiwa vitabu vya *primary schools*, ambapo huko ndiko kwenye kasoro.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba hoja ya Mhe. Mjumbe nimeiona na nimeipokea, tena ni muhimu sana mitaala, vitabu, sera na wakati mzuri wa kuja kuizungumza na kuitafutia marekebisho basi ni ule wakati wa kongamano tu tutakapokuja kulifanya.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ili kufupisha mjadala huu kwanza katika hili la vitabu ningetoa ushauri na tabu hii litaendelea tu mpaka tutakapofika hatua ya kufanya mapitio, kwamba wizara na uongozi wake ijiangalie sana Taasisi ya Elimu, kwa sababu wenzao wenye kitengo kama hichi wa upande wa Tanganyika yamegundulikana matatizo makubwa sana, kwamba waandishi wa vitabu walikuwa ndio wao wahariri, wapitiaji na matokeo yake vitabu hivyo tunavyoambiwa vimeandikwa na waandishi mpaka kutoka *South Carolina University* vimekutikana na matatizo mengi.

Lakini mbali ya ushauri huo na mwakani tutakuja kulihoji tena Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka hili la kongamano, kwa sababu tumejielekeza huko, na kama nilivyosema kwamba mimi nilitaka kuleta hoja binafsi hapa kikao kilichopita. Kwa hiyo, baada ya ahadi ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali baada ya kusema kwamba atafanya kongamano ambalo litatushirikisha sisi, basi nikasema haina haja ya kupoteza muda kwa ajili ya kuleta hoja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba anisaidie mambo mawili tu Mhe. Waziri, ili niruhusu tuendelee katika suala la sera ambalo litajumuisha mambo yote hayo mihutasari, mitaala, maslahi ya walimu, nidhamu maskulini, vifaa au vitendea kazi, mazingira ya elimu, muelekeo wa kiuchumi pamoja na dira yetu ya kiuchumi kiasi gani inasaidiwa na mfumo wetu wa elimu, yaani vitu vyote hivyo nataka anisaidie mambo mawili.

Moja kwamba hilo kongamano amelipanga kulifanya lini, kwa sababu kila tukiendelea kusubiri Mhe. Mwenyekiti huko nje vijana wetu wanateketea na tunaangamiza mustakbali wa taifa letu, kwa sababu mambo ya elimu yakivurugika leo athari inakuja kuonekana miaka mingi inayokuja, kwa hiyo anisaidie kwamba hili kongamano amelipanga lini?

Pili anisaidie kunihakikishia hapa kwamba je, Wawakilishi wa Wananchi katika chombo hichi watakuwa ni sehemu ya kongamano hilo, basi anisaidie hayo mambo mawili tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi huko nyuma nilikotoka nilikuwa Mwakilishi tena *backbencher*. Sasa umuhimu wa Wawakilishi kushirikishwa katika mambo yetu haya ya kitaalamu ni muhimu sana. Kwa hivyo, katika haya mambo mawili ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu ametaka niyajibu. *(Makofi)*

Kwanza basi aniachie tumalize mfungo wa mwezi Ramadhani na tule Sikukuu pamoja na tufunge 6 na baada ya hapo tutakuwa tumetulia tutatoa taarifa lini tunafanya kongamano, na wala sio zaidi ya wiki moja baada ya kipindi hichi. *(Makofi)*

Pili kuhusu kushirikishwa Wawakilishi *as many as possible* hata kama ni wote ni muhimu sana kuwashirikisha Wawakilishi, ili watupe michango yao *on the spot* kama ni kubadilisha sera au mitaala wazungumze, kwa sababu wao ni Wawakilishi wa Wananchi na hii elimu iko kwa ajili ya wananchi kwa nini tusiwaalike, basi tutawaalika. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na nachukua ahadi yake baada ya 6 *inshaallah* nampa na wiki moja aliyoiomba. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti 2,170,000,000/=
Kifungu 0701

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kweli namshukuru sana swahibu wangu Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwanza kwa utulivu wake mwaka huu, na kama alivyosema mwenyewe kwamba wizara anaiweza na kweli anaiweza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi wa hawa walimu wa Elimu Mjumuisho. Kwanza ninamshukuru sana kwamba kile kilio chetu au cha wananchi kupitia kwetu cha ile posho ya shilingi 5,000/= kweli hata yeye Mhe. Waziri pamoja na uongozi wake wameiona ndogo na wameongeza mpaka shilingi 30,000/= tunaishukuru sana wizara na kila mtakapopata nguvu tunaomba muwaongezee.

Lakini suala langu zaidi lilikuwa tokea ilipotamka au ilipotamkwa kwamba fedha au posho hii itaongezwa kuna wengine hawakuwahi kulipwa hata hiyo shilingi 5,000/=, na ndio maana wakauliza tumeambiwa tutaongezwa kutoka shilingi 5,000/= na hiyo shilingi 5,000/= yenyewe hatukuipata, je hicho kinachoongezwa tutakipata.

Sasa naomba kupata ufafanuzi kama walianza kupata baadhi yao hiyo posho ya shilingi 5,000/=, basi wako baadhi ya walimu hawajaipata hiyo posho yao na kama watakuwa hawajaipata posho yao labda Mhe. Waziri ataweza kunisaidia vipi maelezo kwa niaba ya hao walionileta hiyo hoja yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ni kweli Mhe. Hamza Hassan Juma aliliuliza hilo na nimwambie kwamba tayari tumewaandikia wenzetu Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na yale maposho ya Walimu Wakuu, ambapo ya walimu wakuu tayari yameletwa na haya ya madeni ya walimu hawa yanafanyiwa utaratibu nayo yatalipwa si kipindi kirefu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa ukarimu wa Wizara hii hasa wa Mhe. Waziri makini sana Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwa kuwajali walimu wake. Ahsante sana, tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri kwa majibu ambayo wameyatoa, na kwa kweli nilikuwa sina nia ya kutoa hoja kwa sababu Mhe. Waziri namuamini ni mtu mchapa kazi, tena ni msikivu na ni muungwana, pia ni rafiki yangu mpenzi na mimi nimepunguza kutoa mabuti 12 mpaka 2. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kubwa nataka nimkumbushe tu kama ni binadamu, ili tuweze kusaidiana. Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ya Utumishi nakwenda kwenye fungu 221102 mafunzo ya ndani imetoka milioni 28 hadi milioni 73.3 ni ongezeko la asilimia karibu 268. Sasa naomba nijue tu kwa kada ya udereva ambayo ni mafunzo ya ndani mwaka jana wangapi wamepata mafunzo, ili tuweze kuidhinisha fedha hizi kwa ajili ya mwaka mpya, naomba nijue hilo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Hija Hassan Hija arejee tena swali lake taratibu na kile kifungu chenyewe alichokitaja, ili tukifahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, rejea tena swali lako na halafu utaje kifungu pamoja na maelezo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kifungu chenyewe ni 221102

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ukurasa gani?

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 215 buku kubwa la pili kifungu 221102 kuhusu mafunzo ya ndani (*local training*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sawa sawa.
Mhe. Hija Hassan Hija: Kifungu 221102 mafunzo ya ndani, *local training*, fungu hili limetoka milioni 28 mwaka jana hadi milioni 75.3 mafunzo ya ndani. Sasa mimi ninavyotaka kujua tu kwa upande wa kada ya madereva akiwemo dereva wa Mhe. Waziri na wengine, madereva wetu hawa wa serikali wanapata tabu sana kama hatukuwapa matunzo na kuwasaidia. In *case* tukiwadharau wanaweza wakasababisha uzembe na kusababisha matatizo kwa Mhe. Waziri na watendaji wake pamoja na Wakurugenzi.

Mimi naomba kwamba mafunzo ambayo yametolewa kwa madereva ni wangapi kwa mwaka uliopita ili mara hii tuidhinishe milioni 75 na inijengee imani kwamba tayari mafunzo haya yanatolewa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hichi cha mafunzo ya ndani kuhusu suala la madereva, hatukupanga mafunzo ya madereva. Kwa sababu Idara ya Utumishi walitutolea matoleo katika Wizara zote kutwambia kwamba mafunzo haya sasa wanayatayarisha wao kutumia Chuo chetu cha Utumishi. Kwa hivyo sisi tukawa hatukupanga fungu lolote kwa ajili ya madereva wetu mpaka hapo ambapo watatuletea na kutwambia kwamba watakwenda katika chuo gani kujifunza, kwa mwaka jana na mwaka huu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kuanzisha mjadala lakini sikumfahamu vyema Mhe. Waziri, unajua Ramadhani ina matatizo yake, Naomba kwa hisani yake aendelee kunijibu sikumfahamu vyema.

Mhe. Mwenyekiti: Anakwambia mwaka jana kifungu hiki hawakutumia kwa madereva, kwa sababu walipata toleo kutoka utumishi kwamba watawashughulikia wao kupitia Chuo chetu cha Utumishi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, labda nisome kifungu 221100 gharama za mafunzo ya TSh 75,000,000 (sabini na tano milioni) haya ni maelezo ya Mhe. Waziri ambayo kuwa ameyatoa majibu. Yanasema kuwa kutoa mafunzo, kuwalipia ada na nauli wafanyakazi wanane wa kada ya chini katika Chuo cha Utumishi na madereva wanne kwenda Chuo cha Usafirishaji Dar-es-Salaam. Sasa huu ndio mpango mpya, mimi taarifa nilizonazo Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba madereva akiwemo na dereva wa Mhe. Waziri, mwaka jana wamekataliwa.

Sasa nilikuwa nataka sababu za kukataliwa ndio ninazoziomba, ili na mimi nijenge imani kwamba hawatokataliwa tena kwa fedha hizi. Mimi naomba Mhe. Waziri anipe sababu kwa nini mwaka jana waliwakataa? Ni tatizo la

fedha au kuna tatizo jengine ili mara hii nijenge imani kwamba hawa madereva hawatokataliwa ili tuweze kuwaendesha vizuri Wakurugenzi wetu na Mhe. Waziri atuendeshe vizuri. Kuwadharau madereva Mhe. Mwenyekiti ni kusababisha matatizo katika sekta hii ya usafirishaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, jibu nililojibu ni kama ambavyo nimejibu. Hizi pesa ni kama nilivyosema zilikuwepo lakini hazikutumika kwa kazi hii. Kwa sababu tuliletewa waraka maalum ambapo ulitutaka wafanyakazi wetu, tulikuwa tukipeleka. Ukitizama nyumba kote kuna wafanyakazi tumewapeleka watatu, wanne, lakini kwa mwaka jana hatukupeleka. Sababu ya kuwa hatukupeleka ni hizo kuwa Utumishi walituletea waraka maalum ambao ulitutaka kuwa madereva wetu badala ya kwenda Bara watapata mafunzo hapa hapa na watatwambia ni Chuo gani ambacho watashirikiana nacho ili kupatiwa mafunzo.

Kwa hivyo tunalisubiri hilo na tutawahimiza wenzetu Utumishi ili watuletee ni Chuo gani madereva wetu waende ili wakapate ujuzi. Mheshimiwa tunalitaka hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Naibu Waziri, niseme tu kwamba mimi Wizara naiamini sana kwa sababu inayoongozwa na walimu ni wizara moja muhimu sana. Pia namuamini zaidi Mkurugenzi wa Idara hii mwalimu wangu Vuai, niombe tu kwamba madereva ni watu muhimu sana katika kulinda maisha ya viongozi wetu. Wizara hii ina Wakurugenzi wengi, ina Naibu Katibu Mkuu, ina Katibu Mkuu na Waziri. Niiombe tu Wizara kwa hisani yako kupitia Mkurugenzi wa Utumishi mwalimu wangu Vuai, madereva wawape kipaumbele, vyenginevyo madereva tukiwaacha na shida, njaa na ujuzi mdogo, basi ni hatari kwa viongozi wetu. Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi na mimi niulize kidogo kwa sababu nilichangia kwa maandishi, lakini mchango wangu haukupata majibu kutoka kwa Mhe. Waziri. Sasa nimuombe Mhe. Waziri anijibu, maana nilikuwa nimeagiza katika mchango wangu kwamba nitazuia mshahara wa Mhe. Waziri kama sikupata majibu yake. Sasa nilikuwa naomba nipate yale majibu niweze kumuachia.

Mhe. Mwenyekiti: Kikanuni huwezi kuzuia kwa sababu mchango wako wa maandishi, upewe jibu halafu usikilize, kwa hivyo unapewa jibu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kidogo ningeomba hiyo kanuni, kwa sababu na mimi kanuni ninayo ninaiangalia, hakuna kanuni

ambayo inanizuia kwenye mchango wa maandishi nisizuie kwa sababu katika kanuni hiyo ambayo unaizuia Mhe. Mwenyekiti, nafikiria ni kanuni ya 96(4).

Mhe. Mwenyekiti: Ngoja Mhe. Mwenyekiti, juzi ulijibiwa vizuri na Mhe. Spika, hapa na kila Mjumbe kasikia, tena tusianzishe hoja mpya. Subiri jibu lako umeridhika, hukuridhika utatwambia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru...

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako katika majibu ambayo Mhe. Naibu Waziri anaanza kuyatoa. Suala langu mimi liko kwa Mhe. Waziri na huo mshahara ninaouzuia ni wa Mhe. Waziri.

Kwenye Kanuni za Baraza hapa kifungu cha 37 mimi nimeona ambaye anapaswa kujibu hapa imeandikwa kabisa Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa ana wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali alililouliza Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au na Mwanasheria Mkuu, hakutajwa Naibu Waziri.

Lakini vile vile ukiangalia kwenye Katiba kifungu cha 43(5) inaelekeza kwamba uwajibikaji wa pamoja ni *cabinet*, Naibu Waziri sio *cabinet*, sifikirii kama atakuwa na mamlaka ya kunijibu.

Mhe. Mwenyekiti: Atakujibu mwenyewe Waziri.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi sana kwa jibu nitakalolitoa kwa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa aniwie radhi. Mimi mwaka huu sikupokea hoja yake ya maandishi. Nilichokipokea ni barua ya kitisho. Mhe. Mtando ameandika barua ya kitisho, kwamba kwa sababu mwaka jana sikumjibu majibu yake atazuia mshahara wangu. Barua haina *heading* kwamba ni mchango wake alinileta barua ya kitisho, hilo moja.

Lakini la pili mwaka jana alinileta mchango wake tumeshafunga mjadala dakika ya mwisho kabisa, akanambia ameniuliza maswali 17, mimi sikuyaona maswali 17. Lakini niliipitia *hansard*, nilipoipitia jina la Mhe. Mtando halikuorodheshwa katika waliochangia kwa maandishi, nimepitia *hansard* maksudi.

Sisi Mawaziri tunapokuja kutoa maelezo katika hoja zilizozungumzwa na Wajumbe tunataja majina mmoja baada ya mwengine mpaka wale

waliochangia kwa maandishi ni huyu na huyu. Mtando hakuchangia kwa maandishi. Isitoshe Mhe. Mtando alimfuata Naibu Waziri wangu akamwambia nilichangia kwa maandishi maswali 17 hayakujibiwa naomba mnijibu kabla ya bajeti, vyenginevyo nitazuia kifungu. Tishio la pili hilo.

Naibu Waziri wangu akamwambia tusifikishane huko. Mimi niletee maana sisi tumetafuta hiyo nakla ya maswali yako hatukuiona, hebu niletee hiyo nakla yako, tutakujibu kabla ya bajeti. Mheshimiwa akatuahidi atatupa, matokeo yake hakutupa hiyo nakla. Alichotupa ni hii barua ya juzi kwamba atazuia mshahara wangu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki twende kwenye Kanuni, nataka siseme tu Mhe. Mtando kama anaweza kuzuia mshahara wangu na azuie mshahara wangu! Kama alivyozungumza juzi Mhe. Waziri wa Afya na mimi nazungumza hivyo hivyo. Wala sina jibu jengine zaidi ya hivi nilivyojibu. Kama anaweza kuzuia mshahara wangu na auzuie. Mimi Ramadhani hii nitakufa na njaa, nitakufa na watoto wangu, potelea mbali! (*Makofi*)

Lakini Mhe. Mtando ana tabia ya kuleta maswali yake dakika ya mwisho tumeshamaliza kila kitu. Na ndivyo alivyomfanyia Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban (Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati) juzi. Sasa Mheshimiwa kama nilivyosema zaidi ya hili sina jengine. Ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi. Lakini nataka nikwambie Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi Mhe. Waziri namuheshimu sana kabisa, nisingependa nifanye malumbano. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi vile vile nina nakla ya *hansard*, ambayo yeye anasema ameiangalia na mimi anasema sikuchangia kwa maandishi. Sasa *hansard* ninayo na naomba niinukuu. Katika *hansard* hapa kuna maneno yameelezwa hapa anasema Mhe. Waziri wa Elimu wakati anatoa majumuisho mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti: Kwanza Mheshimiwa kwamba alikuomba hayo maelezo uwape, uliwapa?

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Kwanza Mhe. Mwenyekiti, kasema sina mchango ambao nimeutoa kwa maandishi mwaka jana. Kama ulimsikiliza vizuri, *hansard* imeweka kama ni kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio akaomba uwape.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Halafu anasema anaomba nimpe. Sasa nimpe mchango upi kama mimi sina mchango. Sasa mimi nataka kukumbusha tu

kwamba mchango ninao na nilipeleka kwa maswali kabisa. Lakini yeye mwenyewe alisema kwamba nimeyapeleka asubuhi kwa siku ile kwa hivyo atayajibu kwa maandishi. Kwa hivyo yeye ndiye aliyekuwa anawajibika kuyajibu kwa maandishi, maana hiyo ndiyo kazi yake eti.

Ukiangalia kwenye Katiba kifungu cha 88 kazi za Baraza la Wawakilishi kiangalie. Kitakwambia moja katika kazi yetu sisi ni kuihoji serikali, kuiuliza maswali na wao serikali wanapaswa wajibu. Sasa kama yeye hakujibu mimi sina wajibu wa kwenda kumtafuta nikampelekea maswali yangu wakati nimeshamletea hapa. Yeye anapaswa hapa hapa anijibu na yeye alisema kwamba atayajibu kwa maandishi. Naomba niinukuu hii *hansard* kwanza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Haya nukuu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Anasema hivi:-

"Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu nawashukuruni nyote, nasema ile michango niliyoipata leo asubuhi ambayo ilituuliza mengi ya kitakwimu naomba radhi Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) kama alivyosema kuwa kama sitompa majibu hatoipitisha bajeti. Namuomba sana aipitishe bajeti yangu na mimi naahidi majibu nitayaleta hapa Barazani kwa Mhe. Spika, ili sio yeye tu lakini na wengine wote wapate kuyaona na wapate kuridhika.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja."

Haya maneno anayasema Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, hii ni *hansard* Mhe. Mwenyekiti. Sasa Waziri anaposema kwamba mimi sikuchangia kwa maandishi nasikitika sana kabisa. Na anaposema kwamba leo hii nimempelekea barua ya kitisho kama yeye anaogopa hayo, hayo ndiyo mambo ya Baraza, hatuwezi kumuidhinishia fedha ambapo ule uwajibikaji wenyewe haupo. Yeye alipaswa ajibu haya ambayo sisi tunawauliza hapa.

Mhe. Mwenyekiti, anaposema barua ya kitisho mimi sikumpelekea nyumbani. Mimi nimetoa huo ndio mchango wangu kwamba mchango wangu labda niusome. Naomba niusome Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Utachukua muda.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Kwa hiyo tufanyeje?

Mhe. Mwenyekiti: Hebu Mheshimiwa kaa kidogo tuzungumze, kaa tutoe maarifa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mimi nafikiria Mhe. Mwenyekiti, niusome ili tupate kuweka kumbukumbu vizuri kwenye *hansard*.

Mhe. Mwenyekiti: Muda utakuwa mrefu. Mimi nadhani mkubaliane. Mhe. Waziri achukue huo mchango halafu utafanyiwa kazi na Wizara, hilo ndio wazo langu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, huo mchango nimeshampa yeye anaouita barua ya kitisho, na ndio maana hapo katika kutaja pia leo hakunitaja kwamba ni Wajumbe waliochangia kwa maandishi mpaka kakumbushwa na Mhe. Naibu Waziri hapa. Hata hiyo mwaka jana ukiangalia katika *hansard* vile vile hunioni katika waliochangia kwa maandishi hakunitaja. Lakini mwisho ndio akaeleza hili, nikaona mimi hakuna haja ya kuomba muongozo wa Spika, kwa sababu ameshanitaja kwamba nimechangia. Ndio maana leo kumbe yeye alikuwa amefanya vile kwa mtego kwa maana hiyo kwamba hanitaji kama nimechangia kwa maandishi ili asijibu zile hoja ambazo tutakuwa tunazileta.

Lakini bahati nzuri inaonekana hii *hansard* hakuisoma vizuri, mimi nimeiona na ndio maana nimekuja nayo kama ni ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba yale majibu yangu na nilimwambia katika mchango kwenye hii barua ambayo yeye anaiita ya kitisho mimi naita mchango wangu. Nilisema sioni haja ya kuchangia leo kama yale maswali ambayo nimeyauliza mwaka jana hayakujibiwa kwa mwaka mzima. Sasa kama mwaka mzima serikali imechukua maswali yetu haikujibu, leo mimi nauliza mengine ya kitu gani? Kwa hivyo nikawa namuomba nijibiwe kwanza yale ya mwaka jana basi pengine *Inshallah* mwakani nitakuja kuchangia vizuri zaidi. Sasa Mhe. Waziri anaposema barua ya vitisho, sijui kitu gani, hatwendi huko.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Waziri wa Elimu asiwe na jazba, hapa tunakwenda kwa kanuni na sheria. Ikiwa mchangiaji ni mtu mdogo yeye kama ni *senior* mchangiaji ni *junior* sawa, lakini humu sote ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tuna haki sawa. Nikiuliza mimi, akiuliza mwengine ni sawa tu. *(Makofi)*

Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anijibu na kama kuzuia fungu Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaendelea kulizuia kwa sababu ninaposema kuzuia mshahara wa Waziri maana yake nalizuia fungu lenye

mshahara wake. Sio kwamba nitazuia mshahara ule wa kwake yeye tu, nitalizuia fungu lote la 0701 mpaka nipate maelezo ya ziada.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Nimeamua nitumie Kanuni ya 58 kifungu kidogo (8) (b) na (c) lakini kabla sijakinukuu kifungu hichi Mhe. Mwenyekiti, naomba kwamba Baraza lako lielewe kwamba tupo katika jambo kubwa sana, jambo la kutaka kupitisha bajeti ya Wizara nyeti sana Wizara ya Elimu. Kwa hivyo nimelazimika kutumia kifugu hichi nanukuu kama kifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu gani.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ibara ya 58 Kifungu kidogo cha 8 (b) inapatikana ukurasa wa 54 na (c) kwenye Kanuni.

"Ni marufuku...

Mhe. Mwenyekiti: Unatumia kanuni gani mbona huku kwetu sisi hakuna hiyo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba niulize tu, Kifungu hicho cha 58 kinatoka wapi? Kifungu hicho cha 58 Katika Kanuni za Baraza hakipo, hicho anachokisema yeye, sasa atwambie ni kifungu gani?

Mhe. Mwenyekiti: Anatumia kanuni ya zamani. Kwenye kanuni zetu hakimo hicho unaitumia ya zamani hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri na vile vile maelezo aliyoyatoa ndugu yangu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa. Sisi sote tuliokuwemo humu ni binaadamu na wakati mwengine binaadamu hughafilika na wakati mwengine hujitokeza kwa nia njema kurekebisha kasoro zinaweza kujitokeza.

Mimi nimuombe tu Mhe. Mtando akubali tupokee mchango wake huu ambao ameuleta, na kwa mujibu wa *hansard* tayari ameuwasilisha, tuuchukue kama serikali, ufanyiwe kazi na naamini majibu yote yatatolewa vizuri kwa kuletewa kwa maandishi katika siku zinazokuja. Namuomba sana akubali kupokea ili tuweze kuendelea na bajeti yetu hii.

Hasa tukiangalia Mwezi wetu huu mtukufu wa Ramadhani ili tumalize shughuli zetu mapema tuweze kufanya mambo mengi ya ibada katika mwezi

huu. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Mtando akubaliane nasi, apokee majibu haya ya serikali, kwamba tunapokea yale yote yaliyowasilishwa na tukayafanyie kazi na majibu yatakuja rasmi katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, labda tuweke kumbukumbu vizuri pamoja na kauli ya serikali iliyotolewa. Kwanza nieleze basi yale ambayo nimeyawasilisha mwaka jana yale maswali yangu majibu yake yatapatikana, serikali iji- *commit* iniambie kama itajibu au laa? Kwa sababu alichokubali kwamba nimemfahamu vizuri Mnadhimu wa Serikali pale ni kwamba anakubali sasa kuupokea mchango wangu huu niliouwasilisha jana ambalo Waziri anasema yeye hakuupata wakati mimi nilimkabidhi Mhe. Naibu Waziri wa Elimu hapa wakati yeye alikuwa hajafika.

Kwa hivyo kwanza nipate kauli ya serikali kwamba majibu yangu yale ya mwaka jana nitayapata?

Mhe. Mwenyekiti: Ya mwaka huu umeshakubali?

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ya mwaka huu ndiyo anayachukua ameshasema, kwa mujibu wa kauli yake Mnadhimu wa Serikali. Sasa mimi katika hoja yangu nilikuwa nakumbushia yale ya mwaka jana je, nitapata majibu yake na kama nitayapata ni lini?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana kwako na kwa Mhe. Mbarouk Madi Mussa (Mtando) yeye anasema ananiheshimu sana, na mimi namuheshimu sana. Maneno ya Mhe. Haji Omar Kheri yeye ni Mtumbatu wa Juu mimi ni Mtumbatu wa Kisiwani lakini sote ni Watumbatu, kwa hivyo ni lazima tuheshimiane na mimi namuheshimu kweli kweli.

Nataka niseme hivi alimwambia Naibu Waziri wangu kwamba asipopata majibu kabla ya siku ya bajeti yangu atazuia kifungu. Naibu Waziri wangu akamwambia kufupisha suala hili nimeshazungumza na Waziri *with in three days* na hiyo ni kabla ya kupitisha hiyo bajeti, nipatie *copy* ya hayo masuala tutayajibu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) kwa uungwana wake alisema nitakupa kesho au nitakupatia kesho, keshokutwa, mtondogoo, hakuipata. Sasa Mheshimiwa anasema anayo pale mkononi anataka mimi niyajibu ya mwaka jana na nimpe siku gani nitamkabidhi majibu yake. Anipe hayo maswali, anayo yeye na anipe basi kama alivyoahidi maswali anayo yeye anipe.

Mimi namuahidi Jumanne nitamkabidhi mkononi majibu ya maswali yake. Kama kanuni zinaturuhusu maswali ya mwaka jana tuyajibu mwaka huu hakuna matatizo. Anipe nitayajibu Jumanne nitamkabidhi. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mtando, umkabidhi hayo maswali na Jumanne utapata majibu ya mwaka jana, ya mwaka huu serikali imeshaahidi itajibu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hapa tunakwenda kwa mujibu wa sheria na kanuni, mwaka jana niliwasilisha mchango wangu kwake...

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tusirudie keshasema umpe maswali yako ya mwaka jana atajibu na siku ya Jumanne atakuletea majibu. Tunarudia kule kule tena. Si unayo hapo waletee Jumanne watakujibu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Heeh!

Mhe. Mwenyekiti: Au huna?

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Heeh! Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi unipe nafasi basi, maana yake ikiwa hivyo Waziri kasema sasa Kiti kinaonekana kipo upande wa Waziri sasa, badala ya kwamba Kiti kikae kati kati.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nahoji, wewe umesema hakujibu, keshakubali kukujibu mpe.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Sasa naomba na mimi niseme basi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Haya sema.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti mimi niliwasilisha mchango wangu kwake Mhe. Waziri, huo mchango kauweka wapi, kautupa? Na hayo maswali mimi niliyaleta kwake. Mimi siwezi kumpa mengine, kwa sababu niliyawasilisha katika chombo husika, siwezi kwenda kumpa nyumbani. Maswali yangu yeye anayo, mchango wangu anao, si wanahifadhi, wanaweka kumbukumbu.

Kwa hivyo yeye anachosema kanidai maswali yangu nimpe, si kweli. Hatujawahi kukaa mimi na yeye tukazungumza hicho kitu. Na hicho kitu mimi nilikiwasilisha hapa na *hansard* hii hapa na yeye ndiye aliyekiri kwamba nimempa hicho kitu.

Kwa hivyo mimi naomba majibu yangu na ndio maana nilikuwa nauliza, tena nilikuwa sitaki kusema, yeye kashindwa huyu kufanya kazi mwaka mzima. Kule Mnadhimu wa Serikali alikuwa anachukua ahadi. Anachukua ahadi vipi yeye, achukue ahadi Mnadhimu wa Serikali sasa kwamba wao ndio watanijibu maana yeye ameshakaa nayo mwaka mzima hakuweza kutoa jawabu. Mimi niendelee kusikiliza, sasa nimpelekee mimi tena, nimpelekee kwa mara nyengine. Leo tupo mwaka mwengine huu, siwezi kumpa tena Mhe. Mwenyekiti, kama yeye alishindwa kutoa majibu kwa wakati ule.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa tumesikia, kwa hiyo tunaendelea.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Tunaomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hii hali inayoendelea.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja tumeshaimaliza tunaendelea.

Kifungu 0701	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	38,215,000,000
Kifungu 0702		

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa fursa hii. Nilipokuwa nikichangia niliulizia walimu wa TC niliulizia kwamba vile vyeti vyao vinatambulika kimaslahi au ndio wameongeza elimu tu ndio basi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, Tunakushukuru ni kweli Mhe. Asha alipokuwa akichangia alilizungumzia hili. Walimu wa TC ni walimu wetu ambao tumewapandisha ngazi tu kuwasaidia kama somo la hesabau na English. Walimu hawa walitambulika kama vile sifa zao walizokuwa wanazo, tumewapa masomo ya ziada tu ili wawe na uwezo mzuri wa kusomesha kwa yale masomo yaliyokuwa yana matatizo kwao.

Mhe. Asha Abdu Haji: Tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kuweza kumsaidia sana Mhe. Waziri na ndio inavyotakiwa akina mama wawe walezi hasa kutusaidia kazi. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kama nilivyosema kutokana na ufafanuzi uliotolewa lakini nilikuwa nataka tu ufafanuzi wa ziada kwa wale walimu ambao waliopewa kazi maalum kwa ule mradi wa TAP wa kufundisha walimu wa Sayansi, ili kuweza kuongeza uwezo wa walimu wa sayansi na

kuweza kusomesha. Wamelalamika mwaka jana nilizungumza hapa kwamba yale maslahi yao hayajazingatiwa.

Mhe. Waziri mwaka jana aliniahidi kwamba watayaangalia na wataweza kuyaboresha au kuwalipa maslahi yao. Kwa kuwa Mhe. Waziri anatikisa kichwa inaonesha kwamba hili suala analielewa vizuri naamini ataweza kunijibu vizuri ili na wao wale walimu waweze kuridhika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti ninamshukuru sana Mhe. Hamza kwa suala lake la hawa walimu wa TAP, Mhe. Mwenyekiti kweli mwaka jana niliahidi hivyo na alhamdullillahi ahadi nimeitekeleza. Tarehe 24/9/2012 tumepeleka barua Wizara ya Utumishi kuomba tupatiwe maposho yao hawa walimu wa TAP na tulifikia tutawapa *increment* mbili kwa ile kazi nzuri waliyoifanya na kuonesha tumewathamini sana. Kwa sababu hawa walimu tunawahitajia ni walimu wa sayansi tunawahitajia sana, na ninayo orodha hapa ningeomba baadae nimkabidhi Mhe. Hamza ili mimi na yeye sasa tusaidiane kuihimiza Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo ili hizi pesa tuzipate kuwalipa hawa jamaa, nina hakika pesa hizi tutazipata mwaka huu na zimo katika makisio katika bajeti yetu.

Kwa hivyo tukizipata tu na maadam ombi tumeshalipeleka muda mrefu tukizipata tu hizi pesa naomba hawa walimu wa TAP wajiweke tayari kukabidhiwa hizi pesa. Na *infact* kwa sababu tuna hakika ya kuzipata hizi pesa hivi sasa kuna maandalizi ya kupeleka *group* la pili la walimu wa aina hii kwenda kusomesha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti namuomba sana Mheshimiwa rafiki yangu sahibu wangu, mlezi wangu Mhe. Waziri wa Uchumi, Fedha na Mipango ya Maendeleo, Mhe. Mwenyekiti suala hili la haki ya walimu, leo Zanzibar tunalalamika sana kuhusu walimu wa sayansi. Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma alipokuwa akitoa ufafanuzi kumsaidia Mhe. Waziri majibu alieleza tuna *gap* na tuna nafasi za walimu wa sayansi ambao hivi sasa hatuna, leo walimu wetu hawa wameamua kujitolea kuwafundisha walimu wenzao ili kuweza kumudu masomo ya sayansi tumeipitisha bajeti ya Wizara ya Elimu tokea mwaka uliopita, Mhe. Waziri makini sana Waziri wa Uchumi, Fedha na Mipango ya Maendeleo yupo hapa na bajeti hii imo ndani ya OC za Wizara ya Elimu.

Mimi nadhani Waziri wa Fedha, kwa sababu unajua kusema tu Mhe. Waziri atanipa orodha tushirikiane na yeye hili suala bado liko chini ya Mhe. Waziri wa Uchumi na Fedha, hebu atusaidie basi alau tusikie kauli yake ili na hawa

walimu wetu waweze kuwa na moyo wa kuweza kuwasomesha walimu wengine. Naomba maelezo ya Mhe. Waziri wa Fedha. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, Mwenyekiti wangu wa wenyeviti mimi ninampenda sana masuala ya fedha yote ananitupia mimi na mimi ninayapokea. Mimi nataka niseme tu kwamba ni suala hoja yake na nia yake ni nzuri atuachie mimi na Waziri wa Utumishi na Waziri wa Elimu tutalitazama kwa pamoja na *inshaallah* litapata ufumbuzi, atuachie tuliangalie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti naamini kwa vichwa hivi vitatu vikikaa pamoja ninaamini hili suala litaweza kupatiwa ufumbuzi lakini na mimi Mjumbe hauwawi nitaendelea vile vile kufuatilia ili kuona hawa walimu wetu wanazidi kupata moyo wa kusomesha wenzao Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Kifungu 0702 Baraza la Elimu 60,000,000
Kifungu 0703

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti wakati nachangia nilizungumzia kuhusu huduma ya maktaba Pemba, ninampongeza sana Mhe. Waziri wa Elimu na Naibu Waziri kwa majibu yao mazuri, lakini Mhe. Mwenyekiti katika mchango wa Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi alisema kwanza mchango ule ni wa kisiasa, na vile vile tusitake jambo lililofanywa Zanzibar lifanywe na Pemba, na akatoa mfano mwengine aidha lililofanywa Mpendae lifanywe na Donge. Kwanza hapa Mhe. Mwenyekiti naomba Mhe. Naibu Waziri apewe elimu ya kutofautisha baina ya jimbo na jimbo na Kisiwa na Kisiwa.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti hawezi mwanafunzi kutoka Pemba akaja akachukua kitabu maktaba iliyopo Unguja, lakini mwanafunzi kutoka Mpendae anaweza kwenda kuchukua kitabu Donge na akakitumia. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti hapa naomba Mhe. Naibu Waziri apewe elimu na vile vile kuhusu hii Zanzibar, Mhe. Mwenyekiti mimi ninavyoelewa ukisema Zanzibar unakusudia Unguja na Pemba. Lakini leo katika majibu utasikia huwezi ukalinganisha jambo lililofanywa Zanzibar na Pemba sasa hapo kama mimi nasema ni jambo lililofanywa Unguja na Pemba au na Pemba.

Sasa hapo Pemba naona zimeshakuwa mbili na katika majumuisho ya Mhe. Waziri sikumsikia akitoa maelezo kuhusu hili, kama kutetea maendeleo ya wananchi ni kosa au ni wajibu. Kwa sababu mimi naona katika jambo moja ambalo linanilazimu ni kuwasemea wananchi na kuwatetea, na hili nililifanya

kwa ajili ya kuwatetea wananchi wa Pemba. Sasa hapa naomba nipate maelezo ya Waziri au ya Serikali kufanya hivi ni makosa?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti kwa ile *spirit* ya *collective leadership* nachukua jukumu la kumuomba radhi Mheshimiwa kwa hili tamko lililotamkwa na Naibu Waziri kwa makosa nachukua jukumu la kumuombea radhi Naibu Waziri wa Kilimo. Nasema jibu sahihi ni kwamba tumeshalizungumza tumesema pesa tunazo na maktaba tunajenga Pemba. Hayo yaliyozungumzwa kwa bahati mbaya naendelea tena kuomba radhi Mheshimiwa na chukua haya niliyoyasema mimi.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti kwa sababu tunatakiwa binadamu yoyote anapokutaka radhi umsamehe na Mwenyezi Mungu huwa ni rahisi kwake kukusamehe na wewe nasamehe, tuendelee.

Kifungu 0703 Shirika la Huduma za Maktaba 379,000,000
Kifungu 0801

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana na nilimwambia katika jitihada zetu za kumsaidia yeye kujenga yeye kujenga na pale anapomaliza katika hizi skuli zetu za msingi, hizi za sekondari, za maandalizi. Kwa hivyo ninamuomba Mheshimiwa kuna skuli yetu moja hakuniahidi kama atanimalizia, namuomba nimsikie japo sauti yake tu kidogo kunambia kuwa Mheshimiwa hizo jitihada zenu naomba nitakumalizia usiwe na wasiwasi nilitaka hivyo tu Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti tutammalizia skuli yake.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru sana na kama alivyoeleza hapo Mheshimiwa wangu Mwenyekiti wa Wenyeviti na mimi nitakuwa karibu naye kufuatilia ili tuweze kukamilisha suala hili. Naomba tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti hapa nilikuwa na ombi tu kidogo. Na ombi linaweza likakubaliwa au likakataliwa na kuomba si makosa, kuiba ndio matatizo. Kuna Skuli ya Michakaeni ya msingi Pemba, ina wagonjwa wa taahira na wanatia huruma na Mwenyezi Mungu kawajaalia neema moja kubwa sana ya kuweza kula chakula chenye nguvu, hapa nilikuwa naomba wakaifikiria hii skuli kuisaidia Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru Mhe. Jaku kweli alisema hilo na mimi nilimjibu bahati mbaya kama nilivyosema Mhe. Jaku alikuwa na shughuli nyengine hakunisikia. Skuli ile tunaisaidia na kama ambavyo alikwenda akaona kama kulikuwa na matatizo ya bati kuvuja, ile bati tayari tumeitengeneza na tuko katika hatua ya kutia rangi na kama yeye alivyoahidi wakati ule alipokwenda alipokuwa katika kamati ya kusema kuwa atatusaidia ile bati, lakini kwa bahati mbaya tukaona hali inavyozidi kuwa mbaya tukalichukua sisi Wizara lakini bado msaada wako tunauhitaji na tunauthamini sana kwa sababu tunataka kutia rangi pale. Kwa hivyo atusaidie Mheshimiwa na tutashirikiana naye katika suala hili asiwe na wasiwasi.

Mhde. Jaku Hashim Ayoub: Kwa masikitiko makubwa nilichozungumza ni Kiswahili tena cha hali ya chini kabisa nimesema kuna ombi unaweza kukubali au kukataliwa nimeomba ile skuli waiangalie kuhusu bajeti ya chakula, wale watoto Mwenyezi Mungu kawajaalia wana neema kubwa sana ya kula afikirie Wizara ya Elimu kulifikiria hilo, si suala la kuvuja wala kuezeka paa. Ni ombi wale watoto Mwenyezi Mungu kawajaalia wana neema ya kula, Wizara iwafikirie kuhusu chakula, wale watoto wanatia huruma Mhe. Mwenyekiti ilikuwa ni hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Watoto wepi wenye walemavu au wepi?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wenye akili ya taahira, si suala la kwa ndani au kutoka nje.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti tutalifikiria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Unajua Mhe. Mwenyekiti ombi kufikiriwa unaweza ukakubaliwa au kukataliwa lakini tuendelee Mwenyekiti.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti nilikuwa sitaki niseme lakini kutokana na vyuo vya *qur-an* hivi ndivyo ambavyo vinatusaidia kuanzia leo hapa duniani na mpaka kesho akhera. Katika mchango wangu niliokuwa nikichangia Mhe. Mwenyekiti nilisema bado kuna matatizo kwa upande wa walimu wa madrasa.

Moja kwanza upungufu wa majengo na ubovu wa madrasa pamoja na vifaa vya kufundishia na pia wakati mgumu wa kufundisha walimu hao kutokana na ufinyu wa maisha na hali zao duni inabidi walimu wale kuwakamua wazee wa watoto. Hili ningeomba Mhe. Waziri anipe muongozo na anisaidie je walimu hawa atawasaidia nini? Lakini vile vile nilisema kwamba katika

kitabu chake cha mwaka jana ukurasa wa 34, 59 walisema walishindwa kufanya ziara kwa vyuo na madrasa kutokana na upungufu wa fedha. Je, Mhe. Waziri mwaka huu 2013/2014 tayari fedha hizo zimeshapatikana na ziara hizo zitaanza lini. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti ni kweli Mhe. Mwanajuma alilizungumza hilo na mimi katika majibu yangu pia nilimjibu kuwa shughuli za madrasa haziko katika Wizara ya Elimu shughuli hizo ziko kwa Mhe. Abubakar Mufti. Lakini sisi kama Wizara ya Elimu kwa sababu inayotolewa pale ni taaluma sisi huwa tunawasaidia katika kusimamia ile taaluma inayotolewa iwe katika misingi ambayo ni mizuri. Lakini tutashirikiana na Mhe. Abubakar kuhakikisha suala hili tunaliweka sawa.

Kuhusu suala la posho Mheshimiwa hatuwezi kuahidi kwa sababu kama idadi ya vyuo ambavyo tumevitaja na madrasa ni nyingi sana isipokuwa ninachofahamu mimi wazee wao wenyewe huwa wanachangia ili kuwasaidia wale walimu wanaofanya kazi ile ya Mwenyezi Mungu kupata angalau sabuni na sisi kama Wizara huwa tunawasaidia tukipata vijuzuu, tukipata misahafu, tukipata tende pia tunawapelekea Mheshimiwa.

Kuhusu la pili ambalo alilizungumza Mheshimiwa mara hii tumeweka kifungu na nadhani kitatiwa pesa basi tutaendelea kufanya ziara zetu ili kuhakikisha kwa sababu kuna matatizo mengi kama ambavyo walichangia Waheshimiwa Wawakilishi ambayo yanafanyika kwenye madrasa ambayo yanakwenda kinyume na silka na utamaduni wetu kuhakikisha kama tunavipitia vyuo vile na madrasa zile ili kwenda katika hali nzuri Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti suali langu la pili hakunijibu kuhusu ziara lakini nataka nimwambie Mhe. Naibu Waziri anayejibu maswali. Kwa nini akabeba mzigo si wake kuutia katika kabrasha hili kwamba vyuo vya *qur-ani* vimo, kwa nini akabeba mzigo si wake asimwachie mwenyewe Mhe. Abubakar.

Mhe. Waziri wa Nchi Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti kama Mhe. Mjumbe atakumbuka wakati ya bajeti yangu nilisema hili na nilisema hivi sasa kuna vyuo karibu 2000 Unguja na Pemba na tumeshaanza kuvitembelea moja baada ya kimoja, hatujafika vyote 2000 na lengo la vyuo hivi kwanza ni kujaribu kutizama kutokana na yale matatizo ambayo maustadh wetu wanayo na kujaribu kuviandikisha upya ili angalau ile misaada ambayo tunapata tuweze kusaidia. Lakini vyuo 2000 ambavyo ukitizama vinaweza vikawa na walimu karibu 4000 au zaidi kwa sababu chuo kimoja kinaweza kikawa na

walimu watatu au wanne, chuo chengine mpaka walimu 10. Kwa hivyo walimu ni wengi sana ambapo serikali haiwezi kuwapa posho, lakini tunafanya mipango na tuna wakati mwengine tunawasaidia pale ambapo tunapata misaada. Kwa hivyo tutaendelea kufanya hivyo kama nilivyosema katika bajeti yangu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti nasema bado Mhe. Waziri hajanijibu suali langu la ziara za Pemba au ziara za madrasa. Hili sijalipata lakini na vile vile nimuombe Mhe. Waziri wasibebe mizigo iliyokuwa si yao katika shughuli zetu hizi kila mmoja amwachie mzigo wake au abebe mwenyewe apate lawama zake. Ahsante.

Kifungu 0801	Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi	237,945,000
Kifungu 1201	Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala	252,000,000
Kifungu 1402	Chuo cha Kiislam Pemba	31,000,000
Kifungu 1403	Chuo cha Kiislam Unguja	57,000,000
Kifungu 1404	Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia	1,366,000,000
Kifungu 1405	Chuo cha Ualimu Bejamin Mkapa	31,000,000
Kifungu 1406	Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar	4,900,000,000
Kifungu 1407		

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti nilipochangia hoja hii niliulizia juu ya kadhia ambayo mwaka jana tulizungumza Baraza hili kwamba Ofisi ya Mamlaka na Mafunzo ya Amali kuna wafanyakazi wenye ajira zaidi ya moja. Sasa naomba nipate maelezo ilifikia hatua gani.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti ni kweli Mhe. Hija aliichangia hoja hiyo na tumewasiliana na Utumishi na tunaliangalia suala hili la kuchukua mishahara miwili na kuna fununu lakini hatujapata uthibitisho. Kwa hivyo nataka nimhakikishie Mhe. Hija kwamba hatukulidharau tunaliendeleza na tunalifanyia utafiti na uchunguzi na nadhani niahidi tukilimaliza tutaleta taarifa Barazani.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti mimi ninasikitika kidogo kwa nia safi kabisa, kwa sababu sina haja ya kumbana Mhe. Waziri, hoja hii ilizungumzwa mwaka jana na mimi mwenyewe nimezishuhudia barua ambazo wahusika wenyewe wamekiri kwamba wana mishahara miwili. Mhe. Waziri akisema anachunguza mimi ninasikitika sana. Mimi nilikuwa Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, tulizungumza na Mkurugenzi na wahusika wakakiri wana mishahara miwili. Sasa mwaka jana mpaka hii leo bado anachunguza wakati wenyewe wamekiri kwa barua kwamba kweli tuna

ajira sehemu mbili bado mnachunguza jamani mpaka lini mambo haya? Mwenyekiti mambo haya mpaka lini kuchunguza wakati wenyewe wamekiri kwamba wana ajira mbili ni jambo la kuamua tu.

Sisi tulishauri Kamati kwamba waaamue kuacha moja waendelee na moja. Lakini ikiwa wanachunguza jamani mpaka lini Mhe. Waziri anambie. Kama barua hajapewa mimi nitamletea barua ambayo wamekiri kwamba wana ajira mbili. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti narejea tena kusema ni kweli suala la uchunguzi wa aina hii pamoja na kupata hizo barua ambazo anazizungumza ni kweli inachukua muda na nataka nithibitishe. Kwanza nataka nikubali kwamba ni kweli nimechukua muda mrefu si kwa sababu tumelidharau wala sio kwa sababu tunamwachia huyo aliyechukua mishahara miwili tu au aendelee au tusimchukulie hatua hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za mwanzo tulizozichukua tulipotaka kufanya *investigation* ya aina hii kwanza ni kumsimamisha kazi yule mkosa au yule mtuhumiwa ili upate muda mzuri wa kupitia mabuku, kupitia vocha, kupitia vitabu kupitia kila kitu hawa tumewasimamisha kazi na ndio maana sasa tuna wakati mzuri sana wa kuchunguza hili suala. Nataka nimuahidi Mhe. Hija siwezi kuthibitisha lini lakini nataka nimuahidi si muda mrefu utakaokuja hili suala tutalimaliza. Nataka nimuahidi hivyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti bado nasema kwamba mimi Mhe. Waziri ninamfahamu kama ni mtu jasiri anaweza lakini wakati taifa lina tatizo la ajira watu wameajiriwa mara mbili wanajulikana bado serikali inafanya uchunguzi sisi Wawakilishi tuelewe nini? Kila mtu hapa katika Jimbo lake ana tatizo la walimu, na wafanyakazi kuna wengine wana ajira mbili serikali inajua bado mnachunguza tuelewe nini? Mhe. Mwenyekiti mimi ninasikitika sana .

Na mimi niwaombe Kamati ya ustawi kwamba waelewe hili ni tatizo watu wako Mamlaka, yuko Suza, yuko Zenji FM mtu mmoja ana sehemu tatu hii nchi gani tunayokwenda hivi? Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani Mhe. Waziri nimuombe sana awasiliane na Mnadhimu wa Serikali uwasaidie watamuharibia kazi wakati yeye mwenyewe mimi naamini kwamba nia anayo lakini kuna jambo linamkwaza, mimi nimefanya utafiti kuna jambo linamkwaza. Sasa hatuwezi kumuharibia kazi Waziri wakati kuna watu wanalindwa makusudi mtu mmoja yuko Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, yuko Mamlaka, yuko Zenji FM tutakwenda wapi katika nchi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti Waziri nimemwambia mmoja yuko Zanzibar halafu huyo huyo ni jeshi hatuwezi kwenda hivyo, Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani Mhe. Waziri alifuatilie ni jambo ambalo halipendezi, watu wanakosa ajira wakati wengine wana ajira tatu Mhe. Mwenyekiti. Mimi nadhani tuendelee lakini Mhe. Waziri hili suala alifanyie kazi na tukijaaliwa mwakani tukifika sio kwamba kuachishwa kazi tu basi fedha ambazo zimetumika kwa ajili ambayo si sahihi basi fedha zirejeshwe. Mimi sitaki nimsumbue Mhe. Waziri na sina nia mbaya juu yake lakini kwa nini tufanye hivi? Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti ninamheshimu sana Mhe. Waziri lakini kwa masikitiko makubwa naomba nieleze kwamba jana wakati nachangia hapa kwa masikitiko makubwa sana nilimwambia kwamba kuna hoja kongwe kuhusiana na kutolipwa fidia kwa wale wakulima ambao mashamba yao yalipisha ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji. Ni ahadi aliyoichukua miaka mingi sana hadi hii leo haijatekelezwa. Sasa ni lini serikali itamalizia kuwalipa kwa sababu wameanza kuwalipa kidogo lakini muda umekuwa mwingi ni lini watawamalizia malipo yao?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Saleh Mkereketwa suali lake kwamba kwa kweli ni muda mrefu amelizungumza suala hilo na huko tulikotoka kulikuwa kuna matatizo ya yale makisio yaliyofanywa kuwa yamevimbishwa yametiwa hamira yamekuwa makubwa mno, wahusika tukawarejesha kiasi ya mara tatu, hatimae tukapata makisio yaliyokuwa *very reasonable.* Mheshimiwa tumelipa 50 *percent* ya ile gharama ya fidia, kuna matatizo kidogo madogo madogo katika makisio yaliyobakia ameniambia tumwambie tutayalipa lini? Tarehe, siku siwezi kuitoa lakini nataka nimthibitishie kama ananiamini kwamba mimi ni mkereketwa mwenzake naomba kumthibitishia katika bajeti ya mwaka huu pesa hizi tutazipata na tutalipa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Sina haja sana ya kupingana na mkereketwa mwenzangu lakini kubwa ni ahadi hii ameichukua na akumbuke kama huu ni mwezi wa Ramadhani na sitaki niseme kwamba hakusema kweli amelipa asilimia 50 lakini mimi baada ya kuzungumza nao wale wahusika wamenambia ni chini ya asilimia 50. Sasa sijui ukweli uko wapi baina Mhe. Waziri na hawa wahusika. Lakini naomba sana katika hili ahadi ameichukua mbele ya Baraza katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, na kwa sababu ameshaniahidi sana nyuma na bado hajamalizia, kwa hivyo naomba atekeleze hiyo ahadi kusudi hii dhima inatoka kwa watu na kwa Mwenyezi Mungu vile vile. Tuendelee.

Kifungu 1407 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar 2,300,000,000
Kifungu 1408

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nataka kuweka *hansard* yangu vizuri hapa Mhe. Waziri nilichangia suala hili lakini hakupata muda wa kunijibu sitaki nimlaumu lakini mimi ninachotaka kufanya hapa kwanza nishukuru sana kutokana na Mwenyekiti wa Bodi na Kamati yake na kutokana na wingi wa maombi ya watu 1,000 watu ambao wanataka mikopo kwa kwenda kusoma katika elimu ya juu, lakini Mheshimiwa mimi naomba sana hapa nielekeze Serikali, na kwa kuwa mwenyewe Makamu wa Pili yupo hapo, ningeomba sana hapa Mheshimiwa paengezewe pesa kwa wingi sana na kutokana na kasma wanayopewa hawa ni kidogo na watu wanakuwa ni wengi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili, kwa kuwa sisi tuna fedha zetu na za Muungano kule na mara hii sijajua kiasi gani tumetiliwa katika fedha hizi, ningemuomba sana Makamu wa Pili *at least* angeniazima Uwaziri kwa dakika tu ili kwenda kuchukua zile fedha zetu nikaweza kumsaidia Mhe. Shamuhuna, leo tunampigia mabuti kumbe fedha zenyewe hana na kule fedha zimebaki. Kwa hiyo naomba *message* yangu imefika kwa Mhe. Makamu wa Pili aniazime Uwaziri kwa dakika tu niende nikazichukue ili niweke haki sawa.

Kifungu 1408 Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu 9,113,000,000/=
Kifungu 1409

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumza kwa hisia kali kidogo suala la mitihani, na ninaizungumza mitihani ya kidato cha nne na cha sita, ambacho katika kitabu cha Waziri yote yamejumuishwa chini ya fungu hili la Baraza la Mitihani Zanzibar katika ukurasa wa 64 na 65.

Mhe. Mwenyekiti, nilipozungumza, nilizungumza kwamba katika usahihishaji wa mitihani mwaka jana baada ya kuonekana kumetokea tatizo la Tanzania nzima, ilipokuwa la Zanzibar peke yake tuliambiwa ni la kawaida, lakini mwaka jana baada ya kutokea tatizo kote kote kukafanywa uchunguzi, na namshukuru sana katika kujibu hoja yangu hii Mhe. Waziri, Mhe. Ali Juma Shamuhuna, kasema neno zuri sana, kasema kwamba wanafunzi wetu walifelishwa. Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, kwamba ukitizama hizi ripoti za awali za muhutasari tulizozipata katika uchunguzi uliofanyika inaonesha mambo mawili.

Mhe. Mwenyekit, jambo la kwanza hakuna utaratibu unaoeleweka wa alama yaani maksi za kupasishia baina ya masomo tafauti na viwango tafauti, halafu baina ya masomo hayo hayo kila mwaka wanabadilishwa yaani kile kiwango,

mwaka huu unaweza ukauongeza maksi tatu katika alama A mwaka ukapunguza maksi tatu katika alama hiyo hiyo A, mwakani katika alama B ukaongeza maksi mbili na mwaka huu ukapunguza, hakuna uwiano katika usahihishaji mitihani. Lakini pia katika masomo tafauti umeonekana kiwango cha mtihani kinabadilishwa, kwa hiyo pengine mwaka huu ninapaswa nifanye kazi zaidi nipate A na wakati mwaka jana nilifanya kazi ndogo zaidi kwa sababu kila mwaka NECTA inabadilisha viwango hivi bila ya kushauriana na Zanzibar kama alivyokiri Mhe. Shamuhuna, lakini vile vile katika hali ambayo inawafelisha watoto wetu, inawakomoa na hiyo inaonekana kuna mpango maalumu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ni mchango wangu wa mwisho ninataka nitoe mfano mmoja tu. Imedhihirika katika somo la dini ya Kiislamu na somo la biblia viwango vinachezeshwa tafauti ili kuwafelisha wanafunzi wa kiislamu. Mheshimiwa ushahidi huu hapa ninao.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, haja yangu nini? Mfano humu somo la kiislamu na biblia, lakini katika ripoti inaonesha masomo mengine yote *Geography, Physics, Civics* na waraka mwengine huu unaonesha vile vile Mheshimiwa, sasa huku ni kuwatesa na kuwadhalilisha, sasa huku ni kuwatesa na kuwaonea watoto wetu wanaofanya mitihani halafu ikawa matokeo yake wanakuja kufelishwa, sasa hoja yangu hili tunasubiri ripoti yake? Na nilitoa hoja hapa na nasikitika sana kuna mkubwa mmoja wa Serikali labda uanagenzi wake jana kavamia hoja hata hakuielewa akasema labda sijui Mwakilishi labda anataka ashirikishwe yeye, mimi sikuzungumza habari ya kushirikishwa mimi, nime- *appreciate* na nika-*acknowledge* kwamba Mwakilishi katika Baraza hili kashirikishwa nikasema ripoti ile tuijue.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni kwamba moja tuambiwe hii ripoti sisi Wawakilishi itatufika lini? Kwa sababu tumetoa Mwakilishi humu kwenda kutuwakilisha tunahitaji kujua matokeo yake, kwa sababu huu mwaka huu vile vile pia tutafanya mitihani tena hilo moja, la pili katika hoja hiyo Mhe. Mwenyekiti, nataka nisaidiwe Waziri au Wizara au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla wake imejipanga vipi ili suala hili lilijitokeza mwaka juzi na mwaka jana lisijirejee tena katika wanafunzi watakaofanya mitihani kama hii kwa mwaka, ili ufelishwaji wa makusudi wa wanafunzi kama inavyoonekana katika ripoti hizi usionekane tena.

Mheshimiwa wanafunzi wetu wanahangaika usiku na mchana kutafuta masomo. Naomba majibu ya hoja zangu mbili moja kuhusu ripoti, pili kuhusu hili suala kwamba halitorejea mwaka huu na ichukuliwe hatua gani ili kurekebisha suala hili lisitokezee tena kwa mwaka huu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, suala la ripoti nimeshasema na naomba nirejee tena. Hili suala ni la Waziri Mkuu ndiye aliyepewa jukumu la kuunda Tume na Tume Kaunda. Wawakilishi wa Zanzibar walikuwemo, tumefanya *investigation* wamepita nchi nzima na ripoti imeandikwa. Sema hivi sasa hivi ripoti hatujakabidhiwa sisi Wizara, ripoti kakabidhiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kakabidhiwa mwenyewe *Prime Minister* na juzi kakabidhiwa Makamu wa Pili wa Rais.

Kwa hiyo ripoti hizi zipo katika baina ya watu hawa watatu, bila ya shaka itateremshwa chini, na ikiteremshwa chini ikifika Wizara ya Elimu naahidi Wajumbe wote wa Baraza hili mtapata kopi ili katika Kongamano la Kitaifa tupate nafasi nzuri ya kuyazungumza mambo hayo, na hili ndio linajibu hili suala la pili ili tufanye hili lisijirudie tena.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichukua juhudi ya kupita kama nilivyosema Wilaya zote kumi, nikazungumza na wadau wote wanaohusika na suala la elimu na mitihani, wame-*appreciate* mazungumzo yangu, nitarudi tena sasa kuzungumza na walimu wangu wakuu na walimu wa madarasa nchi nzima ili tujipange vizuri zaidi katika kutoa jibu ya hilo alilozungumza Mhe. Jussa la pili, tufanye nini ili isije ikatokea tena.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimthibitishie Mhe. Jussa na Wajumbe wa Baraza hili suala hili kwa sasa hivi lililetwa suala la mtambuka, kufeli au kutofeli mtihani wanafunzi wetu tumekusanya mambo mengi likiwemo uchache wa walimu, wameshaizungumza *syllabus* inatakiwa kufanywa mapitio hii, imeshazungumzwa na vifaa vya maabara na kadhalika skuli zetu hazikutumia, bado yote tunazungumza hayo, haya yanachangia katika watoto wetu kufeli au kupasi. Unapokuwa na skuli imekamilika maabara, walimu, vitabu na kila kitu mtoto hafeli atapasi kama mengine kayaweka sawa, yepi hayo. Tumezungumza sana kuhusu maadili, tumewatupia wanafunzi hawana maadili, tumewatupia walimu nao hawana maadili ni kweli, tabia tulizokuwa nazo sisi tukazipa jina kuchimba, maana kusoma sana maana yake kuchimba, sasa haipo.

Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa Beit el Ras kule tunazuiliwa mpaka saa nne taa zinazimwa ambapo sisi tupo madarasani, basi wakitoka tu tunaendelea na kazi zetu za kusoma. Madarasa ya wanafunzi wetu wa siku hizi ni mtandao, taarifa za habari ovyo ovyo, matelevesheni ovyo ovyo na kadhalika. Lakini niliwahi kusema hapa na nasema tena, matatizo ya kubadilisha utaratibu kama alivyozungumza Mhe. Jussa, leo maksi zitakuwa hivi, kesho utaratibu utakuwa huu, kesho kutwa utakuwa huu bila ya kuambizana tukaelewana, bila ya kuandaa wanafunzi wetu, bila ya kuandaa walimu wetu inatakiwa tuwe makini sana watoto kufeli mtihani.

Palikuwa na suala mimi huwa najiuliza wanafunzi hawa wamefeli wamelishwa, ni kwamba nilikuwa nauliza watoto wetu wamefeli mitihani au mitihani imewafelisha watoto wetu? Nafikiri baada ya uchunguzi wa ile Kamati ya *Prime Minister* tumegundua kwamba watoto wetu wamefelishwa na mtihani sio wamefeli mitihani, hapana, yakapitiwa yaliyopitiwa maksi zikabadilika na hazikubadilika kwa upendeleo zimebadilika kwa kutenda haki, viko vingi lakini nataka nikitaje kimoja tu.

Mhe. Mwenyekiti, mwanafunzi keshafanya mtihani keshamaliza unamgeuzia utaratibu wa maksi za kusahihisha mitihani yake, alivyozowea yeye 50% ni maksi za mtihani na 50% za maksi za kawaida, leo ghafla unamwambia hapana 70% ni mtihani na 30% ni za kawaida, huyu mtoto ameshafanya huo mtihani, huku ni kumfelisha na hilo lipo tumeliona, na katika marekebisho yaliyofanywa ni hayo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana sana na *concern* na Mhe. Jussa juu ya hili, nakubaliana 100% wala sio 90% wala 99% ni 100%, lakini jibu lake la hili suala la pili tufanye nini ili haya yasitokee tena Mhe. Jussa, tutalipata kwenye Kongamano na hiyo ndio imenipa moyo mkubwa zaidi sasa kupata *Professor* wangu wa SUZA kuhakikisha kwamba Kongamano linafanywa mapema iwezekanavyo. Katika Kongamano pia Mtambuka wote tatizo liko na tutapata jawabu, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nizungumzie hoja zangu mbili, ya kwanza kwa ufupi sana nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri, lakini kwa maelezo yake mwenyewe amesema kwamba ripoti ya uchunguzi hii amepitishiwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano, amepitishiwa Waziri Mkuu na amepitishiwa Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawajibika kwa pamoja katika Baraza hili, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yumo ndani ya Baraza hivi sasa katika Kamati hii ya Matumizi, sasa bado mimi ningeomba yeye atusaidie Serikali imepanga lini ripoti hii kutufikishia sisi Wawakilishi ambao tunawawakilisha wananchi hao wanaopiga kelele watoto wao kila siku kufelishwa, tupate majibu hilo moja, ningeomba anisaidie Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ni kuhusu sababu zilizopelekea wanafunzi kufanya vibaya katika mitihani mimi mwenyewe katika mchango wangu nimezizungumza nyingi, na nikaukosoa mfumo mzima wa elimu, kwa hivyo nazijua, hapa nimeziacha zote nazungumzia hoja moja makhsusi ya utendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani NECTA na watungaji sera waliokuwa upande

wa pili ambao wanafanya maamuzi bila ya kushirikisha Zanzibar katika mkakati ambao naamini pia una lengo la kufelisha makusudi. Mhe. Mwenyekiti, ili nisitumie muda mrefu kama aliotumia naomba nitoe mifano michache tu naomba unistahamilie.

Mhe. Mwenyekiti, chukulia kwa mfano nnaoutoa huu baina ya masomo mawili haya yote sawa sawa ya dini, katika elimu ya dini ya kiislamu alama A inatolewa kuanzia 81-100, lakini kwenye elimu ya biblia 80-100 unaweza ukaona ni maksi moja tu, lakini inaamua kwamba umepata A au B. Katika kiwango cha B elimu ya dini ya kiislamu ni 70-80 lakini kwenye biblia ni maksi 65-79 hebu una tafauti, kwenye alama ya C kwenye dini ya kiislamu ni 60-69 ndio umefaulu umepata C lakini katika biblia asilimia 50-64 mfano mdogo tu Mheshimiwa huo. Lakini isije ikatafsirika labda ni masomo ya kidini tu hata haya masomo mengine, huu ni mfano ambao wenyewe waislamu wameandikia barua baada ya kufanya uchunguzi wao.

Mhe. Mwenyekiti, katika maksi nyengine somo kama *Geography* mwaka 2010 ili upate A imeongezwa maksi tatu kutoka mwaka 2011 na 2012 zimepunguzwa. Somo la *Chemistry* limeongezwa maksi 5 ili kuweza kupata A, ili kupata B pameongezwa maksi 5, ili kupata C maksi 5, lakini mwaka uliofuata zikapunguzwa mbili kwenye B zikapunguzwa 4 kwenye C. Sasa huu mfumo hauna ulinganifu wa kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, sote sisi tumesoma, tuliposoma katika kile cheti chako hakibadiliki kwa wanafunzi wote huku nyumba kimeandikwa A ni 80-100 hivyo hivyo kwa masomo yote, B kwa mfano ni 56-79 ilikuwa tukielewa hivyo, sasa utaratibu huu Mhe. Mwenyekiti, kwamba kila mwaka mtu akiamua tu kama Ndalichako sijui ndio nani huko akaamua tu haya ndio yanaleta matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninachokizungumza ninataka Mhe. Waziri katika hili anisaidie haya Kongamano tunalisubiri, na Kongamano tukifanya mwaka huu Mheshimiwa pengine matokeo yake na kukalia sera inaweza ikafika mwakani, mwaka huu ukifika mwezi wa Oktoba na Novemba wanafunzi wetu watakaa tena katika mitihani kufanya, je haya yamefanyiwa kazi na Wizara ya Elimu kwamba haya hayatajirejea kwa mwaka huu, ndio ninataka jawabu hilo, la kongamano nasubiri, nataka jawabu kuhusu hilo kwamba wanafunzi wazee wao wanajikhini ili kusomesha watoto wao, haya ya kufelishwa makusudi hayatowakuta mwaka huu, Wizara imechukua hatua gani kuhusu hili, nataka jawabu hilo. Kwa hiyo naomba tena Mhe. Makamu wa Pili anijibu kuhusu ripoti na Mhe. Waziri anijibu kuhusu mitihani.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, bado ninaendelea kumshukuru Mhe. Jussa na safari hii nasema kwa ufupi sana, suala hili ni la Mtambuka linataka kuchangiwa na watu wengi. Ukituambia Wizara tutafanya nini ili hili lisije likatokea tena mwakani, kweli ni jukumu letu Wizara na najua nakubali. Sisi narejea tena tutafanya Kongamano na tutawaalika wadau mbali mbali akiwemo Mhe. Jussa, na watu kama Mhe. Jussa wenye namna ya uwezo wa kuchambua haya mambo watusaidie, tukishapata jibu tutafanya utaratibu na kuhakikisha haya hayatorudia tena, lakini ukituachia peke yetu ukituuliza suala na mimi Mwenyezi Mungu keshanipa baraka na keshanipa uwezo wa kuitisha kongamano kutafuta wadau mbali mbali wakachangia mimi sioni tena la kuongeza katika hili, tusubiri kongamano tuchangie, tena tutachangia mengi hata wale wa kufunika kombe mwanaharamu apite tutachangia maana tuko peke yetu. Mhe. Jussa, niamini kwa hilo.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa kwa kuwa muda wetu unakaribia kwisha na kazi yetu iliyoko mbele yetu haijamalizika tunamuomba Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweke utaratibu ili tuendelee na shughuli zetu mpaka tukimaliza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshelezi kumaliza shughuli iliyo mbele yetu, hivyo naomba Baraza lako tukufu kuweka muda wa kanuni kando ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja Baraza lako likubali kuongeza muda mpaka pale ambapo tutamaliza shughuli iliyo mbele yetu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Elimu

niongezee masuala kidogo ya nyongeza inayotokana na hoja ya Mhe. Jussa. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane na Mhe. Jussa, aliyoyaeleza ni ushauri mzuri na kwa kuwa ni wajibu wetu kama Serikali kuhakikisha vijana wetu wanafanya kazi nzuri ya kujitahidi katika masomo yao wanapata maksi zinazostahiki ili ziwasaidie wao na isaidie nchi kwa jumla. Kwa hivyo ni kweli anavyosema upo umuhimu wa kuchukua kila jitihada kuhakikisha kwamba mambo haya yaliyojitokeza hayajitokezi tena.

Kwa hivyo, ninataka nimhakikishie Mhe. Jussa, licha ya jitihada zinazochukuliwa na Wizara na Serikali kwa ujumla wake italiona zaidi jambo hili na umuhimu wake na kutokana na ushauri ulioutoa ili tulifanyie kazi kwa kina tuepukane na matukio kama haya yasiweze kujirejea tena, na vijana wanapofanya mtihani basi wote wapate fursa iliyokuwa sawa ili waweze kupata matukio yaliyostahiki kwa kazi waliyoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la ripoti ni kweli ripoti iliwasilishwa kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini wakati hiyo ripoti inawasili ni siku ile ambayo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikuwa anasafiri nje kwa kweli kwenye matibabu, na ni jana tu ndio amerejea kutoka matibabuni nataka nimuhakikishie Mhe. Jussa, kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuipitia ripoti hiyo na wiki ijayo itafikishwa katika Wizara ya Elimu ili wenzetu wa Wizara ya Elimu waweze kuifanyia kazi kwa sababu ni jambo muhimu na lenye maslahi kwa watoto wetu na nchi yetu.

Kwa hiyo tutafanya kila jitihada ifike kwa wakati ili wenzetu waifanyie kazi vizuri na matokeo yake tutamjuilisha kwa ukamilifu Mhe. Jussa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, niliposimama awali kabisa nilikwambia kama nilikuwa na mabuti 22, lakini nikayapunguza yakabakia mawili tu. Nilikuwa na vifungu vya matumizi vingi nivihoji lakini vyote nimeviacha kwa sababu moja tu, na hata katika kufanya majumuisho Mhe. Waziri, nilimwambia kwamba haina haja kufanya majumuisho kwa sababu ya kuokoa muda wa Baraza na mimi sitaki nimchoshe. Lakini hata katika hili ukaniona nimelisimamia kwa umakini kwa sababu hili linagusa maisha ya watu wetu.

Ninakumbuka mwaka juzi na mwaka jana na mwaka huu lilivyotikisa nchi wazee walivyokuja juu. Sasa Mhe. Waziri, katika majibu yake kasema funika kombe mwanaharamu apite.

Mhe. Mwenyekiti, katika historia ya nchi hii alikuweko bwana mmoja akiitwa Sheikh Abdalla Suleiman Al Harthy, alikuwa Rais wa *Arab Association* huyu,

sasa kiswahili kidogo kilikuwa na matata matata akaambiwa kwa lugha ya Kiswahili *funika kombe mwanaharamu apite*, akasema ya nini funika, funua! Sasa na mimi leo nimeamua kufunua pamoja na kwamba ninakijua Kiswahili nimeamua kufunua ndio nikayaleta haya.

Sasa Mheshimiwa hoja yangu ni kwamba natafautisha vitu viwili, ninataka nieleweke vizuri sana, kwanza kuhusu ripoti nimesharidhika na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwamba wameipokea karibuni na wataifikisha Wizara ya Elimu halafu tutaletewa, bila ya shaka kuna hatua ambazo itachukua muda huko.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema mimi ni kwamba ninapata tabu sana kukubali na naona nikikubali ni sawa na kuidhalilisha Serikali yetu kwamba baada ya matukio kama haya na madudu haya niliyoyaeleza hapa ambayo haya Serikalini yapo, kwamba iwe tunangoja ripoti hiyo mwaka huu tutapofanya mtihani watoto wetu katika mwezi wa Novemba iwe Serikali haijakaa kutafakari kwamba angalau, kwa sababu lile Baraza la Taifa la Mitihani si la Tanganyika mpaka sasa hivi linaitwa Baraza la Taifa la Mitihani, na mpaka sasa bado ni chombo cha Muungano, sisi Zanzibar tunapaswa kuwa na kauli sawa kama waliyonayo Tanganyika katika chombo kile.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni kwamba hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo wananchi wa Zanzibar ndio wameipa imani na wameipa amana ya kusimamia maslahi yao, hivyo katika hili baada ya kupigwa dafrau mara mbili katika kipindi cha karibuni iwe haina hatua ilifikia angalau ya kuambiwa NECTA kwamba taratibu hizi wanazozifanya kwa mwaka huu zisitishwe, na kabla hatujafanya mitihani kama viwango vya kupasisha mitihani vinaeleweka, vimekubalika kwa pamoja basi hata hilo Serikali inashindwa kujibu tunaambiwa mpaka tungoje Kongamano, hilo dogo sana.

Sasa ikifika pale ikionekana kwamba Serikali hata hilo hawajajibu basi itakuwa tutakuja kusema kwamba Serikali hii imepoteza hata uhalali wake wa kufanya mambo yao, kwamba hata hili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar leo iwe haina kauli kuweza kuwalindia maslahi yao wananchi wa Zanzibar katika hili la kusimamia mitihani ya watoto wao wa kimaskini hawa ambao wazee wanajinyima kula yao, wanajinyima kila starehe yao ili kusomesha watoto wao angalau akinyanyuka huyu aje ajistiri yeye na familia yake, Serikali katika hili haina hatua ya pamoja ambayo imeiambia NECTA juu ya kulifanyia ufumbuzi. Bado ninataka ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kongamano nimelikubali la kusubiri ripoti nimelikubali, katika hili ninataka kuambiwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hii haina kauli yoyote kwa NECTA ambayo ni mbia, mwanahisa sawa sawa na

Tanganyika katika hili katika kukomesha mambo haya kwa mwaka huu wakati tunasubiri ripoti, siwezi kukubali Mhe. Mwenyekiti mimi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba ushauri wa maelezo ya Mhe. Jussa ulikuwa mzuri, nataka nimwambie Mhe. Jussa, na Waheshimiwa wa Baraza kwamba Serikali imeanza kulifanyia kazi jambo hili, licha ya kusubiri ripoti na hatua mbali mbali zinakuwa zikiendelea. Nataka nimuhakikishie Mhe. Jussa na Wajumbe wa Baraza hili kwamba, haya ambayo yametokea basi hayatoweza kutokea tena. Kama alivyosema sisi ni wadau tulio sawa na wenzetu katika jambo hili, kwa hivyo hatutoruhusu dhana ama tabia yoyote ile inayosababisha kwa watoto wetu kufeli au kwa Zanzibar kukosa haki zake.

Kwa msingi huo, nataka nimhakikishie Mhe. Jussa na wananchi kwa jumla kwamba mtihani utakaofanywa mara hii Oktoba au Novemba utafanywa kwa mashirikiano mazuri, kwa uwakilishi wa kutosha ambao serikali yetu itakuwa imetoa mchango mkubwa katika utekelezaji huo ili kuhakikisha haki ya kila mmoja inapatikana.

Hii ripoti kwa upande mwengine kabla ya kufikia kuchangiwa na wadau wengi tutakuwa tayari tumeona baadhi ya kasoro ambazo ndani ya serikali tutazifanyia kazi. Nataka nimhakikishie kwamba jambo hili serikali inalielewa imeanza kulifanyia kazi na italifanyia kazi vizuri zaidi ili vijana wetu wafanye mtihani bila ya kutokea kasoro ambazo zilitokea. Nataka nimhakikishie hilo na niwahakikishie wananchi wetu wote kwamba kasoro kama haitaweza kutokea tena na hatutoikubali kwa namna yoyote. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru kwa kauli ya serikali kutuhakikishia kwamba hili halitatokezea tena na nataka kuweka rekodi sawa tu, katika kumbukumbu zetu Mheshimiwa. Katika hili mimi wala simbebeshi lawama Mhe. Waziri wa Elimu swahibu wangu, kaka yangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna, kwa sababu katika Waziri ambaye katika hili namsifu ni yeye. Mara zote mbili ilipotoka hatua ya kupandisha viwango vya wanafunzi wanaotaka kuhalalishwa kufanya mitihani ya kidato cha sita Mhe. Waziri wa Elimu alisimama kidete kwa niaba ya Zanzibar. Lilipokuja hili katoa kauli halali, si kawaida kwa watendaji wetu kwa kuoneana muhali, katoa kauli hadharani akasema kwamba haya yamefanywa bila ya Zanzibar kushirikishwa na mimi sijui.

Kwa hivyo, nataka kuweka wazi kwamba simbebeshi lawama lakini nilisema nataka kauli ya serikali. Sasa nashukuru kwamba serikali imetoa kauli na ninachoiambia serikali kwamba, sisi Wawakilishi wa wananchi tunatizama yakija yakijirejea tena hayo baada ya kuwa serikali imeji-*commit* ndani ya

Baraza hili tutaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwajibike, kwamba itakuwa imeshindwa kusimamia maslahi ya wananchi wa Zanzibar katika vyombo vya Muungano. Nashukuru katika rasimu limeondolewa *Inshaallah,* labda itajipanga vizuri zaidi kufanya mitihani yake na naomba wajiandae tangu sasa. Lakini nategemea madhali bado katika kipindi hiki cha mpito bado liko pamoja basi nategemea kwamba kauli ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inasimama, na ikija ikitokezea vyengine humu ndani patakujakuwa hapatoshi katika kuiwajibisha serikali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nasema tuendelee ahsante sana.

Kifungu 1409 Baraza la Mitihani Zanzibar	1,570,000,000/-
Kifungu 1410 Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu	106,000,000/-
Kifungu 1411 Taasisi ya Elimu	100,000,000/-
Kifungu 1601 Idara ya Mafunzo ya Ualimu	250,000,000.-
Kifungu 1701 Idara ya Elimu ya Sekondari	

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, sina azma ya kuzuia fungu na kwa sababu kama nilivyotangulia kusema mwanzo kwamba Mhe. Waziri amefanya kazi kubwa katika Wizara hii. Isipokuwa nilipokuwa nikichangia niliwasilisha kilio changu kwa mara nyengine tena kuhusu walimu wa sayansi katika Skuli ya Sekondari ya Nyerere, skuli ambayo iko ndani ya Jimbo langu na watoto wangu ndio wanaosoma hapo.

Mhe. Mwenyekiti, wasanii wamesema, “Ukiona mtu mzima analia jua kuna jambo’. Kwa hivyo, jambo lipo ndio maana ninalia. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba, wapo walimu wawili wa sayansi na ukiangalia mazingira ya Skuli ya Sekondari ya Nyerere ambayo ina mikondo miwili kwa kweli sijui nisemeje, sijui nizungumze lugha gani. Pamoja na kwamba nafahamu kuna upungufu mkubwa katika eneo hili ambapo Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora alipokuwa akisaidia kujibu hoja tulimuelewa na akasema kwamba anataka kubadilisha utaratibu wa matangazo ya walimu, hasa wa sayansi ili matangazo ya nafasi za walimu basi yaelekezwe katika skuli inayohusika. Mimi nashukuru katika hilo na nampongeza kwa hatua hiyo huenda ikasaidia.

Lakini nilipokuwa nikichangia nilimwambia Mhe. Waziri kwamba atakapokuja kufanya majumuisho sasa anipe idadi halisi ya walimu wa sayansi aliyokuwa nao, ilikuwa lengo langu ni kuoanisha walimu wawili niliyoletewa na idadi ya walimu waliopo na mahitaji yaliyopo. Na kwa sababu kuna fununu kwamba kuna skuli nyingine nyingi hasa zilizoko katika maeneo ya mjini zina walimu wengi wa sayansi kuliko zile za ng’ambu ambazo

walimu wapo, wamerundikana huko lakini hawapelekwi ng'ambu. Jambo hilo lipo na nilitaka nijue juu ya jambo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hili kwa kuwa Mhe. Waziri hakupata nafasi muda ulikuwa mdogo basi namuomba aje anipe kwa maandishi juu ya walimu wale wa sayansi, si leo hata kama wiki ijayo, wale walimu wa sayansi aliyokuwanao ili nijiridhishe kwamba kweli tuna upungufu mkubwa katika walimu hao wa sayansi, nijiridhishe mimi mwenyewe. Na kwa sababu Idara ya Elimu ya Sekondari ndio yenye jukumu la kugawa hao walimu katika skuli zake mbali mbali, kwa kweli tunahitaji hiki kidogo tulichokuwanacho basi tugawane kidogo kidogo na tugawane kwa uwiano ndio utaratibu, haiwezekani kuna wengine wanafaidika zaidi wengine hawafaidiki, hawa wote ni watoto wetu na tunawategemea.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri katika hili nataka aje anipe orodha ya walimu wa sayansi na mahitaji yaliyopo katika skuli zetu, si leo siku yoyote ile akijaaliwa, lakini kabla ya bajeti kumalizika ili wananchi wajue na utaratibu ujulikane.

Lakini narudia tena kusema naupongeza ule utaratibu ambao Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma aliueleza hapa huenda ukatusaidia katika kuona mwalimu anaajiriwa katika eneo maalum na anaomba katika eneo maalum. Kwa hivyo, mimi nadhani tuendelee katika hili lakini hoja yangu ndio hiyo.

Kifungu 1701 Idara ya Elimu ya Sekondari 1,706,700,000/-
Kifungu 2001 Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hapa nilitaja Skuli moja ya Mapopwe Pemba, Jimbo la Gando ilikuwa na kilio cha kisima, watoto pale walikuwa wakipata shida ya maji na kuhangaika na mikebe yao. Mhe. Naibu Waziri alinijibu kuwa kisima hicho kinaendelea hivi sasa. Nilikuwa nataka kujua tu kisima hicho wanajenga wao Wizara ya Elimu au kuna mtu kajitolea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana, kisima hicho sio Wizara ya Elimu ambayo imetoa pesa ya fungu lake, isipokuwa Wizara ya Elimu imetafuta mfadhili na tuko katika hatua za mwanzo za kuhakikisha kisima hicho kinachimbwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba tu Mhe. Waziri baada ya kumaliza kisima hicho wakamuandikia barua ya pongezi mfadhili huyo Abdalla Msewe. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati jana nachangia nilizungumzia sana suala la hatimiliki za skuli pamoja na jinsi Skuli ya Ndagoni inavyomega shamba la marehemu Mzee Ayoub Suleiman ambapo watoto wake Suleiman Ayoub na wenzake wapo. Ardhi hii inachukuliwa na skuli ile bila ya kusikilizana na familia hii, bila ya makubaliano. Sasa nilikuwa nataka Mhe. Waziri pamoja na kwamba Mhe. Naibu Waziri alijibu kwamba ina hatimiliki, lakini kwa kweli lile shamba hiyo hatimiliki kama nilivyowaambia watu wa ardhi wameitoa kimakosa baada ya ushawishi wa baadhi ya wananchi wa pale kusema aah, acha tuchukue hili ni shamba la Waarabu bwana tutalimaliza lote; ile hatimiliki imetolewa kimakosa na wale warithi wa shamba wanayo hatimiliki yao *original*.

Sasa nilikuwa nafikiria kwamba ni hatua gani Mhe. Waziri ataweza kulitatua tatizo hili kwa sababu yeye ndiye mwenye dhima, ndiye anayeongoza hiki chombo, hatimiliki ile imetolewa baada ya baadhi ya wakaazi kujenga hoja kwamba lile shamba acha tuchukue tu. Mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri aende pale akakae na Suleiman Ayoub pamoja na wenzake wa lile shamba kama wanataka ku-*extend* ile skuli basi wafanye mazungumzo na sio kumega mega mashamba ya watu tu hiyo ni dhulma. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ni lini utakutana na ile familia ya Suleiman Ayoub na ndugu zake wale ili kuweka sawa juu ya shamba lao ambalo kila kukicha ardhi yao inachukuliwa kwa kujenga mabanda pamoja na uwanja wa mpira. Hata juzi wamekata miembe, minazi, mikangazi kwa ajili ya kujenga uwanja ni lini atakutana nayo familia ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nilijibu suala hilo na ni kweli Mhe. Saleh Nassor aliliuliza jana na kama ambavyo alitoa ushauri tumeuchukua kwa mikono minne, yangu miwili na ya Waziri wangu miwili, tukimaliza tu kwenye Baraza hili tutakwenda twende tukaonane naye huyo mzee kama huo waraka ulitolewa kimakosa tutajua, kama ulitolewa kiuhakika tutajua na hapataharibika kitu. Kwa sababu hatutaki kusimamia dhulma, leo tuko duniani tuna madaraka tuliyopewa kesho hatupo tutakwenda kuulizwa juu ya haki za watu. Kwa hivyo, tutakwenda tutazungumza naye na naamini penye wengi hapataharibika kitu, muafaka utapatikana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kutokana na hekima za Mhe. Waziri na Naibu wake nina hakika kwamba penye wengi hapataharibika neno. Kwa hivyo, mimi nitaendelea kufuatilia hilo nione kwamba kweli neno halitaharibika, lakini likiharibika tutakuja kukutana humu humu tena kipindi chengine. Baada ya maelezo hayo tuendelee.

Kifungu 2001

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumza kwamba kuna mwalimu katika skuli zilizopo katika Jimbo langu la Chambani alifariki tokea mwaka jana, hii ni bajeti ya pili. Lakini mpaka leo warathi wa marehemu yule bado hawajapatiwa mafao yao kupitia Wizara hii ya Elimu na sikupata maelezo yoyote ya Mhe. Waziri wala Naibu Waziri kwamba watu hawa ni lini watapewa mafao yao. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri anipe maelezo ya kina na lini watoto hawa mayatima watapewa mafao yao kupitia Wizara hii. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alipokuwa akichangia Mhe. Mohammed alilizungumzia suala hilo na ni kweli sikupata nafasi ya kumjibu, ni mmoja ya watu ambao hawakupata fursa ya kujibiwa katika suala hilo. Na nimwambie leo asubuhi hii nilizungumza na watendaji wangu wakanambia kwamba suala hili tayari liko mikononi na tayari Wizara ya Fedha washalikabidhi kwao. Kwa hivyo, mara tu tukimaliza hii bajeti suala hili litamalizika Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Nashukuru sana kwa maelezo ya Mhe. Naibu Waziri juu ya hili lakini ili niwe na umakini juu ya hili namuomba Mhe. Naibu Waziri anishirikishe katika kujua kwamba hizo hatua walizofika ili watoto hawa nijue vya kuzungumza nao juu ya umakini wa kupata haki zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, hakuna matatizo yeye ni Mwakilishi wa wananchi kwa hivyo tutamshirikisha.

Kifungu 2001 Idara ya Mipango na Sera Pemba	871,000,000/-
Kifungu 2201 Idara ya Utumishi na Uendeshaji Pemba	15,790,000,000/-
Kifungu 2301 Idara ya Elimu Pemba	81,055,000/-
Kifungu 2501 Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala Pemba	50,000,000/-
Kifungu 2801 Idara ya Mafunzo ya Ualimu Pemba	50,000,000/-
Kifungu 2901 Idara ya Elimu Sekondari Pemba	113,300,000/-
Kifungu 2902 Idara ya Teknolojia ya Habari Unguja	300,000,000/-
Kifungu 3001 Idara ya Teknolojia ya Habari Pemba	100,000,000/-
Jumla ya Fungu	**80,200,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia bajeti hii niliwasilisha maombi kwa Mhe. Waziri, lakini kutokana na ufinyu wa muda hakupata nafasi ya kulizungumzia au kulitolea maelezo lile ombi langu. Naamini kama angepata muda basi ombi langu angelikubali, na kwa sababu ya uzito wa ombi lenyewe na juu ya uungwana wa Mhe. Waziri angenikubalia.

Nilisema juu ya mradi huu wa uimarishaji wa elimu ya lazima ambapo kuna fedha zilizotengwa katika utekelezaji wake kiasi ya shilingi 18 bilioni ambapo katika utekelezaji wa bajeti hiyo inasema fedha hizi zitatumika katika kukamilisha ujenzi wa madarasa katika skuli nne za sekondari yaliyoanzishwa na wananchi. Pengine anayo maeneo mengine ambayo ametenga kwa ajili ya fedha hizo, lakini mimi kwa ghafla nimeona katika eneo hili.

Nilimuomba Mhe. Waziri kwamba kutokana na msongamano uliopo katika skuli ya Sekondari ya Nyerere, na kwa kuwa kuna banda ambalo tayari limeshakamilika kukabidhiwa Wizara ya Elimu ningeomba katika mwaka huu wa fedha katika mradi huu kwenye hizi skuli nne basi angalau Mhe. Waziri akubali kulimalizia lile banda ambalo limejengwa pale na kwa sababu ya msongamano uliopo, na kwa sababu ya wilaya hii kuwa haina majengo mengi mapya Wilaya ya Mjini, basi akubali alimalizie katika haya maeneo manne ambayo yamepangwa pamoja na kwamba limekuja mwisho kuliko mengine nakubali, ili tupunguze ule msongamano uliopo. Na *Inshaallah* kama atalikubali hili nataka kutumia nafasi hii kumualika katika sherehe za Elimu bila ya Malipo aje aliweke jiwe la msingi banda lile. Kwa sababu mwezi wa tisa tuna sherehe za kuadhimisha Elimu bila ya Malipo. Kwa hivyo, nimualike rasmi awe mgeni rasmi katika uwekaji wa jiwe la msingi la banda lile. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anipe majibu juu ya ombi langu ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alivyosema Mhe. Salmin juzi nilikuweko katika skuli yake nimeona msongamano walivyo watoto, lakini kwa kweli ile skuli hawajatukabidhi rasmi. Kwa hivyo, jengo lile Mhe. Salmin watukabidhi rasmi na mahitaji tunayajua ambayo mnahitaji tutawamalizia.

Kuhusu kumualika Mhe. Waziri kuja kuweka jiwe la msingi kaninong'oneza hapa kasema kakubali mualiko wako.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri hilo jengo kama Mwalimu Mkuu hajalikabidhi basi nitamwambia alikabidhi, kwa sababu tumelimaliza hivi karibuni, tumelijenga haraka haraka

kutokana na umuhimu wa matatizo yaliyopo. Kwa hivyo, nitamwambia Mwalimu Mkuu basi aandike barua ili aikabidhi rasmi Wizara ya Elimu na nimshukuru Mhe. Waziri kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika sherehe ya uwekaji jiwe la msingi katika Sherehe za Elimu bila ya Malipo. Nashukuru tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti	19,147,160,000/-
Kifungu 0703 Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar	400,000,000/-
Kifungu 0801 Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi	

Mhe. Rufai Said Rufai: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba kuna mwalimu anakaimu karibu huu mwaka mmoja na nusu na zaidi katika Skuli ya Sizini. Na jana katika kujibiwa nimejibiwa masuala yangu mengi lakini katika kujibiwa suala hili sikupatiwa jawabu au sikulisikia. Kwa hivyo, naomba nipate jawabu yake rasmi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti: Hapa Kazi za Maendeleo kama unataka kujibiwa ujibiwe tu lakini sio pahala pake. Mhe. Waziri kwa faida ya Mjumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nitamsaidia Mhe. Rufai. Ni kweli alivyosema na tayari mapendekezo ya majina tushaletewa karibu tukimaliza bajeti tukikaaa kikao chetu basi baada ya muda si mrefu Mwalimu Mkuu atapatikana wa skuli hiyo hatakaimu tena.

Kifungu 0801	Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi	10,779,632,000/-
Kifungu 1201	Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala	2,029,906,000/-
Kifungu 1402	Chuo cha Kiislamu Pemba	100,000,000/-
Kifungu 1406	Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar	3,090,921,000/-
Jumla ya Fungu		**35,547,619,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha za Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale waliokubali bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2013/2014 wanyooshe mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa ushirikiano wenu wa tangu asubuhi hadi hivi sasa na kukubali kuongeza muda ili kumaliza kazi yetu, tunamshukuru Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri na pia nakushukuruni nyinyi kwa kuipitisha bajeti ya Wizara ya Elimu ili watoto wetu wapate kusoma. Baada ya hayo niakhirishe kikao chetu hiki hadi kesho tarehe 19/07/2013 siku ya Ijumaa saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 8:26 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 19/07/2013 saa 3:00 asubuhi)